

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

## BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Saba – Tarehe 6 Februari, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu kwa orodha ya shughuli za leo, ninapenda kwanza nimpongeze *Corporal Fauster*. Napenda niwafahamisheni, ni mara ya kwanza katika historia ya Bunge letu Spika kutanguliwa na *Sergeant-At-Arms* ambaye ni mwanamke. Tulikwishasema awali Bunge hili litaendeshwa kwa viwango na viwango ni pamoja na kuzingatia jinsia. Hakuna kazi ambazo ni za wanaume tu peke yao. Ahsante sana *Corporal Fauster*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimerejea, nimesitisha safari ya Marekani. Nalazimika kutoa maelezo kwa sababu ya maneno mengi tu. Safari ile kwenda kule ilipangwa kwa kuzingatia mambo mawili :- Moja, ni umuhimu tu wake. Wenzetu Amerika, wiki ya pili ya Mwezi Februari kila mwaka mihimili yote mitatu ya Dola wanakaa pamoja kwa mlo wa asubuhi, inaitwa *National Prayer Breakfast*.

Pamoja na mambo mengi yatakayofanyika, Rais wao ataongea pale kwenye *Prayers Breakfast*. Lakini wanawatambua baadhi ya viongozi mashuhuri ambao wana ushirikiano mwema nao. Mimi kama Spika wa Bunge hili, nilialikwa kwa msingi huo. Kwa hiyo, hoja kwamba labda ningeweza kumtuma mtu mwingine, haipo kwa sababu ni mwaliko wa heshima kwa jina. *(Makofi)*

La pili ni kwamba, nikitazama ratiba na Kanuni ya 24 ya Bunge, ilikuwa ni kwamba Miswada inaendelea na kwa hiyo, nilidhani mambo mengine kama vile taarifa za Kamati yangukuja kama ilivyo kawaida katika wiki ya mwisho, na mimi nilikuwa narudi Ijumaa asubuhi. Kwa hiyo, yote yangewezekana. Sasa hilo lilishindikana, niliwaarifu wenyeji wetu kule Marekani na wamesikitika, lakini wamesema kama wanasiasa, wameelewa, kwa sababu niliwaeleza mazingira ambayo yalinifanya nisiende.

Nashukuru kwamba katika ujumbe wangu yuko Mheshimiwa Nyarandu, yeye yuko Marekani ataendelea na zile shughuli nyingine ambazo ni za kawaida akituwakilisha Bunge letu, kwa sababu msafara wangu ulikuwa wa Waheshimiwa Wabunge wawili; Spika na Mbunge mmoja.

Sasa, kwa nini nimerudi? Maana yake nalo linaulizwa, mbona yuko Naibu Spika! Ndugu zangu Wabunge kwa dhati kabisa nasema, tafsiri za mambo haya tukizichukua kwa ubinafsi zinaleta matatizo. Mimi nina imani kubwa sana na Naibu Spika wetu. Ni mchapa kazi mzoefu na kwa hakika amebobea zaidi katika Bunge la vyama vingi kuliko mimi kwa sababu mimi nilikuwa Mbunge wakati wa chama kimoja. Nathamini sana ushauri wake na kila siku tunashauriana.

Namwomba radhi kwamba nilitumia neno kukurupuka! Limetumika na wengi kuchafua tu hali! Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba radhi, mbele ya Wabunge na mbele ya wananchi kwa sababu neno hili limeanza kutumika kutuondoa kwenye ajenda muhimu za taifa ambazo ndiyo wananchi wametutuma hapa. Kwa hiyo, jana nimemwomba radhi kwenye Kamati ya Uongozi na leo nimemwomba radhi hadharani. Sikuwa na maana mbaya. Tafsiri kwamba yeye ni mtu wa kukurupuka si kweli, tunashauriana na hata sababu ya kurudi ni yeye mwenyewe aliponiarifu matokeo ya Semina ya Jumapili, tarehe 4 mwezi huu. Ningekuwa Spika wa ajabu, niende nchi za nje wakati kwa namna fulani, “nyumba inaungua”. (*Makofi*)

Narejea tena, narejea hapa Bungeni si kwa sababu sina imani na Naibu Spika, au hata wenyeviti. Narejea, kwa msingi wa utawala bora wa uwajibikaji, mimi ndiye Spika. Mimi ndiye niliyeitamka hiyo Kamati Teule kwa majina, nikawapa na hadidu za rejea. Chini ya Ibara ya 84 ya Katiba, mwajibikaji Mkuu katika mambo ya Bunge ni Spika. Spika, ambaye yakitokea mambo magumu, atajificha uvunguni, hafai! (*Makofi*)

Kwa hiyo, nimerejea kwa sababu hoja ya leo nataka niisimamie mwenyewe. Sasa anayetaka kusema mengine, shauri yake. Nimerejea kwa sababu hiyo tu. Kwa sababu kama ingekuwa ni miswada ya kawaida, hakuna haja. Lakini kwa hili, naliona ni zito na ni zito kwa sababu semina isingevunjika Jumapili na kwa sababu tuna mawasiliano mazuri, ilionekana dhahiri kwamba ni muhimu niweze kuvunja safari na kuwa hapa na ninyi. (*Makofi*)

Bada ya hayo, jana Kamati ya Uongozi, tulizingatia kwamba tuanze na taarifa hii ya Kamati Teule ya Mchakato wa Zabuni ya Kuzzalisha Umeme wa Dharura – *Richmond Develeopment Company ya Houston*. Tulikubaliana kitu ambacho kumbe hakiwezekani. Tulikubaliana kwamba ingewezekana Mwenyekiti wa Kamati akaweka mezani, halafu shughuli zote ziahirishwe. Nimeshauriwa kisheria kwamba hilo haliwezekani na sina mamlaka hayo. Kwa hiyo, itabidi baada ya kuwasilisha kwa maana ya hati kuwekwa mezani baada ya matangazo, itabidi nimwite Mwenyekiti aweze kuwasilisha hoja yake. (*Makofi*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI.**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI TEULE – (MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA):**

Taarifa ya Kamati teule ya Bunge iliyochunguza Mchakato wa Zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura uliipa ushindi *Richmond Development Company LLC* ya *Houston, Texas* – Marekani, 2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 88

**Barabara toka Sanya Juu – Mowo**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kwa kushirikiana na Serikali imeanza kujenga daraja la Lima na Siki na lile la Mese kwa kushirikiana na *TANAPA*; na kwa kuwa barabara itokayo Sanya Juu kwenda katika vijiji vya Mowonjamu, Nsherehehe na Ngaronyi ina hali mbaya sana na hivyo kutopitika wakati wa mvua:

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi wa barabara hiyo hasa ikizingatiwa kuwa wananchi wa vijiji nilivyotaja ni wakulima wa mazao kama kahawa, ndizi, maharage na kadhalika.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia yenye urefu wa kilomita 8 ni mojawapo ya barabara ambazo zipo chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

Barabara hii inahudumia vijiji vya Mowonjamu, Nsherehehe na Ngaronyi. Kijamii barabara hii ni muhimu kwa kuhudumia taasisi mbali mbali zikiwemo shule za msingi 4, zahanati 2 na shule za sekondari 2. Kiuchumi, barabara hii inatumika kwa kusafirisha mazao ya biashara na chakula yakiwemo madini, maharage, ndizi na kahawa.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara hii si ya kuridhisha na inahitaji matengenezo. Matengenezo yanayohitajika ili kuifanya ipitike ni ukarabati mkubwa. Gharama ya kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe ni shilingi milioni 208. Kutokana

na uwezo mdogo wa kifedha wa Serikali na Halmashauri kwa ujumla, barabara hii haijaweza kufanyiwa matengenezo kwa kiwango kinachohitajika.

Hata hivyo ujenzi wa madaraja ya Lima na Siki umekamilika. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Hai katika mwaka wa fedha uliopita wa 2006/2007 ilitenga kiasi cha shilingi milioni 3.2 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi yenye urefu wa kilomita 3.2. (*Makofi*)

Kwa mwaka wa fedha 2007/2008 barabara hiyo ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 41.69 kwa ajili ya matengenezo. Matengenezo haya yamekwishafanyika na wananchi wanapita sehemu hii bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali itajitahidi kuendelea kuzifanyia matengenezo barabara zake kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu. Hata hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Hai inashauriwa kuendelea kushirikiana na wananchi wake kuifanyia matengenezo madogo madogo ili barabara hiyo iweze kupitika kwa muda wote wa mwaka.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninaomba nishukuru kwa majibu ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Pamoja na majibu hayo, ningependa kuuliza kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Wilaya ya Siha ni Halmashauri ambayo ni changa, ni mpya na Serikali inafahamu jambo hili. Kwa hiyo, suala la kuomba misaada kutoka Serikali Kuu haliwezi kukwepeka hapa.

Je, kama Serikali ilikubali ikatusaidia kuweka daraja la Siki na Daraja la Lima ambalo limechukua gharama sana; Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kusaidia katika barabara kwa sababu itakuwa na maana gani basi kuweka madaraja yenye gharama kubwa kiasi hicho *and yet* ikaonekana kwamba Serikali haiwezi kusaidia katika mpango huo?

Pili, kwa vile Serikali imekubali kwamba kweli eneo hili ni muhimu kwa mazao ya kahawa, mahindi na maharage na na mbao na vitu vingine; Serikali inadhani kwamba itafanya nini kutusaidia katika hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali ina nia nzuri tu ya kutengeneza barabara hii. Na kama nilivyoeleza kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inasafirisha mazao ya biashara pamoja na mazao ya chakula. Kwa hiyo, umuhimu wa barabara hii Serikali inautambua ndiyo maana inaweka mkakati wa kupanga fedha kila mwaka ili kuimarisha barabara hiyo.

Kwa mfano; kwa mwaka huu, bajeti nzima ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha ni shilingi milioni 200. Lakini kati ya fedha hizo, shilingi milioni 41 zimetengwa kwa ajili ya

barabara hiyo kutokana na umuhimu wake. Kwa hiyo, Serikali kama ilivyokuwa na nia nzuri kwa kujenga madaraja ya Lima na Siki na sasa hivi Serikali inajipanga kuangalia umuhimu wa barabara hii na kadri fedha zitakavyopatikana, barabara hii itapewa kipaumbele kama ilivyopewa kipaumbele kwa mwaka huu wa fedha.

Na. 89

### **Fidia kwa Nyumba Zilizovunjwa Kamwanga**

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojenga barabara ya Kamwanga iliwavunja wananchi nyumba zao na kusababisha kukosa makazi na mpaka sasa wapo wananchi ambao hawana makazi kabisa:-

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Kamwanga ambao wanasubiri fidia kwa nyumba zao zilizovunjwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Serikali ilipanga kujenga barabara kutoka Tarakea kupitia Rongai (Halmashauri ya Wilaya ya Rombo) hadi Kamwanga (Halmashauri ya Wilaya ya Longido) yenye urefu wa kilomita 32 kwa kiwango cha lami. Ujenzi huo ambao unafanywa na Mkandarasi wa Kichina, Kampuni ya *SIETCO*, ulianza kutekelezwa tarehe 25 Oktoba, 2004. Gharama za ujenzi wa barabara hiyo ilikadiriwa kufikia Tsh. 14, 418.4 bilioni fedha ambazo zinagharamiwa na Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa barabara hiyo, kuna baadhi ya nyumba za makazi na majengo ya kutoa huduma yaliathirika. Maeneo hayo yapo katika vijiji vya Mbomai na Kikelelwa katika Halmashauri ya Rombo na Kamwanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Serikali imefanya tathmini ya athari zinazotokana na ujenzi wa barabara hiyo kwa kuzingatia upana wa ujenzi wa mita 30 (*Construction corridor*).

Kazi ya uthamini huo ilishirikisha wananchi na viongozi wa maeneo yaliyoathirika na ujenzi huo. Idadi ya Kaya zilizoathirika na ujenzi wa barabara hii katika Kijiji cha Kamwanga ni Kaya 24 pamoja na Kanisa na Kituo cha Polisi. Jumla ya shilingi milioni 146.892 zitalipwa kama fidia kwa wananchi wa kijiji cha Kamwanga.

Aidha, jumla ya fidia kwa wananchi wote walioathirika na ujenzi wa barabara hiyo ni shilingi bilioni 1.6. Hivyo, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa utaratibu wa malipo unafanyiwa kazi ili wananchi walioathirika waweze kulipwa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nikupongeze sana kwa kukubali kuomba radhi kwa sababu ni viongozi wachache wa ngazi ya juu wanaothubutu kusimama Bungeni na kuomba radhi. Nakushurkuru sana! (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi hawa waliovunjiwa nyumba ni watu maskini sana na mpaka sasa hawana pa kuishi.

Je, Serikali itaharakisha fidia hiyo ili wananchi hawa waweze kupata maeneo ya kuishi hasa wengine wanaishi katika nyumba za jamii?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli maandalizi na kupata gharama kamili za fidia zimekamilika hivi karibuni na *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro imewasilisha karibuni Makao Makuu ya *TANROADS* gharama hizo. Juhudi zinafanyika ili fedha hizo au fidia hiyo ilipwe haraka iwezekanavyo.

Na. 90

### **Vyombo vya usafiri kwa Waratibu Elimu Kata**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa Waratibu Elimu wa Kata wanafanya kazi katika mazingira magumu sana ya kukosa vyombo vya usafiri na kwa kuwa Serikali ina utaratibu wa kuwakopesha watumishi wake vyombo vya usafiri kama vile pikipiki, magari na baiskeli na kadhalika:-

- (a) Je Serikali ina sababu gani za msingi za kutowakopesha Waratibu Elimu Kata, vyombo vya usafiri?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuwakopesha watumishi hao pikipiki kutawasaidia sana katika utekelezaji wa majukumu waliyonayo kuliko ilivyo hivi sasa?

- (c) Je, ni Waratibu Elimu wa Kata wangapi wamekopeshwa vyombo vya usafiri hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la ukosefu wa usafiri kwa Waratibu Elimu Kata na Maafisa Ugani wengine wanaofanya kazi vijijini jinsi linavyoathiri utendaji kazi wa kila siku wa Maafisa hao. Aidha, Serikali ingependelea kuona Waratibu Elimu Kata wakiwa na vyombo vya usafiri kama pikipiki na baiskeli ili iwe rahisi kwao kusimamia shughuli zote za Elimu katika Kata zao.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina nia ya kukopesha Waratibu Elimu Kata vyombo vya usafiri, hata hivyo katika mwaka huu wa fedha, mpango huo haukujumuishwa katika Bajeti za Halmashauri nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kutokana na ufinyu wa Bajeti na ukosefu wa fedha. Ni imani yangu kwamba hali ya fedha itakapokuwa nzuri Serikali itatimiza adhema yake hiyo japo kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea kusubiri utekelezaji wa nia hiyo ya Serikali Waratibu Elimu Kata na Maafisa Ugani wengine walio katika Halmashauri za Wilaya, Jiji, Manispaa na Miji wanashauriwa kukopa aina ya vyombo vya usafiri kupitia Makampuni yanayotoa mikopo ya vyombo hivyo kama *Tanzania Schools Equipment (TASEQ)* ambao wameonyesha nia ya kukopesha pikipiki kwa walimu kwa riba nafuu.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kuwa Serikali haikuwa na mpango wa kukopesha Waratibu Elimu Kata pikipiki huko nyuma hivyo hakuna takwimu zozote zilizopo za Waratibu Elimu Kata ambao wamekopeshwa vyombo hivyo vya usafiri.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Waratibu Elimu Kata na Walimu ndio wanasimamia taaluma katika shule zetu; na kwa kuwa ili kuboresha taaluma katika shule zetu iko haja kuhakikisha kwamba hawa Waratibu Kata na Walimu wote kupatiwa usafiri ili waweze kuboresha taaluma hasa kwa suala la ufuatiliaji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba iko haja sasa ya kuwapatia vitendea kazi kama vile Wizara ya Kilimo inavyofanya kuwapatia vitendea kazi Maofisa Ugani wake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kabisa kwamba ili kuboresha elimu, lazima kuwe na vitendea kazi vya kuridhisha ili hao Waratibu Elimu

Kata waweze kufuatilia kazi yao vizuri katika Kata zao. Lakini Serikali inafanya hivyo kwa awamu ndio maana utakuta kwamba kwa mwaka 2007/2008 Wizara ya Kilimo wenzetu wamejitahidi kuweka kwenye Bajeti yao kuwanunulia Maafisa Kilimo pikipiki ili waweze kurahisisha kazi.

Pia upande wa Serikali Kuu, Makatibu Tarafa nao wana vyombo vya usafiri. Kwa hiyo, Serikali inajipanga kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuhakikisha kwamba vitendea kazi hivyo vinawafikia walengwa. Ni nia ya Serikali kabisa kwa dhati kuhakikisha kwamba vitendea kazi vinapatikana kwa watendaji wetu wa Kata, wa Wilaya na kadhalika. Wizara ya Elimu pia imejitahidi, sasa hivi wana mpango wa kuwanunulia Waratibu wa Elimu za Sekondari vifaa vya kazi. Hizo zote ni jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba watendaji wetu wanapata vifaa hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waratibu Elimu Kata pindi Serikali itakapokuwa na uwezo, nina uhakika kwamba tutawasaidia na wenyewe. Tatizo lao tumeliona, tunajipanga ili kuona kwamba tutawasaidia namna gani.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa Naibu Waziri wakati anajibu swali la msingi amezungumzia uhaba wa fedha; na kwa kuwa baadhi ya watendaji wakuu wa Wizara mbali mbali wamekuwa na vyombo vingi vya usafiri, vingine vya ziada. Je, isingekuwa vizuri sasa kupunguza baadhi ya vyombo vya usafiri katika baadhi ya Wizara na kuvishusha vyombo hivi vingine ili kusaidia ngazi hizi za chini ziweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo?

**SPIKA:** Majibu! Nilidhani Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezesaji. Kumbe anatoka tu! (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya Wizara ambazo zina vyombo vya ziada. Sasa hivi kuna zoezi linalofanyika chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi kuangalia ni Wizara zipi ambazo zina vyombo vya ziada ili viweze kushuka huko chini. Kwa hiyo, zoezi hili linaendelea. Kama kuna mahali kuna vyombo vya ziada vitashuka chini. Lakini, kama vyombo vinatosheleza, Serikali itazidi kujipanga ili kuwasaidia hao watu wa chini waweze kupata vyombo hivyo. Hata hivyo, ningependa kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo vizuri kwa Wizara ambayo imeishatumia gari, limechakaa, halafu tunawapelekea wenzetu wa chini. Ni vyema, tukawapatia vyombo vipya ambavyo vitadumu kwa muda mrefu zaidi.

Na. 91

**Hatua za Kinidhamu kwa Askari Waliomtesa Msichana Mdogo**

**MHE. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-



Je, ni hatu zipi za kinidhamu zilichukuliwa dhidi ya Askari waliomtesa sana na kutaka kumbaka msichana mdogo (Ndugu Alice Nahumu Saria) mnamo tarehe 25 Agosti, 2007 bada ya msichana huyo kutuhumiwa na aliyekuwa mwajiri wake (Ndugu Sia Evans Lyimo) kuwa amemwibia shilingi laki nne, (400,000/=) na kumpeleka kituo cha Polisi Mabatini – Kijitonyama ambako aliamuru huyo binti ateswe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujajibu, napenda kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote kukupa pole kwa kufiwa na mtu wa karibu sana, dereva wako na hasa ukizingatia kwamba kifo chenyewe kilikuwa ni cha aina ya ukatili mkubwa. Lakini, pia kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, napenda kukupongeza kwa jinsi ulivyoonyesha utu na ubinadamu, ukashirikiana na familia mpaka dakika za mwisho. Ahsante sana! (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA NA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nipokee shukrani za dhati kutoka kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge na namwombea Marehemu mahala pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, napenda kutoa maelezo ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Afisa yeyote wa Polisi wakati anatekeleza wajibu wake wa msingi wa kuzuia na kupeleleza uhalifu, kulinda na kudumisha amani na usalama wa jamii kulingana na sheria, kanuni na haki za binadamu kwa kuzingatia Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu katika swali Na. 107 katika Mkutano wa Tisa wa Bunge lililoulizwa na Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, endapo Askari yeyote wa cheo chochote atagundulika kufanya kazi na huku akikiuka taratibu na maadili ya kazi yake atachukuliwa hatua za kinidhamu kulingana na kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi (*P.G.O*) na *Police Force Service Regulations*, ikiwa ni pamoja na kushitakiwa Kijeshi. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokelewa kwa taarifa ya malalamiko ya Bi. Alice Nahumu Saria, dhidi ya Askari Polisi hao wawili wa Kituo cha Polisi cha Kijitonyama, Dar es Salaam jalada lilifunguliwa ili kufanya uchunguzi wa malalamiko hayo. Baada ya uchunguzi kukamilika Askari wawili walifunguliwa mashtaka ya Kijeshi ambapo Bi. Alice Nahumu Saria aliiitwa kutoa ushahidi wake. Kwa sasa shauri hilo liko katika hatua za Hukumu. Iwapo itabainika Askari hao kutenda makosa hayo watastahili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kimbita swali la nyongeza pamoja na tahadhari kwamba jambo hili sasa linashughulikiwa na mahakama

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hiyo. Ni kwamba hili swala linashughulikiwa na mahakama ya Kijeshi lakini lilishahukumiwa katika mahakama ya mwanzo ya Kinondoni na huyu binti kuonekana kwamba ana hatia na kuhukumiwa miezi 18 kuripoti Ustawi wa Jamii Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na hatua zilizochukuliwa ni kitendo kilichomdhalilisha sana huyu binti mdogo baada ya kutuhumiwa na kupelekwa Polisi Kijitonyama mabatini, alifinywa chuchu zake kwa *plies* na mateso mengine na kupigwa. Kinachosikitisha ni kwamba Mkuu wa kile Kituo ni mwanamke, Mkuu wa Upelelezi katika kile Kituo ni mwanamke lakini walishuhudia haya mateso mabaya kwa huyu binti mdogo. Kwa nini baada ya mimi kufika kituoni na kulalamika kwa yule mkuu wa kituo hakufanya jitihada zozote mpaka nilivyoleta swala hili katika Bunge hili?

Swali la pili Mheshimiwa Spika ni kwamba; je, Ofisi ya Mwanasheria Mkuuwa Serikali itakuwa tayari kufuatilia mwenendo mzima wa kesi hii ya unyanyasaji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kimbita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taarifa za mateso ya kijana huyo hazikuwahi kutufikia Wizarani kwetu; na kwa kuwa Kituo hiki cha Polisi kilificha taarifa hizi, ndiyo maana Wizara haikufahamu. Lakini mara tu baada ya kufahamu taarifa hizo Wizara ilichukua hatua zinazofaa na ndiyo maana utaratibu wa kisheria ndani ya Jeshi la Polisi utachukuliwa na hivi sasa itakapobainika kwamba mateso haya yalitokea kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba hivi sasa kama nilivyosema hatua ziko katika mahakama ya kijeshi na baada ya hukumu ya mahakama ya kijeshi hatua za kisheria zitafuata baada ya hapo.

**MHE. KABWE Z. ZITO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Nafahamu kwamba toka *IGP* mpya ameteuliwa, kumekuwa na maboresho katika Jeshi la Polisi lakini kesi za wananchi kuteswa kabla hawajafikishwa mahakamani na vituo vya Polisi ni tatizo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu na linaendelea sana; je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na swala la Polisi kutesa wananchi kabla hawajawafikisha mahakamani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba askari yeyote haruhusiwi kumtesa ama kumwonea mtuhumiwa yeyote yule. Ni kinyume na taratibu za sheria na pale inapojulikana kwamba askari huyu amefanya makosa ya aina hii hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yake, na hivi sasa kuna operesheni maalumu ndani ya jeshi la polisi kuchunguza askari wote ambao wanakwenda kinyume na utaratibu wa kanuni za Jeshi la Polisi na pia tumeanzisha utaratibu wa semina mbalimbali kuwafahamisha askari kufanya wajibu wao kwa mujibu na utaratibu wa utawala bora. Hivi sasa tuna Kamati Maalumu za maadili ndani ya Wizara kufuatilia mambo haya, kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua kali zitachukuliwa dhidi ya askari wanaotesa raia kinyume cha utaratibu. *(Makofi)*

Na. 92

### **Kuboresha Kituo cha Polisi cha Kibakwe**

**MHE. GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE** aliuliza :-

Kwa kuwa kituo kidogo cha Polisi cha Kibakwe ni muhimu sana kwa sababu kinahudumia eneo kubwa la Jimbo la Kibakwe; na kwa kuwa eneo hilo lina matukio mengi ya uhalifu yakiwemo ya ujambazi, wizi wa mifugo na kujinyonga:-

(a) Je, ni lini kituo hicho kitawekewa umeme?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutokuwapatia askari wa Kituo hicho usafiri angalau wa pikipiki kunazorotesha ufanisi na pia kuhatarisha usalama wa askari wanaofuatilia matukio ya uhalifu kwa usafiri wa baiskeli na kutembea kwa miguu.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu :-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama na Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo :-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuweka umeme katika vituo vya Polisi hapa nchini kikiwemo Kituo cha Polisi cha Kibakwe kilichopo Wilaya ya Mpwapwa. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Jeshi la Polisi imekuwa vigumu kutekeleza mahitaji yote kwa wakati mmoja. Lakini nia ya Serikali ya kuweka umeme katika vituo vya Polisi hapa nchini kikiwemo cha Kibakwe ipo palepale na itaendelea kutekelezwa kwa awamu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kuwapatia askari Polisi vitendea kazi ikiwemo magari na pikipiki. Aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti na mahitaji makubwa ya vitendea kazi Serikali inashindwa kutoa mahitaji yote kwa wakati mmoja.

Hata hivyo, Serikali itaendelea kulipatia jeshi la Polisi vitendea kazi kadri ya uwezo wa fedha wa Serikali utakavyoruhusu. Kwa kutambua hilo Serikali tayari imepeleka gari moja aina ya *Landrover 110* na pikipiki moja kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mpwapwa ili kuimarisha shughuli za doria, misako na huduma nyingine katika eneo lote la Wilaya ikiwemo Kibakwe, Chipogoro, Rudi na Mtera.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza askari polisi kwa kuendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kwa ujasiri mkubwa na uzalendo wa hali ya juu. Serikali itaendelea kuongeza bajeti yake ya kila mwaka ili kulipatia jeshi vitendea kazi kwa nia ya kuboresha utendaji wao wa kazi.

**MHE. GEORGE B.SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nimshukuru tena kwa sababu pikipiki tayari imeshafika Kibakwe, lakini nina swali dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu tangu Kituo cha umeme cha Kibakwe kilichojengwa kwa nguvu za wananchi tangu kimeanza kufanya kazi; na kwa kuwa wakati mwingine nyakati za usiku askari wanapata matatizo kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika; je, Wizara itawasaidia vipi askari hawa kuondokana na shida hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia naomba kumjibu Mheshimiwa Simbachawene swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Simbachawene kwamba tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba umeme katika Kituo kile cha Kibakwe unapatikana katika muda si mrefu kuanzia sasa.

**MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA:-** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa tatizo la Jimbo la Kibakwe linafanana kabisa na tatizo la Jimbo la Lulindi ambalo ni kubwa katika Wilaya ya Masasi je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwa na kituo kingine cha Polisi katika Jimbo la Lulindi ambako wakati mwingine wananchi wanalazimika kwenda katika Wilaya nyingine ya Newala

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kumchaya kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba upo umuhimu wa kuwa na Kituo kingine katika Jimbo la Lulindi na hata tathmini ya Jeshi la Polisi iliyofanywa katika kuangalia utaratibu mzima wa kuweka vituo vya Polisi nchini inaonesha umuhimu huo upo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kumchaya kwamba hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba tunajenga Kituo cha Polisi katika Jimbo lako lakini kama unavyojua uwezo wa kifedha na mahitaji haya ni kwa nchi nzima, lakini tutahakikisha kituo kinajengwa katika eneo hilo.

**SPIKA:** Ili nitende haki siwezi kuiacha Zanzibar. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MOHAMMED RAJABU SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa suala la umeme wa Kibakwe linalingana na suala la Polisi Ziwani ambako utakuta jengo zima lenye familia zaidi ya nne wanaishi pamoja na wanatakiwa walipe umeme kwa mita moja, Mheshimiwa Waziri naomba atusaidie ili kutupa maelezo tuweze kupata ufafanuzi wa tatizo hili ambalo ni kubwa

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Rajabu Soud, kama ifuatavyo:- Lipo tatizo la malipo ya umeme katika Kambi ya Ziwani lakini nataka nimhakikishie kwamba limepata ufumbuzi, Jeshi la Polisi litalipia malipo ya umeme kwa wale wote ambao wanakaa katika Kambi za Polisi nchini.

Na. 93

### **Kesi za Uchaguzi**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza :-

Kwa kuwa baada ya uchaguzi wa mwaka 2005, kuna kesi nyingi ambazo zilifunguliwa na wagombea wa Ubunge:-

- (a) Je, ni kesi ngapi zilifunguliwa;?
- (b) Je, ni kesi ngapi zimeshapatiwa ufumbuzi?
- (c) Je ni kesi ngapi bado hazijapatiwa ufumbuzi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Hamis Juma, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Ni kesi 33 zilizofunguliwa baada ya uchaguzi Mkuu wa Disemba 2005;
- (b) Kesi 32 zimepatiwa ufumbuzi kutoka majimbo yafuatayo ya uchaguzi:- (1) Mbulu; (2) Arusha; (3) Babati; (4) Simanjiro; (5) Same; (6) Moshi Mjini; (7) Vunjo; (8) Moshi Mjini; (9) Moshi Vijijini; (10) Muheza; (11) Kilindi; (12) Handeni; (13) Korogwe; (14) Ubungo; (15) Chalinze; (16) Kibaha; (17) Kigoma Mjini; (18) Kasulu Mashariki; (19) Geita; (20) Mwibara; (21) Tarime; (22) Musoma Mjini; (23) Bukoba Mjini (24) Biharamulo; (25) Mpanda; (26) Nkasi; (27) Namtumbo; (28) Namtumbo; (29) Tunduru; (30) Songea; (31) Kilwa Kusini; (32) Mtwara Mjini; (33) Kwela; (34) Maswa.

(c) Kesi ambayo bado ipo Mahakamani na inasubiri maamuzi ni ile ya Karatu. Kesi bado inaendelea kusikilizwa na tunategemea itapatiwa ufumbuzi ndani ya kipindi cha miezi sita.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Naibu Waziri naona amenitajia tu kuwa ni majimbo fulani tu hakunifafanulia kwamba ni Jimbo gani uchaguzi umetenguliwa; hakunieleza, amenijibu tu kifupi, nataka kujua ni majimbo mangapi ambayo uchaguzi wake umetenguliwa na ikiwa yapo uchaguzi huo utafanyika lini?

(b) Kwa nini kesi ya Karatu inacheleweshwa sana? Nataka kufahamu.

**SPIKA:** Sina hakika, naona hili linahitaji takwimu nyingi sana kufafanua majimbo 32, lipi imekwenda vipi na lipi limekwenda vipi. Mheshimiwa Naibu Waziri unadhani na hili la sijui kuchelewesha Karatu hilo si swali la Serikali ni la Mahakama? Nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri ungetulia tu maana yake mambo haya yamekaa si sawasawa.

Na. 94

### **Matumizi ya Makaa ya Mawe**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, makaa ya mawe ni chanzo muhimu na rahisi cha kuzalisha umeme :-

(a) Je, Serikali inajua kuwa Namwale kuna makaa ya mawe ya kuweza kuzalisha umeme na kupikia kwa kipindi cha zaidi ya miaka 200 ;

(b) Je, mwekezaji Mtanzania aliyeanzisha juhudi hizo atasaidiwa vipi na Serikali hasa katika kumuunganisha na kampuni toka nchi zilizoendelea katika matumizi ya makaa ya mawe kuzalisha umeme.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sera ya Taifa ya Nishati inatambua umuhimu wa kuongeza wigo wa vyanzo vya kuzalisha nishati ya umeme kwa ajili ya kupunguza utegemezi wa umeme wa maji. Mojawapo ya chanzo kinachopewa kipaumbele ni makaa ya mawe, hata hivyo, tathmini ya wingi wa makaa hayo pamoja na ubora wake inabidi kufahamika

kabla ya kuanza uchimbaji. Aidha, miundombinu ikiwemo ya barabara, reli, maji, madaraja na ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme kwa ajili ya kuunganisha kituo cha kuzalisha umeme kwenye gridi ya Taifa hupewa kupaumbele katika tathmini nzima ya ubora wa mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inafahamu kuwepo kwa makaa ya mawe huko Namwale Mkoani Rukwa tangu miaka ya 1940 ulipofanyika utafiti wa kijiolojia uliofanywa na *geological Survey Department* ya Tanzania kwa kushirikiana na shirika la *Colonial Development Corporation*. Utafiti huo ulibaini kuwepo na mashapo tani milioni 7.8 ya makaa ya mawe huko Namwale. Hiki ni kiasi kidogo ukilinganisha na Songwe Kiwira yenye mashapo yafikayo tani milioni 140, Mchuchuma tani milioni 199 na Galula iliyoko Rukwa tani milioni 140. Serikali inakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wanaopenda kuwekeza katika makaa ya mawe ya Namwale na maeneo mengine ya nchi ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 kifungu Na. 5, mtu au Kampuni yoyote kabla ya kuanza kujishughulisha na shughuli za Madini inalazimika kuwa na leseni inayoruhusu kufanya shughuli hizo, hivyo, tunamshauri mwananchi mwekezaji wa Kitanzania anayeanzisha juhudi za kuendeleza makaa ya mawe ya Namwale pamoja na wananchi wengine wenye azma kama hiyo waombe leseni. Kama maeneo atakayoombea leseni hayako chini ya leseni zilizowahi kutolewa atapatiwa leseni.

Mheshimiwa Spika, iwapo eneo atakaloomba litakuwa ndani ya leseni iliyotolewa kabla, tutamshauri aingie makubaliano ya ubia na mmiliki wa leseni. Baada ya kumiliki eneo kisheria itamlazimu kufanya kazi mbalimbali za kijiolojia na kijioteknolojia na kisha kuandaa taarifa za kitaalamu za madini ambazo ataweza kuzitumia kuvutia wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi. Taarifa hizo zitajumuisha wingi na ubora wa mashapo yaliyopo katika eneo lake na taarifa ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ina taarifa kwamba Bwana Kasiano Kaengele anayemiliki kampuni ya *Upendo Group* ana nia ya kuendeleza mradi wa kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe huko Namwale. Katika jitihada za kufanikisha azma hiyo mwezi Novemba, 2005 alifika ofisi ya *TANESCO* – Mkoa wa Rukwa kutoa taarifa, tena tunamshauri Bwana Kaengele na kampuni yake wafuate utaratibu nilioulezea. Aidha, tunamkaribisha Wizarani kwetu kwa ajili ya ufafanuzi zaidi kama atapenda kufanya hivyo.

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Waziri amesema kwamba utafiti wa kwanza wa kijiolojia ulifanyika mwaka 1940, atakubaliana na mimi kwamba utaalamu wa kutafuta madini hayo hayo wa mwaka 1940 ni tofauti na utaalamu uliopo sasa, na hivyo taarifa hizi hazawezi kuchukuliwa kama

ni taarifa sahihi; je, anajua pia kwamba *Norwegians* walifanya utafiti wa mara ya pili mwaka 1974 na kugundua kwamba *deposit* ya madini ya makaa ya mawe iliyopo pale ni tani milioni 28,000?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunakubali kwamba kutokana na mabadiliko ya teknolojia taarifa za miaka ya 1940 kwa vyovyote vile zitakuwa zinaweza kutofautiana na taarifa kama vile ambavyo Mheshimiwa Dr. Mzindakaya alivyosema za mwaka 1974 au hata za hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, nataka niliarifu Bunge hili Tukufu kwamba shughuli ya utafiti inafanywa kama tulivyosema na wananchi ambao wana nia ya kufanya shughuli za madini katika maeneo mbalimbali. Kinachofanyika, ama Serikali inachofanya ni kuwawezesha wananchi wenye nia hiyo kuwapa maeneo hayo kwa kuwapa vibali kwa maana ya leseni kwenda kufanya shughuli hizo kama tunavyofahamu sera yetu ni ya kushirikisha sekta binafsi. Kwa hiyp, tunaamini kwamba endapo watajitokeza watu wa kuwekeza ama kufanya utafiti wa kiwango cha mashapo kwa kiwango cha sasa hatimaye ikaonekana kwamba yanaweza kuchimbwa kibiashara. Tunakaribisha na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi Serikali haina pingamizi na hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ofisi yetu kimsingi ndiyo inayoratibu takwimu. Tunakubaliana na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya kwamba yawezekana kuna taarifa zingine lakini kwa taarifa ambazo zipo ofisini kwetu napenda kumkaribisha Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili tuendeleo kuzifanyia kazi pamoja na pengine kuona kama kuna wawekezaji wengine kuweza kuendeleza eneo hilo.

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mbali ya Namale na Mchuchuma kuna taarifa kwamba sehemu nyingi Tanzania makaa ya mawe yapo; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inatafuta wawekezaji; na kwa vile tuna matatizo makubwa ya ukosefu wa umeme kwa muda, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza ni kwa nini kwa muda wa miaka yote hiyo hatujapata mwekezaji wa sekta hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ningependa kutoa ufafanuzi huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kuna vyanzo vingi vya aina mbalimbali vya umeme ambavyo vinaweza kutatua matatizo yetu ya umeme humu nchini kama Mkoa wa Rukwa swali ambalo ameliuliza Mheshimiwa Dr. Mzindakaya. Tunatambua kuna matatizo makubwa ya umeme kwa sababu ule unaotoka Zambia hautoshelezi, kwa hiyo, hiki kingekuwa chanzo kizuri cha kuwa na umeme, na ndiyo sababu katika taarifa zetu baada ya matatizo kumalizika ndiyo tunapendekeza sheria mpya kusudi kuwaruhusu watu kama bwana Kassian Kaengele ambao wana nia ya kuwekeza katika vituo hivyo walindwe kisheria. Katika kufanya hivyo ndiyo sababu tunapendekeza hii Sheria ya kuruhusu watu binafsi kuwekeza katika sekta hii. (*Makofi*)



**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. *TANESCO* ilikuwa na *corporate plan* ya miaka mingi kutoa umeme kutokana na maji ambayo ndiyo rahisi sana kuliko aina yoyote duniani ya utoaji umeme. Na katika *corporate plan* yao ilikuwa wakishamaliza Kihansi waende Lukali ambako kungetoa karibu megawati 400. Baada ya hapo waende Luhuji ambayo yote hii ilikuwa ni ya kutoa umeme kutokana na maji; je, Serikali imebadili msimamo wa kusema badala ya kwenda kwenye umeme wa gharama rahisi wa *Hydro* sasa twende kwenye umeme wa gharama kubwa wa makaa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Malecela, kama ifuatavyo:-

Tunatambua kwamba umeme unaotokana na *hydro* ndiyo umeme wa gharama za chini kabisa kama alivyozungumza Dr. Malecela. Na tunatambua kwamba kulikuwepo na *master plan* ya zamani kama tulivyozungumza ambayo inaendelea kufanyiwa mabadiliko na ndiyo sababu mwaka jana wakati wa kipindi cha Bajeti tulitangaza kwamba sasa hivi tuna-*update* ile *power master plan* yetu ambayo kwa *programme* yetu ni kwamba ripoti ya mwisho inabidi kuwa imemalizika mwezi huu wa pili. Na tumekwishapata hiyo *draft* ripoti, tukipata nafasi tu tutaitoa katika Bunge lako Tukufu ambalo linaainisha vyanzo hivi kama ilivyoviangalia, lakini hiyo ripoti inaangalia *load focused*, mahitaji ya sasa tuliyonayo na ya baadaye na chanzo gani kiingie katika gridi yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa hivi vyanzo vingine ambavyo tumevisema vya makaa ya mawe, upepo, *biogas* ni vitu ambavyo vinahitajika kwenye maeneo ambayo tunayaita *off grid* ambayo yako mbali na gridi ya Taifa ambayo si rahisi kuingiza ndani gridi ya Taifa bila kutumia gharama kubwa. Kwa hiyo, tunaangalia vyanzo vyote vya umeme tulivyonavyo na uwezekano wake na unafuu wake wa kuwahudumia wananchi, vile ambavyo vipo karibu na gridi vinawekwa, vile ambavyo viko mbali na gridi vitakuwa vinaitwa *offgrid* na vitatumia chanzo ambacho wanacho pale.

**SPIKA:** Samahani Waheshimiwa Wabunge, kwa utamaduni wa Mabunge ya *Commonwealth* anaposimama Kiongozi wa Upinzani inabidi nimtambue kwa kweli. Swali la mwisho!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa ziko kampuni za *IPTL*, *SONGAS* na kadhalika; je, Waziri anaweza kulieleza Bunge hili zinavyotumika? Katika majibu yake amesema tunahitaji sheria mpya, je, ni sheria gani imetumika kwa haya makampuni ambayo tayari yapo *IPTL* na *SONGAS* hivi sasa?

**SPIKA:** Naliruhusu tu kwa sababu linatokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi Kampuni zote ambazo zinazalisha umeme hapa *IPTL*, *SONGAS* hata *ATMAS* ambayo

inazalisha megawati kidogo, *DOWANS, AUSTRUM* zote zinazalisha kwa kuiuzia *TANESCO*, hazizalishi na kujisambazia zenyewe. Kwa hiyo, zinafanya kazi kwa mkataba ambao kwa kiwango kikubwa, na Waheshimiwa Wabunge mmelizungumzia na Serikali imesikia, kwamba mtindo wa namna hii kwa kuzalisha na kuiuzia *TANESCO* una mzigo sana kwa *TANESCO* na ndiyo sababu tunataka kuondokana na hilo tuwe na utaratibu mwingine zaidi ya kuzalisha umeme na kuiuzia *TANESCO*.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, bado tupo Wizara ya Nishati na Madini. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Paschal Degela ingawa kabla hajauliza niliposoma swali hili nikawa naona kama vile Vijiji vinavyotajwa viko Rungwe lakini basi ndiyo nchi yetu, Mwailanje, Mwaikisabe. (*Kicheko*)

Na. 95

### **Ukosefu wa Umeme – Mwailanje na Mwaikisabe**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Soya Wilayani Kondoa kilipatiwa umeme kupitia mradi wa *Electricity IV*; na kwa kuwa Vijiji vya Mwailanje na Mwaikisabe viko jirani sana na Kijiji cha Soya:-

- (a) Je, kwa nini Vijiji hivyo havikuunganishwa katika mradi wa *electricity IV*?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani kwa sasa wa kuvipatia umeme Vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Ni kweli kuwa Kijiji cha Soya kilicho jirani na vijiji vya Mwailanje na Mwaikisabe katika Wilaya ya Kondoa kilipatiwa umeme kupitia mradi wa *Electricity IV*. Mradi wa *Electricity IV* ulitekelezwa kwa fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Kabla ya kutekelezwa kwa mradi wa *Electricity IV* ulifanyika upembuzi yakinifu uliokuwa na lengo la kubaini Vijiji vilivyokuwa na sifa za kupelekewa umeme pamoja na gharama halisi za kupeleka umeme katika Vijiji vilivyoonekana kuwa na sifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu uliofanyika kabla ya mradi kuanza ulionesha kuwa kwa wakati huo Vijiji vya Soya na Hamai vilikidhi sifa za kupatiwa umeme ikilinganishwa na Vijiji vya Mwailanje na Mwaikisabe. Ndiyo maana licha ya

Vijiji vya Mwailanje na Mwaikisabe kuwa karibu na Kijiji cha Soya havikuweza kupatiwa umeme chini ya mradi *Electricity IV*.

(b) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Mwailande kimepangwa kupatiwa umeme chini ya mradi wa *Millennium Challenge corporation (MCC)*. Jumla ya shilingi milioni 317 zitatumika kupeleka umeme katika kijiji hicho kutoka kwenye laini kubwa (*high tension*) ya umeme wa kilovoti 33 iliyopo takriban kilomita 8 katika Kijiji cha Soya.

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Mwaikisabe hakikuwekwa katika mradi wa *MCC*. Upelekaji wa umeme katika kijiji hicho kutokea Mwailande utatekelezwa kupitia wakala wa Nishati Vijijini. Gharama za kupeleka umeme katika Kijiji cha Mwaikisabe kutokea Mwailande ambapo ni takriban umbali wa kilomita 12 kwa sasa zinakadiriwa kufikia shilingi milioni 724.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ahadi yake ya kupeleka umeme katika kijiji cha Mwailande kupitia mradi wa *MCC*.

(a) Kwanza naomba nifahamu huu mradi wa *MCC* ambao utatumika kupeleka umeme Mwailande utaanza lini?

(b) Kwa kuwa Meneja wa *TANESCO* Wilaya ya Kiteto alianza mradi wa kupeleka umeme katika shule ya Sekondari ya Soya ambayo ipo katika Kijiji cha Soya; na kwa kuwa ameshindwa kuendelea na mradi huu kutokana na ukosefu wa vifaa; je, Wizara itasaidia vipi ili kuweza kupata vifaa haraka ili shule hiyo ya Sekondari ya Soya iweze kupatiwa umeme haraka? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Degera Mbunge, kama ifuatavyo:-

La kwanza, kama ambavyo Wizara/Serikali yetu imekuwa ikiliarifu Bunge hili Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba ufadhili kupitia Mfuko wa *MCC* kwa miradi mbalimbali Tanzania mazungumzo yameshafikia naweza kusema kiwango cha juu, na kinachofanyika sasa hivi kwa kweli kinachosubiriwa ni fedha tu. Niseme kwamba imani yetu ni kwamba ndani ya mwaka huu miradi hii hasa ambayo kwa upande wa sisi wa Wizara ya Nishati na Madini kuhusu masuala ya umeme tunategemea kuianza baada ya kupata fedha hizi kutoka *MCC*. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuzidi kuwasiliana kwa sababu ni mradi mkubwa matarajio ni mazuri kwa maana ya kwamba ahadi hii tuna imani kwamba itatekelezwa na Serikali itafaidika sana kupitia mradi huu.

Kuhusu vifaa na hasa shule ya sekondari ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja wiki iliyopita tulijibu swali hapa tukielezea mipango ambayo Shirika letu la *TANESCO* limekuwa likifanya na limeshaagiza vifaa mbalimbali. Na kwa kweli matarajio yetu ni kwamba vifaa vingi vitakuwa vinaingia katika mikoa mbalimbali kutoka nje ya nchi ambapo vilikuwa vimeagizwa ndani ya mwezi huu. Kwa hiyo, tuna imani kwamba baada

ya vifaa kufika tuna imani kwamba pia mojawapo ya miradi ambayo itafaidika ni miradi ya Mheshimiwa Mbunge kama vile ambavyo amekuwa akifuatilia. Lakini tena tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ushirikiano ambao amekuwa akiuonyesha kwa Wizara yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kumpongeza Mheshimiwa Degera kwa kutukumbusha kitu kimoja muhimu sana ambacho ni hii miradi ya *MCC*. Tunatambua kwamba hivi karibuni tutakuwa na ugeni mkubwa wa Rais Bush hapa Tanzania na kati ya kitu ambacho anakuja kukifanya kikubwa ni kusaini miradi hii ya *MCC*. Kwa hiyo, tungependa Watanzania wamkaribishe wote na wananchi wa Kigoma ambao mwanzoni walikuwa wanafikiri sasa kwamba umeme kwao hautafika, huu ndiyo ukombozi baada ya kusaini mkataba wa *MCC*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tumekaa sana kwenye Wizara ya Nishati na Madini, naona tuendeleo.

Na. 96

**Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na  
luga za Bunge la Afrika Mashariki**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (K.n.y. MHE. ZUBEIR ALI MAULID)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa nchi za Rwanda na Burundi ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

(a) Je, ni lini sasa nchi hizo zitafanya chaguzi za Wabunge ili waungane na wenzao wanaotoka nchi za Tanzania, Kenya na Uganda katika Bunge la Afrika Mashariki?

(b) Kwa kuwa hivi sasa Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi katika shughuli za Bunge la Afrika Mashariki; je, ni lini Kifaransa nacho kitaingizwa kuwa lugha rasmi ili kusaidia nchi mbili za Jumuiya?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, (Mb.) wa Kwamtipula, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Kifungu Na. 48(1)(a) cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kimefanyiwa marekebisha na Nchi Wanachama ili kuruhusu Wanachama wapya kuwa na Wabunge katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Novemba, 2007, Mkutano wa Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliridhia marekebisha hayo.

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho awali kilitaja kuwa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki litakuwa na idadi ya Wabunge ishirini na saba kwa maana ya Wabunge tisa kutoka nchi tatu wanachama waanzilishi. Baada ya marekebisho hayo, kifungu hicho sasa kinabainisha kwamba kila Nchi Mwanachama itachagua Wabunge 9 wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo kutoa fursa kwa Wanachama wapya kuchagua Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtipula, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nchi za Rwanda na Burundi zitachagua Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya Nchi Wanachama waanzilishi wote kukamilisha zoezi la kuridhia marekebisho ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakayoruhusu wanachama wapya kuchagua Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(b) Mheshimiwa Spika, kifungu namba 137 cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kimeainisha kuwa lugha ya Kingereza ndiyo lugha rasmi itakayotumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba lugha ya Kiswahili imeelekezwa kama lugha ya mawasiliano (*lingua franca*). Wakati wa majadiliano ya maombi ya Nchi za Rwanda na Burundi kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi za Rwanda na Burundi zilikubali kwamba zitatumika lugha za Kingereza na Kiswahili baada ya kujiunga na Jumuiya. Hivi sasa Jumuiya ya Afrika Mashariki haijaanzisha mchakato wa lugha ya Kifaransa kuwa lugha rasmi wala kuwa lugha ya mawasiliano ya Jumuiya.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baada ya uchaguzi wa Kenya hawakuweza kuwachagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki mpaka sasa; je, Bunge hilo litaendelea bila Wabunge wa Afrika Mashariki kutoka Kenya au litasimama mpaka ufumbuji wa matatizo ya Kenya yapatikane?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa uchaguzi mkuu uliomalizika hivi karibuni nchini Kenya ulihusu uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Kenya. Lakini uchaguzi wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaowakilisha Kenya tayari walikwishapatikana ingawa yalitokea matatizo, ilikuwepo kesi, kesi hiyo ilikamilika na baadaye taratibu zilifuatwa. Wabunge wakapatikana wanaowakilisha Kenya na Bunge la Jumuiya ya Afrika la Awamu ya pili, tayari limeanza kazi na linaendelea kufanya kazi zake na Wabunge wa Kenya wanaowakilisha Kenya wanashiriki vikao hivyo kama kawaida.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kiswahili sasa hivi kimekuwa ni lugha rasmi hata katika Umoja wa Afrika kama tulivyojionea juzi wakati Mheshimiwa Rais mpendwa alipokuwa akihutubia Umoja wa Afrika; je, kwa nini Tanzania sasa ising'ang'anie kuwa Kiswahili siyo kitumike tu katika Afrika Mashariki lakini kiwe katika Katiba ya Afrika Mashariki na lugha nyingine hizo ndogo ndogo ziwemo lakini Kiswahili kiwe ni lugha rasmi? Ahsante.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikubaliane naye juu ya umuhimu wa Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni kweli kwamba Tanzania tunao wajibu wa kuhimiza kwamba Kiswahili kiingizwe katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ndiyo lugha rasmi. Niseme tu kwa hivi sasa Kiswahili kama ambavyo amesema Mheshimiwa Naibu Waziri ni vizuri Kiswahili ni lugha inayotumika ya pili baada ya Kingereza.

Lakini kwa sababu jambo hili linahusu mabadiliko ya mikataba mimi napenda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwanza Tanzania huwa inashinikiza na inang'ang'ania tuseme umuhimu wa kubadili utaratibu wa sasa wa kuzungumza Kingereza ili tuweze kuweka Kiswahili kama ndiyo lugha rasmi.

Kwa sababu utaratibu huu unahitaji uende kwa mujibu wa Katiba napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba ujumbe wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki utafikisha pendekezo la kuhakikisha kwamba mkataba wetu unahuishwa kama ambavyo maeneo mengine yanahuishwa pamoja na hili ili tuingize Kiswahili kama lugha rasmi na tuwashawishi wenzetu waweze kutumia Kiswahili kama lugha rasmi. (*Makofi*)

Na. 97

### **Daraja la Mto Simiyu**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa Elinino mwaka 1997, Daraja la Mto Simiyu Wilayani Magu lilichukuliwa na maji na kusababisha vifo vya watu na wanawake kupata shida wakati wa kujifungua; na kwa kuwa daraja hili ni muhimu sana kwa kuwa limeunganisha barabara ya Magu, Kijiji cha Misungwi, Lumeji hadi Kabila; na kwa kuwa daraja hilo limetengenezwa kwa mbao na sasa zote zimeoza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kulitengeneza daraja hilo kabla mvua za masika hazijaanza kunyesha?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Sukuma katika mto Simiyu lililopo kwenye barabara ya Magu – Kabila lenye urefu wa mita 80 ni daraja la chuma linalohamishika (*Bailey Bridge*) ambapo sehemu ya kutembelea magari imejengwa kwa mbao. Kwa kawaida mbao hizi hurudishiwa angalau mara moja au zaidi kwa mwaka kutegemea na uchakavu wa mabo hizo.

Wizara yangu kupitia wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Mwanza, imekuwa ikilifanyia matengenezo daraja hili kwa kubadilisha mbao kila mwaka kama ifuatavyo:-

Mwaka 2004/2005 jumla ya shilingi milioni 34.1 zilitumika, mwaka 2005/2006 jumla ya shilingi milioni 35.0 zilitumika, na mwaka 2006/2007 jumla ya shilingi milioni 30.0 zilitumika. Katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 jumla ya shilingi milioni 22.23 zimetumika kubadilisha mbao katika daraja hili na kuliwezesha kuwa linapitika bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu kupitia wakala wa barabara Mkoa wa Mwanza, itaendelea kulifanyia matengenezo na ukaguzi wa mara kwa mara daraja hili. Aidha, pamoja na matengenezo yanayofanyika mara kwa mara, Serikali tayari inafanya usanifu wa daraja katika mto Simiyu kwa lengo la kulijenga liwe la kudumu pindi fedha zikapopatikana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, fedha zimekuwa zikitengwa, nikijumlisha tu tangu 2004 mpaka 2005 jumla mpaka walivyosema kwenye mwaka 2007/2008 napata milioni 121 ambazo ni fedha nyingi sana za Watanzania na matengenezo ninavyozungumza hapa hayafanyiki kulingana na fedha hizi zilizotengwa na bado misumari ipo juu juu katika daraja hilo:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa akihakikishe fedha hizi zilitengwa milioni 121 zimetengenezwa kutokana na matengenezo hayo?

(b) Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielewe usanifu huu utamalizika lini ili watu wa maeneo ya makabila hayo, daraja hili la kudumu litatengenezwa lini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama alivyosema fedha zimekuwa zikipatikana kidogo kidogo na ndiyo tatizo kubwa kwamba kwa sababu zinatengwa milioni 30 huwezi ukajenga daraja kwenye mto mkubwa au daraja kubwa kama la Simiyu. Kwa hiyo, tumekuwa tukikarabati kila mwaka na tunajua kwamba milioni 30 ukitoa ndiyo kwa ajili ya mbao na mambo mengine ya mwaka huo. Zingekuwa zinapatikana kwa pamoja tungeweza tukafanya kazi kubwa. Lakini kuhusu kwamba labda fedha hizo hazitumiki vizuri ni jambo ambalo tutalifuatilia tuone kama zinatumika vipi. Kwa mfano, shilingi milioni 22 ambazo zimetumika juzi nina hakika kwamba zitakuwa zimetumika vizuri ama sivyo tutafuatilia. (*Makofi*)

Lakini kuhusu usanifu nimesema tunafanya usanifu ili baadaye kama fedha zitapatikana tuweze kujenga daraja. Kwa hiyo, usanifu ule kwa kweli ni maandalizi ya kwamba tuje tujenge daraja la kudumu fedha zitakapatikana. Kwa hiyo, itategemea kabisa upatikanaji wa fedha.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Matatizo yanayowapa wananchi wa wilaya ya Magu yanafanana kabisa na ya Wilaya ya Nanyumbu Kata ya Nakacho, Kijiji cha Mpombe ambako kuna Mto Lukwamba na kwamba Serikali mwaka jana iliahidi kujenga daraja Mto Lukwamba, lakini mpaka sasa hivi hakuna chochote kinachofanyika.

Je, Serikali itatimiza lini ahadi yake hii ya kujenga daraja mto Lukwamba?  
(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – MHE. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ya kujenga daraja la mto Lukwamba liko pale pale na taratibu zinaendelea tutaendelea kufuatilia ili tuone lini hasa kazi hii inaweza kuanza lakini ahadi ya Serikali ni ya uhakika.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, inakatisha tamaa tunapopata majibu kwamba mara fedha zitakapopatikana, mara hasa tunapozungumzia tatizo la mwanamke kujifungua. Hivi wanawake kama watakata tamaa kujifungua katika hali ya usalama je, *population* ya Tanzania kutoka milioni 34 haitawawia vigumu?  
(*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Nadhani swali la awali linahusu daraja kwa hiyo, nadhani umma wote wa Tanzania umesikia. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 98

### **Mkoa wa Dar es Salaam Kufaidika na Rasimali ya Bandari**

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam kiutawala una Wilaya tatu na Halmashauri zake tatu yaani Wilaya ya Temeke, Kinondoni na Ilala; na kwa kuwa rasilimali kubwa ya mkoa huu ni bahari; kwa hiyo, Wilaya zote tatu zinatakiwa kupata mchango wa mapato yatokanayo na rasilimali za Bandari kama vile Mamlaka ya Bandari Tanzania na vitengo vyake muhimu kama vile *TSCAN* na kadhalika kama ilivyo kwa mikoa yenye madini inavyofaidika na madini hayo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuziwezesha Halmashauri za Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam kwa maliasili hiyo kwa kupatiwa mgawo wa fedha kutokana na matumizi ya rasilimali?

(b) Kama hilo haliwezekani, je, Serikali itaeleza sababu za kutowezekana huko?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-



Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahmna Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali inaona umuhimu wa kuziwezesha Halmashauri za Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kuzipatia mgawo wa fedha kutokana na matumizi ya rasilimali hiyo. Hivyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, kwamba Manispaa zote tatu za Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Serikali Kuu zinapata mapato mbalimbali yatokanayo na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Baadhi ya mapato hayo ni kama vile: *City Service Levy* na *Property Tax* zinazolipwa kwa manispaa zote tatu. Baadhi ya mapato yanayotolewa kwa Serikali Kuu kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA) ni kama vile *Corporate Tax*, *Value Added Tax (VAT)*, *PAYE TAX*, *Skills & Development Levy (SDL)*, *Land Rent* na *Dividend*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, takwimu za kipindi cha miaka minne iliyopita yaani mwaka 2003/2004 mpaka Machi, 2007 zinaonyesha kwamba mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imetoa mchango wa zaidi ya *T.shs.* 90.075 bilioni ambapo Serikali Kuu ilipata zaidi ya *T.Shs.* 89.175 bilioni. Manispaa ya Temeke imepata *T.Shs.* 836,539,000 , Kinondoni *T.Shs.* 35,544,000 na Ilala *T.Shs.* 27,572,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka pia imekuwa ikitoa misaada mbalimbali ya huduma za kijamii kwa Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam. Baadhi ya huduma hizo ni ujenzi wa kituo cha feri, mchango wa mbio za mwenge, ujenzi wa visima vya maji na kuweka *culverts* maeneo ya Tabata.

Hivyo hakuna sababu za kutoziwezesha Halmashauri za Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam, kwa maliasili hiyo kwa kupatiwa mgawo wa fedha kutokana na matumizi ya rasimali hizo.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Lakini kutokana na maelezo yake kwamba faida wanayopata Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam baada ya kumsikiliza vizuri ni kutokana na kodi za kawaida na maombi madogo madogo ya kawaida:-

Kama wenzetu wa *National Parks*, wenzetu wa madini wanavyopata mrabaha inakuwa wazi kwenye mikataba yao; haoni wakati umefika sasa Dar es Salaam kuwekewa taratibu kama hizi kwa asilimia fulani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kama atakubaliana nami kwamba mapato mengi yanayotokana na bandari yanasaidia kuendesha Serikali na ndiyo maana tunaweza kufanya masuala ya shule na hospitali. Tukianza kusema tunafanya mrabaha itakuwa vigumu sana. Lakini tushukuru kwamba tunapata nafasi ya kuwasaidia wenzetu wa Ilala na Kinondoni na Temeke kwa kila ambacho wanakitolea jasho. Ahsante. (*Makofi*)

## Huduma ya Simu – Selous-Rufiji

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA (K.n.y. MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa wapo wananchi, wafanyabiashara na watalii wengi kwenye maeneo ya Hifadhi ya *Selous – Rufiji* ambao wanahitaji mawasiliano ya simu za mkononi kama vile vijiji vya Ngarambe, Kingupira Kilimani, Ngorongoro na Nyaminywili, Mtanza, Mloka na Mbwara:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kwa kutumia Sheria ya *Universal Communications Services Act* kuziwezesha Kampuni kama *Celtel, TTCL, Mobitel au Tigo, Vodacom* zijenge minara katika vijiji hivyo?

(b) Je, sheria hiyo mpaka sasa imeziwezesha Kampuni ngapi na vijiji vingapi vimekwishapata huduma hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya *Universal Communications Services Act* ilipotungwa na kupitishwa na Bunge ililenga kuwawezesha wananchi waishio maeneo ya vijijini kupata huduma za mawasiliano. Utaratibu mzima wa kufaidika na sheria hiyo ni kuanzisha mfuko wa *Universal Communications Access Fund* kwa ajili ya kuhudumia.

Mfuko huu utakapokuwa umeanzishwa, yamkini vijiji vyote nchini vikiwemo vile vilivyopo Wilayani Rufiji vitafaidika na mfuko huo na vitapata huduma ya mawasiliano kwa utaratibu utakaokuwa umekubaliwa baada ya mfuko huo kuanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa *Universal Communication Access Fund* utatoa ruzuku kwa makampuni ya mawasiliano yatakayokuwa yameshinda zabuni ili yaweze kufikisha huduma vijijini na maeneo yaliyo na shida ya mawasiliano mijini. Aidha, mfuko huo utachangiwa na watoa huduma za mawasiliano nchini yakiwemo makampuni ya simu aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, wahisani na taasisi nyingine zinazotoa huduma za mawasiliano nchi ili kutimiza lengo la kufikisha huduma za mawasiliano hadi vijijini. Mchakato wa kuanzishwa mfuko huo umekwishaanza na unatarajiwa kukamilika mwaka huu. Pamoja na mchakato huo, Serikali itaendelea na utaratibu wa kumpata mshauri mwelekezi (*consultant*) ambaye atakapopatikana atashirikiana na Wizara katika utekelezaji wake.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi muulizaji alitaka kujua vijiji ambavyo amevitaja, vitapata lini huduma hiyo ya simu na ameviorodhesha vijiji vingi tu. Je, mpaka sasa katika vijiji vile vilivyotajwa kuna

kampuni yoyote iliyokwenda kutoa huduma katika vijiji hivyo ili viweze kuhudumiwa kuweza kupata huduma hizo za simu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba mfuko huu utakapoanzisha makampuni ya simu ndiyo yatakayohusika na kutakuwa na *biding process* na hivi sasa wamesha-*bid* watu mbalimbali wenye makampuni ya simu. Vijiji alivyovitaja kwa kupitia mfuko huu, kwa sababu haujaanzishwa, havijafaidika na huduma hizi. Lakini nilimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashirikiana naye katika kufanikisha wapate mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Rufiji.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa ruhusa yako naomba niishukuru Serikali hususan Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr. Maua Daftari kwa ushirikiano mzuri walionipa na makampuni ya simu na sehemu kubwa ya Namtumbo *tunalonga* na simu za viganjani. Kwa kuwa bado bado kuna kata za Mkongo na Mabengo na Kitanda mawasiliano yanachenga; je, Serikali inaweza kutumia busara yake ile ile kuyaomba makampuni ya simu kutupatia huduma ya simu katika kata hizo zenye wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na biashara? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi namshukuru Mheshimiwa Kawawa kwa kufuatilia kwa karibu masuala yanayogusa wapiga kura wake. Kama nilivyomwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuwasiliana na makampuni kuona uwezekano wa kupeleka mawasiliano katika maeneo ambayo yamebakia, na kama nilivyomwahidi Mheshimiwa Mbunge wa Rufiji, masuala hayo nitayatekeleza. (*Makofi*)

Na. 100

### **Benki ya CRDB kufungua Tawi Zanzibar**

**MHE. AME PANDU AME** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imefungua milango ya uwekezaji ndani ya nchi yetu; na kwa kuwa Benki ya CRDB ina wateja Tanzania nzima:-

- (a) Je, ni sababu gani zinazopelekea benki hiyo isiwe na tawi Zanzibar?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua tawi la benki ya CRDB katika Visiwa vya Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki ya *CRDB* ilikwishajiwekea lengo la kufungua biashara zake Zanzibar. Hivyo imeanza kwa kuweka *POS* (kifaa cha malipo kwa *Tembo Card*), baadaye itaweka *ATM*. Hivi sasa upembuzi yakinifu wa kufungua tawi Zanzibar umekamilika. Hivyo *CRDB* imeamua itafungua Tawi lake mjini Zanzibar mwaka 2008. Tayari wataalamu wake wamekwishapendekeza sehemu kadhaa zinazofaa kuweka Tawi. Mazungumzo na wamiliki wa majengo husika yamekwishaanza na mara ikikamilika tawi litaanzishwa.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza:-

Kwa kuwa Zanzibar ina miji midogo na miji hiyo kwa hivi sasa inakua kwa kasi kubwa sana, pamoja na hilo pia uchumi wa Zanzibar unakua kwa kiasi fulani; je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba watupelekee wataalamu wa benki kwenye mji wa Nungwi na wakiona inafaa kujengwa benki basi watujengee japo tawi dogo kwenye mji wa Nungwi ili wananchi wake pamoja na wawekezaji wa kitalii wapungukiwe na usumbufu wa kufuata huduma hizo za benki kule mjini? (*Makofi*)

**MHE. AME PANDU AME:** Swali la pili, Mheshimiwa Spika,

**SPIKA:** Alaah, mawili kumbe.

**MHE. AME PANDU AME:** Ee! (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ulitulia kidogo.

**MHE. AME PANDU AME:** Ee ndiyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina azma ya kuwapunguzia umaskini wananchi wake, je, kwa nini haipeleki huduma hizi za kibenki mpaka kule vijijini badala yake inarundika huduma hizi kwenye miji mikuu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kuweka Tawi Nungwi, nafikiri kwa sababu *CRDB* wameshakamilisha upembuzi yakinifu, wameshapata mahali pa kuweka Tawi pale Mjini Zanzibar, tungoje kwanza hilo Tawi moja lifunguliwe baada ya hapo ndipo sasa *CRDB* inaweza ikaamua kufungua matawi mengine katika miji mingine. (*Makofi*)

Swali la pili, biashara ya kibenki kwa sasa hivi ni biashara ambayo anayewekeza anataka faida na ndiyo maana hata kufungua tawi pale Mjini Zanzibar ilibidi wafanye upembuzi yakinifu. Sasa kama kitapatikana vijiji kule Nungwi ambacho kinafaa kuweka tawi na benki ikajiridhisha kwamba kwa kuweka tawi kule watapata faida, tutaishawishi *CRDB* baada ya kufungua tawi Zanzibar waende Nungwi, waende na mahali pengine wakafungue matawi. (*Makofi*)

**Matawi ya NMB katika Mikoa**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2006, Benki ya *NMB Limited*, imeongeza matawi sita (6), katika miji mikuu ya Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Kilimanjaro na Tanga:-

Je, ni sababu zipi zilizokwamisha kufungua tawi la *NMB Limited* Unguja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli *NMB* haina tawi Unguja na kwamba huduma za kibenki zinahitajika katika maeneo mengi hapa nchini. Ufunguaji wa matawi ya benki unahitaji tathmini ya kina ili kuona kama vigezo muhimu vinavyokidhi matarajio ya biashara ya kibenki vinatimizwa. Hivyo, *NMB* itafanya tathmini ya kufungua tawi Unguja kulingana na vigezo hivyo ili kuona uwezekano wa kufungua tawi la Benki hiyo hapo. *NMB* pia imenuia kupanua mtandao wake kwa kufungua matawi sehemu ambazo huduma za kibenki hazijafika kwa lengo la kuwafikia wananchi zaidi. Aidha, matokeo ya tathmini ndiyo yatayozingatiwa katika kutoa kipaumbele cha ufunguaji wa matawi mapya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha mazingira muafaka kwa mabanki kufanya shughuli zao kwa ufanisi pamoja na kuishawishi *NMB* kuipa Unguja kipaumbele katika kuamua maeneo ya kufungua matawi mapya.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa vigezo vya mabanki vinalingana nchi nzima na *CRDB* wameshafanya tathmini, je, vigezo hivyo hivyo haiwezekani vikatumika kwa *NMB*?

(b) Mheshimiwa Waziri amesema kuwa Serikali itaweka mazingira mazuri, hivi sasa Zanzibar mazingira yake ni mazuri tu haihitaji kufanya mazingira mengine yawe mazuri ni kuipeleka tu hii benki, tatizo liko wapi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, mabanki yanafanya kazi zake kwa ushindani. Kwa hivyo, vigezo ambavyo *CRDB* wametumia kufungua Tawi Zanzibar haviwezi vikawa *a hundred percent* hivyo hivyo kwa *NMB*. Nilichosema ni kwamba tumeshawishi mabanki yote kwenda Zanzibar na tumeandaa mazingira mazuri kwa nchi nzima. Kwa hiyo,

tutaishawishi *NMB* ifanye haraka kufungua tawi lake pale na si lazima wafungue tawi pale pale ambapo *CRDB* wamefungua. Inawezekana wakaamua kufungua tawi mahali pengine kufuatana na vigezo ambavyo wao watakuwa wameridhika navyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa maswali umepita, mtakumbuka pale mwanzoni nilitumia takribani dakika 10 kutoa maelezo yangu, kwa hiyo, nikatumia muda wa maswali. Kwa hiyo, tutaweza kupata labda swali moja la nyongeza, baada ya hapo tutakwenda swali la mwisho. Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o swali la nyongeza!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa *NMB* imedhamiria kuwa benki ambayo inahudumia vijijini na kwa kuwa *NMB* ina tawi moja tu katika Wilaya ya Makete na kwa kuzingatia jiografia ya Wilaya ya Makete kwamba ni ngumu na kwa vile kuna Tarafa ya Matamba ambayo ni ngumu ukitaka kuja Makete mpaka uzunguke Wilaya ya Njombe ili uweze kufika Makete na watumishi wengi inabidi wafuate mishahara yao Makete, je, *NMB* ina mpango gani wa kuweka tawi katika Tarafa ya Matamba ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma za kibenki? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwa vile tuna tawi tayari pale Makete, Makao Makuu ya Wilaya, sisi tutajitahidi kama Wizara kuishawishi *NMB* lakini ningemshauri Mheshimiwa Mbunge akazungumze na Meneja wa Tawi la *NMB* pale Makete ili aweze kwenda kwenye sehemu ambayo ungependa awekwe tawi lingine na kama wataona inafaa, nina hakika watafungua tawi la pili Wilayani Makete.

**SPIKA:** Swali fupi kabisa la nyongeza, Mheshimiwa Devota Likokola.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma walishaiomba *NMB* wafungue Tawi katika Wilaya ya Namtumbo na walishafanya utafiti na wakakubali kufungua tawi katika Wilaya ya Namtumbo, ni nini kinasababisha kuchelewa kufungua tawi hilo la *NMB* katika Wilaya ya Namtumbo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwamba biashara ya benki ni biashara ambapo anayefungua benki anataka faida. Kwa bahati nzuri, *NMB* imeshafanya utafiti sasa kinachongojewa ni utafiti huo umeleta nini. Tutazungumza na *NMB* kuona kama utafiti wao umeona kama panafaa kufungua benki, tutawashawishi wafungue benki. Lakini pia ninapenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba benki nyingi sasa zimeanza kufungua matawi katika Wilaya. Kwa hiyo, namshauri ajaribu kuongea na watu wa *NMB*, na *CRDB* ambao pia wamejikita katika kufungua matawi kwenye Wilaya. Kama *NMB* itachelewa pengine hizi benki nyingine zinaweza kufungua mapema.

## **Bima za Maisha kwa Walimu – Songwe**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu miaka minne iliyopita Bima za Maisha za Walimu wa Shule za Msingi, Jimbo la Songwe zilikwishaiva na kwa kuwa tangu bima hizo ziive hadi sasa Walimu hao hawajalipwa haki zao kama mkataba wa bima unavyoelekeza:-

Je, ni lini Serikali itashughulikia kero za madai hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sigonda, Mbunge wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Shirika la Bima la Taifa lina madai ya bima zilizoiva katika Wilaya ya Chunya ambayo ni pamoja na Jimbo la Songwe yapatayo 284 na yenye thamani ya Shs.65,161,880.00. Kati ya madai hayo, madai 26 yenye thamani Shs. 8,360,257.00 ni ya vifo na madai 258 yenye thamani ya Sh.56,801,623.00 ni ya bima zilizoiva.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa, linatambua madai hayo na mengine kwa ujumla wake. Shirika linaendelea kulipa madai hayo na mengine yanayoendelea kuiva pale fedha zinapopatikana. Kwa mfano, katika mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2007, Shirika lilipa madai ya Bima za Maisha zenye thamani ya shilingi bilioni 2.27 kwa nchi nzima kati ya madai ya Shs. 6,273,531,797.20 yaliyokuwa yameiva.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Shirika za kulipa madai hayo, Shirika linakabiliwa na matatizo makubwa ya ukwasi unaopunguza uwezo wake wa kulipa madai yote ya bima kwa wakati mmoja. Hata hivyo, Shirika limejiwekea mikakati ya kupata fedha za kulipa madai hayo kwa awamu kutegemea na umri wa madai yenyewe (*FIFO*) kadri yanavyoiva. Mikakati hiyo, ni pamoja na ifuatavyo:-

- (a) Kuuza mali za Shirika hilo ambazo hazina uhusiano wa moja kwa moja na biashara ya bima (*non core assets*);
- (b) Kuuza asilimia 30 ya hisa za Shirika hilo katika mradi wake wa Ubungo Plaza;
- (c) Kutumia gawio linalotokana na hisa zilizowekezwa na Shirika hilo kwa niaba ya Serikali katika makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zilizotajwa za kulipa madai ya bima, Serikali imeandaa mapendekezo ya kulirekebisha Shirika hilo ili liweze kujiendesha kibiashara kabla ya kulibinafsisha kwa kuuza hisa kwa wananchi. Mapendekezo haya yalijadiliwa

na Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako Tukufu na Serikali inatazamia wakati wowote kuyapeleka mapendekezo haya Serikalini ili yaweze kufanyiwa maamuzi.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, nadhani itabidi nimruhusu muulizaji kwa sababu ana haki ya maswali mawili, muda umepita kabisa.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba ni kweli Walimu hao wamekuwa wakidai madai yao kwa kipindi cha miaka minne na kwa kuwa fedha ambazo walikuwa wameshalipa zilikuwa zinaendelea kuendesha hilo Shirika na kwa kuwa mkataba unasema kwamba endapo bima itaiva basi muhusika atalipwa fedha zake, je, Serikali itakuwa tayari kuwapa fidia ile ya ziada ya yale malipo ya kawaida Walimu hao ambao kwa muda wa miaka minne wamekuwa wakidai fidai? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa tayari mipango ipo, Serikali inafanya jitihada gani za kulipa madai yale? Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwapa matumaini wananchi wa Jimbo la Songwe kwamba mwaka huu watalipwa madai hayo? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu fidia. Kwanza kabisa, bima ni mkataba kati ya yule anayedhaminiwa na anayetoa bima. Tumekiri kwamba ni kweli Walimu 284 wana bima zao ambazo zimeiva lakini pia nimesema kwamba Shirika hili liko katika hali mbaya, inabidi tuliruhusu Shirika liuze hata baadhi ya mali zake ili liweze kukidhi mahitaji ya madeni wanayodaiwa. Nimeshasema kwamba mapendekezo yote yalishapelekwa mpaka hata kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wanajua kwa kina kabisa matatizo ya Shirika hili. Kama nilivyosema, ikiwa mapendekezo yote ambayo Wizara itapeleka Serikalini na yakapitishwa, naweza kukuhakikishia kwamba kwa sehemu kubwa madai ya wananchi hawa yatalipwa. Lakini ningependa wananchi wako wa Songwe wajue kwamba hakuna ambaye atakosa kulipwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Matangazo, wageni wetu Bungeni leo ni wageni wa Mheshimiwa Yunus Haji ambao ni Khadija Haji, Salama Yunus na Nassor Haji. Ningependa wageni hao wasimame ili Waheshimiwa Wabunge wawatambue. Wale pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wanachuo sita kutoka Chuo cha Biashara Dodoma, CBE Dodoma, wale pale, karibuni sana vijana. (*Makofi*)

Kuna wanafunzi 7 kutoka Shule ya Sekondari ya Kiwanja cha Ndege, Dodoma. Wamekuja kujaribu kujifunza mambo ya Bunge, wale pale. Karibuni sana katika Bunge letu. Ahsante sana. (*Makofi*)



Taarifa ya vikao. Mheshimiwa Hassan Khatib, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Maliasili na Mazingira, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, kutakuwa na kikao leo saa 7 mchana, Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu, kutakuwa na kikao muhimu sana leo saa 5 asubuhi katika Ukumbi Namba 428 asubuhi hii. Kwa hiyo, saa 5 asubuhi, Ukumbi Namba 428 Kamati ya Miundombinu.

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Halima Kimbau, anaumwa. Amelazwa jana usiku pale *Dodoma Regional Hospital*. Asubuhi leo nilikwenda kumwona, nikaona amepata nafuu kidogo, ana tatizo la kupumua. Lakini nimepata barua sasa hivi kutoka kwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, ambaye ametoka huko baada ya mimi kuondoka kwamba hali tena imegeuka. Kwa hiyo basi, tumkumbuke mwenzetu lakini ni vizuri tukipata nafasi twende kumtembelea. Namshukuru Mheshimiwa Shah, Mbunge wa Mafia, yupo pale wakati wote. Namshukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

## **HOZA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyochunguza  
Mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura  
Uliopa Ushindi *Richmond Development Company LLC ya Houston, Texas* –  
Marekani Mwaka 2006**

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kuomba mwongozo wako. Tarehe 28 mwezi uliopita, siku ya Jumatatu katika Kikao cha *briefing* kwa Wabunge wote, tulielezwa shughuli ambazo Bunge lako hili kwa Mkutano huu itazishughulikia. Miongoni mwa shughuli za Bunge hili, ni Miswada mbalimbali na Maazimio ambayo Serikali ilikuwa iwasilishe.

Naomba mwongozo wako kupitia Kanuni ya 30(4) ya Kanuni za Bunge kuhusiana na utaratibu huu. Kwa uwelewa wangu mdogo, ni kwamba shughuli za Serikali ndiyo zinapewa kipaumbele isipokuwa kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa kushauriana na Spika watakubaliana vinginevyo. Sina Taarifa kwamba Miswada yote ambayo Serikali ilikuwa inakusudia kuwasilisha katika Mkutano huu kama imekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona tupate mwongozo wako katika hatua hii muhimu ili tuweze kujua ni nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kwa utaratibu, Bunge linaongozwa kwa kuzingatia maamuzi ya Kamati ya Uongozi. (*Makofi*)

Kanuni ya 34, imepanga mtiririko huo ambao unauweleza lakini Kamati ya Uongozi ambayo inajumuisha Wawakilishi pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge ambaye ameshiriki kikamilifu, imeamua hivi ilivyoamua na mimi kama Spika nimeona ni busara. Kwa sababu baada ya tukio la Jumapili kwenye Semina, hisia za Wabunge zinanielekeza kwamba uamuzi huu ni sahihi. Kwa hiyo, kama tulivyofanya siku za nyuma pale inapoonekana ni muhimu kupanga mpangilio upya basi tunafanya hivyo na hilo ndilo lililofanyika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati Teule, ninaomba kueleza kwamba Kamati hiyo hiyo ya Uongozi imependekeza na ndiyo uamuzi kwamba Mwenyekiti akishawasilisha Taarifa yake basi tuahirishe Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii ni ndefu sana kama mnavyoiona lakini hii ni theluthi moja tu ya kazi vielelezo ni mara tatu ya hivi.

**WABUNGE FULANI:** Vimekwishatolewa.

**SPIKA:** Alaah, vimekwishatolewa. Hivi ndivyo vielelezo. Nawaonyesheni ili kila mtu apate vitu kamili. Hii ndiyo taarifa na hivi ndivyo vielelezo na kuna *Hansard* tatu. Kwa hiyo, Kamati ya Uongozi, iliyokutana jana, iliona ni vema basi baada ya Mwenyekiti kuwasilisha Taarifa tuweze kuahirisha Bunge ili mjadala uweze kuanza kesho. (*Makofi*)

Kwa maelezo hayo, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati Teule iliyochunguza *Richmond Development Company*. (*Makofi*)

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE (MWENYEKITI WA KAMATI TEULE YA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa tarehe 13 Novemba, 2007 na Bunge hili Tukufu kuchunguza mchakato wa zabuni ya uzalishaji umeme wa dharura uliofanyika mapema mwaka 2006 na kuipa ushindi *Richmond Development Company, LLC*, ya Houston, Texas, Marekani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa Kamati Teule, kukupongeza wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa uamuzi wa kuunda Kamati hii maalum kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kikatiba ya Bunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule kuwasilishwa na kuafikiwa na Bunge, uliwateua Wabunge watano wafuatao kuunda Kamati Teule kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Wa kwanza Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mbunge, wa pili Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge, wa tatu Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge, wa nne Mheshimiwa Lucas Lumambo Seleli, Mbunge na wa tano Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Novemba, 2007, uliipa Kamati Teule siku thelathini kukamilisha kazi yake na Hadidu za Rejea zifuatazo kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo ya uchunguzi:-

(1) Kubainisha *Richmond Development Company, LLC* ni kina nani na ni kampuni inayofanya shughuli zipi na hivyo kupima uwezo wake wa kupatiwa zabuni ya kuleta nchini na kujenga mtambo wa umeme wa gesi wa *megawatts* 100;

(2) Kutathmini mchakato mzima wa jinsi zabuni waliyoshinda *Richmond* ilivyoshughulikiwa kuanzia Kamati ya Zabuni hadi mwisho ili kujiridhisha kuwa Sheria, taratibu, miiko na maadili ya zabuni yanayotawala zabuni za aina hiyo vilifuatwa au vipi;

(3) Kutathmini mkataba baina ya *Richmond Development Company, LLC* na *TANESCO* ili kujiridhisha kuhusu uhalali wa masharti ya mkataba huo ukizingatia gharama na masharti mengine ukilinganisha na masharti yaliyomo katika mikataba ya aina hiyo iliyoafikiwa na *TANESCO* na Serikali;

(4) Kubainisha huduma na misaada mbalimbali waliyopewa *Richmond* kama vile kufunguliwa *Letter of Credit* na kupima uhalali wake;

(5) Kuziangalia na kuzitolea maoni taarifa za *TAKUKURU, PPRA* na taarifa zozote nyingine zilizoangalia utaratibu wa zabuni ya *Richmond*; na

(6) Kuangalia mambo mengine yoyote yenye uhusiano na mchakato mzima wa *Richmond* ili kutoa mapendekezo ya kuboresha taratibu za zabuni kwa siku zijazo, kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004, wajumbe walinichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati Teule. Aidha, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii ya awali, kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa imani kubwa waliyotunyeshwa mimi na Mheshimiwa *Engineer* Manyanya ya kutuchagua kwa kauli moja kuiongoza Kamati Teule ya Bunge (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilianza kazi yake mara moja kwa kukusanya na kuzisoma nyaraka mbalimbali za msingi kama vile mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company, LLC*, Sheria ya Ununuzi wa Umma (*Public Procurement Act*) ya Mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, Taarifa ya Uchunguzi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, *TAKUKURU*, wakati huo ikiitwa *TAKURU* na taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma, *Public Procurement Regulatory Authority - PPRA*, kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati Teule ilianza kuandaa hati (*summons*), kwa mujibu wa vifungu 13(1) na 14(1) na (2) vya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya Mwaka 1988 (Sura ya 296), za kuita mashahidi mbalimbali waliohusika kwa njia moja au nyingine katika mchakato wa zabuni hiyo ya uzalishaji wa umeme wa dharura.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Desemba, 2007, jumla ya mashahidi 46 walihojiwa na maswali 2061 kuulizwa. Pamoja na Kamati Teule kutumia vyombo vya habari kuwatia moyo watu wenye ushahidi kuhusu suala hili ili wajitokeze na kueleza Kamati Teule, hakuna shahidi hata mmoja aliyekuja kwa hiari yake mwenyewe bila kupelekewa hati ya kuitwa. Aidha, mashahidi wote waliotuletea maelezo kimaandishi kwa njia ya simu au barua, hawakuweka majina yao wala anuani zao, hivyo kuipa Kamati Teule wakati mgumu kufuatilia kauli zao.

Mheshimiwa Spika, matokeo haya, yanaonesha hali halisi iliyopo Tanzania, hali ya uoga na ya kutojiamini inayowakumba Watanzania walio wengi wanapotakiwa kuelezea kwa uwazi maneno yale yale wanayoyanong'ona pembeni kwa hamasa kubwa. Kwa mtindo huu, Taifa letu linaweza kuishia kuwa la walalamishi wasio na ujasiri wala dhamira ya dhati ya kukemea maovu pale inapobidi (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, mashahidi wengi walioitwa kwa hati hususan kutoka *TANESCO*, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Wizara ya Katiba na Sheria walionyesha hofu, mashaka na hali ya kutojiamini kwa kutoa majibu yaliyofanana ya kiitifakiitifaki na yaliyokosa mvuto na ushawishi wa kawaida mithili ya watu walioketishwa pamoja na kukaririshwa hoja za kujibu. Wataalam wa *TANESCO*, mathalani, waliikataa *Richmond Development Company, LLC*, mara tatu wakati wa kutathmini zabuni ya umeme wa dharura, kwa hoja za kitaalam kuwa haifai kwa vigezo vyote muhimu. Walipofika mbele ya Kamati Teule, wakawa wapambe nambari moja wa kampuni hiyo, wote wakiimba sifa za kulazimisha za kampuni hiyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nyaraka nyingi ambazo Kamati Teule ilizipata toka Serikalini na taasisi mbalimbali, zilikuwa nakala zilizokosa mtiririko wa kimasijala. Kamati Teule ilipodai nyaraka halisi kulinganisha na nakala ilizokuwa nazo, ilipewa majalada yaliyoonyesha dalili zote za kukarabatiwa (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, hali hii ilijitokeza zaidi kwa *TANESCO* na Wizara ya Nishati na Madini. Jalada halisi kutoka *TANESCO* lilichukua siku tatu kuifikia Ofisi Ndogo ya Bunge likiwa na nyaraka zenye namba zilizokosa mtiririko stahili. Wizara ya Nishati na

Madini ndiyo iliyotia fora kwa kumtuma Msaidizi wa Katibu Mkuu, Ndugu Julius Sarota tarehe 18 Desemba 2007 akiwa na maagizo ya kuwafungulia Wajumbe wa Kamati Teule kurasa maalum tu na si nyinginezo hivyo kuinyima Kamati Teule mtiririko halisi wa mawasiliano. Kamati Teule haikuridhishwa na utaratibu huo, hivyo ilimtaka Msaidizi huyo wa Katibu Mkuu aondoke na majalada yake na kumpelekea hati ya kuitwa Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi afike yeye mwenyewe na majalada hayo.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 19 Desemba 2007, Katibu Mkuu huyo kwa maneno mengi na ya kuzunguka, alithibitisha kuwa alichokifanya Msaidizi wake yalikuwa maelekezo ya Wizara. Kwa kuzingatia uhaba wa muda wa kukamilisha kazi ya Kamati Teule na kwamba suala hilo tayari lilikuwa limechukua siku tatu nzima za Kamati Teule, ugeni wa Katibu Mkuu huyo katika Wizara hiyo na katika masuala ya Bunge na uwezekano uliokuwepo kwa Kamati Teule kupata taarifa za ziada kupitia njia nyingine, Kamati Teule iliamua kusonga mbele na kumuacha Katibu Mkuu huyo na siri kubwa za Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na changamoto hizo, Kamati Teule ikaona kuwa ni vyema baadhi ya Wajumbe wake waende Houston, Texas, Marekani ili kupata taarifa za kina na za ziada kuhusu suala hilo.

Kamati Teule inamshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuzielewa changamoto zilizokuwa zinaikabili Kamati Teule na kuwawezesha Wajumbe watatu kwenda Washington DC kukutana na maafisa wa Ubalozi wetu, na vilevile Houston Texas kukutana na wamiliki wa *Richmond Development Company, LLC*.

Mheshimiwa Spika, wajumbe hao walioondoka Dar es Salaam kwenda Marekani tarehe 10 Desemba 2007, ni Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge, Mheshimiwa Lucas Lumambo Seleli, Mbunge, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge na Ndugu Anselm L. Mrema, Katibu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Desemba 2007, Kamati Teule ilikuandikia barua kukuomba uiongezee muda kwa sababu kuu mbili. Kwanza, wajumbe watatu kati ya watano na Katibu wa Kamati Teule walikuwa nchini Marekani kuanzia tarehe 10 Desemba 2007, kujiridhisha na taarifa mbalimbali ambazo Kamati Teule ilizipata kuhusu *Richmond Development Company, LLC*. Kwa kuwa wajumbe hao walikuwa wanategemea kurejea nchini tarehe 15 Desemba 2007, siku ambayo Kamati Teule ilitakiwa kuwasilisha taarifa yake na kwa kuwa taarifa ambazo wangepata Marekani zingetakiwa kuingizwa kwenye taarifa ya Kamati Teule na hata kubadilisha baadhi ya masuala katika taarifa hiyo, muda wa ziada ulihitajika.

Pili, baada ya uchambuzi wa kina wa ushahidi wa maandishi na wa mdomo uliotolewa mbele ya Kamati Teule chini ya kiapo, Kamati Teule iligundua kuwepo kwa mgongano wa ushahidi, hivyo kutia mashaka juu ya dhamira ya baadhi ya mashahidi. Kamati Teule iliona umuhimu wa kuwaita tena baadhi ya mashahidi kuthibitisha kauli

zao na hata kuwachukulia hatua za kisheria baadhi yao ambao wangeendelea kusema uongo chini ya kiapo ili kulinda heshima ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, uliuona umuhimu wa kuiongezea muda Kamati Teule, hivyo tarehe 13 Desemba 2007, ukaridhia ombi la Kamati Teule na kuweka tarehe 31 Desemba 2007, kuwa tarehe ya kuwasilisha taarifa ya uchunguzi. Tunakushukuru sana kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2007, siku Kamati ilipowasilisha taarifa yake kwako, Kamati Teule ilikuwa imewahoji jumla ya mashahidi 75 na kuuliza maswali 2717 na kuzipitia nyaraka na kumbukumbu 104. Mashahidi 4 kati ya hao walikuja kwa hiari yao bila kupelekewa hati za kuitwa. Mashahidi 7 waliitwa mara mbili. Mashahidi wawili, Ndugu Daniel Yona na Mheshimiwa Rostam Aziz, Mbunge, walipelekewa hati za kuitwa mbele ya Kamati Teule lakini hawakufika kwa maelezo kwamba walikuwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ndugu Daniel Yona alitakiwa na Kamati Teule atoe maelezo kuhusu msingi wa uamuzi wake wa kuipa *Richmond Development Company, LLC*, haki maalum ya kipekee, *exclusive right*, ya miezi 18 kuhusu mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza mwaka 2004 wakati huo akiwa Waziri wa Nishati na Madini. Maelezo ya ziada ya mradi huu nitayatoa baadaye kidogo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Rostam Aziz alitakiwa atoe maelezo kuhusu uhusiano wake na Kampuni za *Richmond Development Company, LLC* na *Dowans Holdings S.A* baada ya mashahidi kadhaa kudai kuwa ana uhusiano nazo.

Aidha, alitakiwa na Kamati Teule aeleze kwa nini anwani ya barua pepe ya kampuni yake ya *Caspian Construction Ltd* ilitumiwa na *Dowans*. Kamati Teule ilitaka vilevile kupata ufafanuzi kutoka kwake kuhusu baadhi ya wafanyakazi wa kampuni yake wanaosemekana kuwa ni watumishi vilevile wa *Dowans Holdings S.A*.

Mheshimiwa Spika, leo tunapowasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu, tunajisikia kuutua mzigo mzito sana ulioanza kutuelemea kutokana na kuzongwa kila kukicha na kila aina ya uzushi, uchochezi, uchonganishi na hata vitisho. Tumezushiwa kuhongwa magari ya kifahari na fedha taslimu; tumetuhumiwa kuendesha vita dhidi ya Waislamu na mara nyingine tuhuma hiyo ikageuka kuwa vita dhidi ya Wakristo ndani ya Serikali; tumesingiziwa kuibadilisha taarifa yetu mara mbili, baadhi wakisema kwa ushawishi wa fedha, wengine wakidai kwa shinikizo la Mheshimiwa Spika na wengine kwa shinikizo la Waziri Mkuu; tumeshuhudia pilikapilika za usiku na mchana za kujipanga na kuwashawishi baadhi ya Mawaziri na Wabunge kuikana taarifa hii na mapendekezo yake kiasi cha wengine wetu kujiuliza: kulikoni mtu asiye na hatia kuweweseka?

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa Kamati Teule, kukuhakikishia wewe binafsi na Bunge lako tukufu kuwa tumekamilisha kazi tuliyopewa kwa uaminifu na ujasiri mkubwa, dhamira safi, moyo wa uzalendo na kwa kumtanguliza mbele Mwenyezi Mungu katika kila tulilolifanya. Tulichukua kila tahadhari tusibanwe na

mgongano wowote wa kimaslahi kiasi kwamba mjumbe mwenzetu, Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*, mwajiriwa wa muda mrefu wa *TANESCO* ambaye alikuwa kwenye likizo isiyo na malipo, akaamua kukatisha ajira yake kwa kujiuzuru.

Aidha, tunakuhakikishia Mheshimiwa Spika kuwa hatukupokea senti tano ya mtu wala baiskeli yake. Mwenye ushahidi tofauti, basi alithibitishie Bunge hili Tukufu na mimi na wajumbe wenzangu wa Kamati Teule tuko tayari kuwajibika kisiasa.

Mheshimiwa Spika, ukame na tatizo la uzalishaji umeme nchini. Kwa takribani miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2002, nchi yetu ilikumbwa na tatizo la ukosefu wa mvua za kutosha. Athari za tatizo hilo hasa katika uzalishaji umeme, zilianza kuonekana mwaka 2004 na kufikia mwishoni mwa mwaka 2005 ikawa dhahiri kwamba nchi ilikuwa inaelekea kwenye janga kubwa la upungufu wa umeme. Mahitaji ya mitambo ya gesi ya kuzalishia umeme wa dharura yakajitokeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, mwezi Desemba 2005, *TANESCO* iliomba Serikali kufikiria na kuidhinisha mpango wa kukodisha mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura kwa kutumia gesi kutoka kwenye makampuni yanayofahamika kwa biashara hiyo chini ya mikataba ya kuuziana umeme kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili.

Mheshimiwa Spika, tarehe 28 Desemba 2005, Serikali ilikubali ombi hilo na kuiruhusu *TANESCO* kuwasiliana moja kwa moja na kampuni ya *SONGAS* iliyopo nchini kuhusu mahitaji hayo ya dharura. Bila kuchelewa, *TANESCO* wakawasiliana na *SONGAS* ambayo ikaanza mara moja kuandaa makisio ya mradi huo.

Tarehe 11 Januari 2006, *CDC Globeleq*, kampuni mama ya *SONGAS*, iliwasilisha *TANESCO* makisio ya kukodisha mitambo ya gesi ya kuzalisha umeme wa *Megawatts 74* ambayo ingefungwa Ubungo na kuanza kuzalisha umeme katikati ya mwezi Aprili 2006.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Januari 2006, Bodi ya Zabuni ya *TANESCO* ilianza kujadili zabuni hiyo ya *CDC Globeleq* na siku sita baadaye, yaani tarehe 19 Januari 2006, Bodi hiyo ikathibitisha mapendekezo ya zabuni hiyo na kuingia katika majadiliano na *CDC Globeleq*. Tarehe 30 Januari, 2006 Bodi ya Zabuni ya *TANESCO* iliyakubali mapendekezo ya Kamati ya Tathmini ya kuingia mkataba wa uzalishaji umeme kwa miaka mitano au mitatu kama ifuatavyo:-

Kwanza, miaka mitano kwa bei ya senti za Kimarekani  $3.2/kWh$ ; au pili miaka mitatu kwa bei ya senti za Kimarekani  $5.3/kWh$ . Chini ya mpango huo, mitambo hiyo ya kuzalisha umeme ingekuwa mali ya *TANESCO* baada ya kipindi cha kukodi kumalizika.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi pamoja na mapendekezo ya Wizara ya Nishati na Madini yaliwasilishwa na kujadiliwa katika Kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 10 Februari 2006, yaani siku nne baada ya kuanza mgao wa umeme kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara inayounganishwa na Gridi ya Taifa. Pamoja na mambo mengine, Baraza

la Mawaziri liliweka msimamo wa Serikali wazi kuwa *CDC Globeleq* ikubali kuiuzia Serikali mitambo yake au iikodishe Serikali kwa bei ambayo Serikali ingeridhika nayo na siyo kwa kipindi cha miaka mitano bali kipindi kile tu cha matatizo ya umeme kutokana na ukame.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri haukuwa makini. Kwani siku hiyo hiyo ya tarehe 10 Februari 2006, Wizara ya Nishati na Madini, badala ya kuwatumia ujumbe sahihi *CDC Globeleq* kuwa Serikali inataka wabadilisha masharti yao kama nilivyokwishaeleza, ikapeleka ujumbe tofauti kabisa kuwa Serikali inafuta mpango wa kukodisha mitambo kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumhoji aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini kipindi hicho Mheshimiwa, Dr. Ibrahim Msabaha, (Mb) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Arthur Mwakapugi kwa muda mrefu na katika siku nne tofauti, Kamati Teule ilishindwa kupata majibu ya uhakika kwa maswali yake manne, swali la kwanza:-

(i) Je, kulikuwa na kikao kingine cha Baraza la Mawaziri siku hiyo hiyo ya tarehe 10 Februari, 2006 kilichotengua maamuzi yake ya awali ya siku hiyo hiyo?

(ii) Ikiwa jibu ni hapana, kwa nini Wizara ilipeleka *CDC Globeleq* ujumbe tofauti na ule ulioagizwa na Baraza la Mawaziri?

(iii) Kwa nini Wizara isitume barua hiyo baada ya kushindwa kuwashawishi *CDC Globeleq* kubadilisha masharti yao?

(iv) Maamuzi kama hayo, siku nne ndani ya mgao wa umeme wa nchi nzima na katika kipindi ambacho Serikali haikuwa na mkakati mbadala uliokuwa umeiva kama wa *CDC Globeleq*, hayo kweli yalikuwa maamuzi makini ya kunufaisha Taifa?

Mheshimiwa Spika, kutokana na msimamo huo mpya wa Wizara, *TANESCO* ikaachana na mpango wa kukodisha mitambo na kuelekeza nguvu zake kwenye kununua mitambo mipya ya kuzalishia umeme. Hivyo, tarehe 20 Februari 2006, *TANESCO*, iliwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini mpango wa ununuzi wa moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji wa mitambo ya kuzalishia umeme wanaofahamika duniani chini ya utaratibu unaotambuliwa kama *international shopping* chini ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo ikafuatiwa na kikao cha Waziri wa Nishati na Madini na watendaji wa Wizara na *TANESCO* tarehe 21 Februari 2006 ambacho Waziri alikutumia kuisitiza kuwa mpango wa Serikali si kukodisha mitambo bali kununua na kuiagiza *TANESCO* kutangaza zabuni mara moja. Waziri alitaka tangazo la zabuni lichapishwe magazetini siku ya Alhamisi tarehe 23 Februari 2006 na kuwapa *TANESCO* masharti yafuatayo:-



Kwanza zabuni ifunguliwe baada ya siku 10, yaani tarehe 6 Machi 2006, pili tathmini ya zabuni ifanyike kwa siku mbili tarehe saba na nane Machi 2006.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya zabuni. Tarehe 22 Februari 2006, *TANESCO* iliomba idhini ya Mamlaka ya Udhubiti wa Ununuzi wa Umma, *PPRA*, kutangaza zabuni hiyo kwa muda wa siku 10 badala ya siku 45 zinazoainishwa katika Kanuni za Ununuzi. Tarehe hiyo hiyo ya 22 Februari 2006, *PPRA* ikaijibu *TANESCO* kwa kuitahadharisha kuwa utaratibu huo utakuwa kinyume cha taratibu na Kanuni za ununuzi. Muda wa siku 10 hautoshi kuitisha zabuni ya kimataifa na kuweza kupata wazabuni wenye sifa zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ikaishauri *TANESCO* kuwa badala ya kutumia njia ya kutangaza zabuni ya kimataifa, *international competitive tendering*, itumie njia mbadala ya ununuzi wa kimataifa, *international shopping*, ambapo makampuni mengi yanayotengeneza mitambo ya kuzalisha umeme yanaalikwa na “kuyashindanisha kwa kuyaomba yawasilishe zabuni zao badala ya kutangaza kwani utaratibu huo ungesaidia kuondoa makampuni ya kati yasiyohusika na uzalishaji umeme”.

Mheshimiwa Spika, tarehe hiyo hiyo 22 Februari, 2006, *TANESCO* ikaiarifu Wizara kuhusu ushauri wa *PPRA*. Wizara ikaukataa na kuiagiza *TANESCO* kutekeleza agizo la Wizara na Waziri bila kukosa kwa kuitangaza zabuni hiyo. Zabuni hiyo ikatangazwa kwa utaratibu wa ndani tarehe 23 Februari 2006. Hatua hiyo iliishitua *PPRA* ambayo iliandikia barua *TANESCO* kuelezea kushangazwa kwake na hatua ya shirika hilo kukaidi ushauri wa kitaalamu na wa kisheria. *PPRA* ikasisitiza kuwa, njia pekee kwa *TANESCO* kupata wazabuni wazuri na wenye sifa stahili katika kipindi kifupi ni kutumia utaratibu ilioupendekeza wa *international shopping*.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji umeme nchini iliendelea kuwa tete na kulazimu kikao cha Baraza la Mawaziri kufanyika tarehe 23 Februari 2006, na kuagiza utaratibu wa haraka, *fast track*, wa kukodi mitambo ya kuzalishia umeme wa dharura ufanyike. Katika kutekeleza maamuzi hayo, Baraza liliagiza kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 zizingatiwe. Pamoja na msisitizo huo wa Baraza la Mawaziri, Wizara ya Nishati na Madini ikaendelea kuishinikiza *TANESCO* kufuata maagizo ya Wizara na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* ikionyesha dhahiri kusukumwa tu na Wizara, ikaiandikia tena *PPRA* Jumapili tarehe 26 Februari 2006 kuelezea kuwa sasa imeagizwa na Serikali kuitangaza zabuni hiyo magazetini, hivyo Mamlaka hiyo ya Udhubiti wa Ununuzi wa Umma itoe idhini ya kutangaza zabuni ya kimataifa kwa siku chache kuliko zilizowekwa na Sheria. *TANESCO* huku ikijua kabisa kuwa *PPRA* isingeweza kuipata na kuijibu barua hiyo Jumapili, ikatangaza zabuni hiyo magazetini tarehe 27 Februari 2006 na kuwataka wazabuni wawasilishe zabuni zao tarehe 6 Machi 2006 yaani siku 10 baada ya kuchukua nyaraka za zabuni tarehe 24 Februari 2006.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Machi 2006, *PPRA* ikajibu *TANESCO* kuwa pamoja na kuendelea na zabuni hiyo, isingekuwa rahisi kwa Shirika hilo la umeme la Taifa kupata mzabuni anayefaa katika kipindi hicho kifupi cha siku 10. Hata hivyo, *PPRA* ikaitaka *TANESCO* kuufuatilia utaratibu mzima wa zabuni hiyo kwa karibu ili kuhakikisha kuwa taratibu zinafuatwa, ili kuepusha malamiko yasiyo ya msingi kutoka kwa wazabuni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza *PPRA* kwa kuonyesha subira ya hali ya juu, uwazi na ukweli wa kitaaluma, Kamati Teule ilishindwa kubaini moja kwa moja chanzo cha ujasiri wa kiburi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini kiasi cha kupindisha maamuzi ya Baraza la Mawaziri kama tulivyoona na kukaidi ushauri wa mamlaka iliyowekwa Kisheria. Aidha, Kamati Teule ilishangazwa na Ofisi ya Waziri Mkuu iliyokuwa ikifuatilia kwa karibu sana mchakato huo, kushindwa kukemea ukaidi huo wa Wizara ya Nishati na Madini (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, mchakato wa zabuni ndani ya *TANESCO*. Hadi muda wa zabuni ulipoongezwa, yaani tarehe 20 Machi 2006, jumla ya wazabuni ishirini na sita (26) walinunua nyaraka za zabuni zilizouzwa kwa fedha isiyorejesheka, *non refundable*, ya Dola za Kimarekani 100. Ni wazabuni wanane (8) tu ndio waliorudisha nyaraka za zabuni hiyo kama ifuatavyo; *M/S Aggreko International Projects Ltd* ya Uarabuni, *M/S Quantus* ya Ujerumani, *M/S APGUM Co. Ltd* ya Ujerumani, *M/S Globeleq Ltd* ya Kanada, *M/S Real Energy Projects* ya Uingereza, *M/S Renco SPA* ya Italia, *M/S Richmond Development Company LLC* ya Marekani na *M/S GAPCO(T) Ltd* ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, zabuni zikafunguliwa na wazabuni wote wanane waliorudisha nyaraka zao za zabuni waliwakilishwa kwenye ufunguzi. *TANESCO* ikaunda Kamati ya Kutathmini Zabuni iliyokuwa na wajumbe 12, kati yao wanane walitoka *TANESCO*, wawili kutoka kampuni ya ushauri ya *Lahmeyer International*, mmoja kutoka Wizara ya Fedha na mwingine Wizara ya Nishati na Madini. Kamati hiyo ilipewa wiki moja tu kumaliza kazi yake na kuiwasilisha taarifa ya tathmini kwenye Bodi ya Zabuni ya *TANESCO* tarehe 28 Machi, 2006.

Mheshimiwa Spika, Vigezo vya Tathmini, *Preliminary Evaluation*. Kamati ya Tathmini ikitumia vigezo mahsusi karibu ya 30 vya kupima uwezo wa mzabuni, ikathibitisha kuwa hakuna mzabuni hata mmoja kati ya wanane aliyetimiza au kukidhi vigezo vya zabuni vilivyowekwa. Kutokana na hali ya kutisha ya ukosefu wa umeme nchini, Kamati ya Tathmini ikalazimika kuondoa zaidi ya nusu ya vigezo na kubakiza tisa tu ilivyoviona muhimu sana kwa ngazi ile ya uchambuzi ili kumpata mshindi katika kundi hilo la wazabuni wanane.

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyobakizwa ni; muda wa kuleta mtambo na kuanza kazi, dhamana ya zabuni, *tender security*, uwepo wa mtambo tayari kuletwa Tanzania, uzoefu wa mzabuni kutekeleza miradi/ kuendesha mitambo ya aina hiyo, uzoefu na sifa za kitaaluma au za kiufundi za mzabuni, viambatisho vya idhini ya kisheria kuweza kufanya maamuzi ya mwisho, *Power of Attorney*, uwepo wa maelezo ya lazima ya

kiufundi, ujazaji fomu ya zabuni kikamilifu na mchanganuo wa bei au gharama ya umeme.

Mheshimiwa Spika, wazabuni wote wanane wakafanyiwa tathmini ya pili kwa kuzingatia vigezo hivyo tisa tu. Hata hivyo matokeo yakawa yale yale. Wazabuni wote wanane wakashindwa kukidhi vigezo hivyo vichache.

Mheshimiwa Spika, nyaraka tulizopata kutoka *TANESCO* zinaonyesha maeneo mbalimbali ya udhaifu miongoni mwa wazabuni hao kama ifuatavyo:-

*M/S Aggreko International Projects Ltd* ya Uarabuni ilikutwa na maeneo 7 yenye mapungufu, *M/S Renco SPA* ya Italia maeneo 9, *M/S APGUM Co. Ltd* ya Ujerumani maeneo 12, *M/S GAPCO(T) Ltd* ya Tanzania maeneo 13, *M/S Globeleq Ltd* ya Kanada maeneo 14, *M/S Real Energy Projects* ya Uingereza maeneo 15, *M/S Quantus* ya Ujerumani maeneo 16, na *M/S Richmond Development Company, LLC*, ya Marekani ilikutwa na maeneo 17 yenye mapungufu (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Tathmini haikuona busara kutangaza kuwa imeshindikana kabisa kumpata mshindi. Hivyo, ikapunguza vigezo zaidi na kubakiza vitano tu kama ifuatavyo:-

Muda ambao mtambo utanza kazi, uwepo wa mtambo tayari kuletwa Tanzania, uzoefu wa mzabuni kutekeleza miradi au kuendesha mitambo ya aina hiyo, uzoefu na sifa za kitaaluma au kiufundi za mzabuni na uwepo wa maelezo ya lazima ya kiufundi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii wazabuni wanne (4) wakashindwa kukidhi vigezo vichache vilivyobakizwa, hivyo kushindwa kufuzu kuingia hatua ya pili ya kufanyiwa tathmini ya kina, *detailed evaluation*. Wazabuni wengine wanne wakaonekana kuwa na afadhali kidogo na kuruhusiwa kuingia hatua ya pili ya kufanyiwa tathmini ya kina. Nao ni; *M/S Real Energy Projects* ya Uingereza, *M/S Renco SPA* ya Italia, *M/S GAPCO(T) Ltd* ya Tanzania, na *M/S Richmond Development Company, LLC*, ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya kina ya wazabuni hao wanne walioonekana afadhali kidogo, ilionyesha kuwa *Richmond Development Company LLC* ya Marekani bado ilikuwa na mapungufu mengi yaani 13 kupita wazabuni wengine watatu. *M/s Renco SPA* ya Italia ilifuatia kwa kuwa na mapungufu 10; *M/s GAPCO (T) Ltd* ya Tanzania mapungufu 9 na *M/s Real Energy Project* ya Uingereza mapungufu 8. Kamati ya Tathmini iliwasilisha matokeo ya tathmini kwa Bodi ya Zabuni ya *TANESCO* ikielezea kwamba hakuna mzabuni hata mmoja aliyetimiza masharti, hivyo wote walikosa sifa za kupata zabuni. Hivyo Kamati ikashauri zabuni itangazwe upya.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Zabuni ya *TANESCO* baada ya kuridhia mapendekezo hayo, iliyawasilisha kwenye Bodi ya Wakurugenzi wa *TANESCO* tarehe 30 Machi 2006. Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO* ilipitia tathmini nzima na kuamua

kwa kauli moja kuishauri Serikali kurejea kwenye ushauri wa *PPRA* wa kutumia njia ya *international shopping* ili kupata *quotations* moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji wa mitambo ya kuzalishia umeme kwa gesi.

Mheshimiwa Spika, kesho yake, yaani tarehe 1 Aprili 2006, Waziri wa Nishati na Madini, wakati huo Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge, akionesha dhahiri kutotaka njia ya *international shopping* kutumika, akawaita wajumbe wote wa Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO* na kuwaagiza wahakikishe kuwa Bodi ya Zabuni ya Shirika inawaita tena wazabuni wote waliojitokeza awali na makampuni mengine yoyote yenye uwezo wa kuingiza nchini mitambo hiyo.

Aidha, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge, alisisitiza kwa barua kwamba, nanukuu:-

*“Mshindi wa tenda ya ununuzi wa mitambo mipya atajulikana baada ya idhini ya Serikali kutolewa. Composition ya wajumbe wa TANESCO Tender Board ibadilishwe na kuimarishwa kwa kuwa na wajumbe wenye uwezo na ni pro-active”.*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa agizo hili la Waziri lilikuwa batili kwani Sheria ya Ununuzi wa Umma haimpi Waziri mamlaka ya kuingilia uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Zabuni za mashirika yaliyo chini ya Wizara yake. Agizo hilo la Waziri likafuatiwa na uamuzi wa Waziri Mkuu wa kuliondoa suala hilo mikononi mwa *TANESCO* na kulikabidhi kwa Kamati Maalum iliyokuwa inaundwa na Katibu Mkuu, Hazina, Katibu Mkuu, Nishati na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tarehe 13 Aprili 2006, Mkurugenzi Mwendeshaji wa *TANESCO* wakati huo, Bwana Adriaan Van De Merwe, akaiondoa *TANESCO* rasmi kutoka kwenye mchakato huo kwa kumtumia Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini nyaraka zote kuhusu zabuni yenyewe na uchambuzi wote uliofanywa na *TANESCO (Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa zabuni ndani ya Wizara. Tarehe 20 Aprili 2006, Wizara ya Nishati na Madini iliamua kuunda timu ya wataalamu ili ichague mzabuni mmoja kati ya wanane walioshiriki kwenye zabuni na kufanya naye majadiliano ya mkataba. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ilikuwa tayari imejiandaa na Kamati zake zifuatazo:-

Kamati ya Makatibu Wakuu, Kamati ya Wataalam na Kamati ya Serikali ya Majadiliano.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Makatibu Wakuu, iliundwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 10 Februari 2006, ikiwajumuisha Makatibu Wakuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati hii ilipewa jukumu la kusimamia mchakato mzima wa zabuni. Ili kuharakisha zoezi hilo, Serikali iliunda Kamati ya Wataalam, *Team of Experts*, ili kuisaidia kwa karibu Kamati ya Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule iligundua kuwa Kamati ya Wataalam ndiyo iliyokuwa inafanya maamuzi ya msingi katika mchakato huu na iliyokuwa na

mawasiliano ya karibu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, kwani kufuatana na ushahidi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Gray Mgonja, Kamati ya Makatibu Wakuu ilikutana mara moja tu toka iundwe.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kwanza ya Kamati hiyo ya Wataalam ilikuwa ni kupitia upya na kuichambua tathmini iliyofanywa na *TANESCO*. Kazi ya pili ya Kamati hiyo ilikuwa ni kumpata mzabuni ambaye angeweza kutekeleza mradi huo wa umeme wa dharura kwa haraka. Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati hiyo ikatupilia mbali vigezo vya msingi vilivyotumika na Kamati ya Tathmini ya *TANESCO* na kuweka vyake vivhya vichache, ambavyo, kwa maoni ya Kamati Teule, vilifanana na vigezo vya mchezo wa zamani wa watoto wa sadakarawe; “*mwenye kupata apate, mwenye kukosa akose*”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo vilikuwa, uwepo wa mitambo yenyewe pamoja na mitambo ya akiba, uunganishwaji wake kwenye gridi ya Taifa, hali ya usalama wa mitambo yenyewe kwa kulinganisha na usalama wa gridi ya Taifa, muda wa kuleta mitambo na bei ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni ya Kamati Teule, vigezo hivyo vilikuwa haviendani na uzito na utaalum wa kazi iliyokusudiwa. Pia vilikuwa vinatoa mwanya bayana kwa wazabuni hata walio dhaifu kupenyezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Wataalamu ikawaalika wazabuni wote 8 kwa usaili wa kuwapima kufuatana na vigezo hivyo vipya. Mzabuni mmoja kati ya wazabuni wanane, *M/S GAPCO (T) Ltd* hakushiriki. Baada ya usaili huo, Kamati hiyo ikapata wazabuni wanne ambao walionesha kukidhi vigezo hivyo vipya. Wazabuni hao ni *Richmond Development Company LLC*, *Renco SPA*, *Aggreko International Projects Ltd* na *APGUM Co. Ltd*.

Mheshimiwa Spika, *Aggreko International Projects Ltd* walidai kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa *megawatts* 40 kwa senti za Kimarekani 6.0/*kWh*; *Renco SPA* walidai kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa *megawatts* 60 kwa senti 10.0/*kWh*; *Richmond Development Company LLC* alidai kuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa *megawatts* 100 kwa senti 4.99/*kWh*; na *APGUM Co. Ltd* ilidai kuwa na uwezo kuzalisha umeme wa *megawatts* 100 kwa senti za Kimarekani 5.4/*kWh*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na madai hayo ambayo hayakuwa na uthibitisho, Kamati ya Wataalamu ikaipendekeza *Richmond Development Company LLC* kuingia kwenye majadiliano ya mkataba na Serikali. Katika kuhalalisha ushindi huo wa *Richmond Development Company LLC*, wajumbe wote wa Kamati hiyo ya wataalamu, Waziri wa Nishati na Madini aliyetangulia Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge, Waziri wa sasa wa Wizara hiyo, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mbunge, Katibu Mkuu wake, Ndugu Arthur Mwakapugi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mbunge, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Gray Mgonja na Maafisa wote Waandamizi wa Serikali na *TANESCO* waliotoa ushahidi mbele ya Kamati Teule,

walitoa kauli zilizofanana mithili ya wimbo maarufu kuhusu sifa za *Richmond Development Company LLC* zilizoifanya ishinde, kuwa:-

Kwanza, bei yake ya umeme ilikuwa chini kupita makampuni mengine. Pili, kampuni hiyo ilikuwa na ubia na kampuni kubwa na maarufu duniani ya *Pratt & Whitney* ya Marekani inayotengeneza mitambo mbalimbali ya umeme na tatu, iliwasilisha pendekezo lake kama mwendelezaji miradi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wimbo huo wa Richmond kunoga, Kamati Teule ilishangazwa na udhaifu mkubwa wa hoja hizo uliokuwa haulingani kabisa na ujuzi na uzoefu walionao watendaji wa *TANESCO* na Serikali, hivyo kujenga hisia kuwa *Richmond Development Company LLC* ilibebwa. Kwa mfano, hoja ya kwanza inayohusu bei iliyopendekezwa na *Richmond Development Company LLC* kuwa ilikuwa ndogo, haijitoshelezi. Je, Kamati hiyo ililinganisha bei hiyo na kigezo kipi? Kwani katika kuangalia kumbukumbu za mchakato wa majadiliano, Kamati hiyo haikuwa na kiwango chochote cha makadirio ya bei ya umeme wa kukodi ambacho kingetumika kama kigezo cha kupima unafuu huo kama ulikuwepo badala ya kulinganisha na bei kubwa za makampuni ambayo yalikwishatubebesha mzigo mkubwa wa malipo hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati Teule ilipata tetesi na baadaye ushahidi kuwa *Richmond Development Company LLC* ilikuwa na wapambe ndani ya Wizara ya Nishati na Madini na *TANESCO* waliokuwa wanaipa taarifa, *insider dealing*. Mfano mdogo tu ni wa Ndugu Mohamed Saleh, aliyekuwa Mkurugenzi wa Usambazaji wa *TANESCO* na rafiki wa karibu wa wamiliki wa *Richmond Development Company LLC*. Alishiriki kwenye Kamati ya Wataalam na Kamati ya Serikali ya Majadiliano. Alipostaafu tu *TANESCO*, akawa mmoja wa Wahandisi Waandamizi wa *DOWANS HOLDINGS S.A* iliyochukua majukumu ya *Richmond Development Company LLC*.

Mheshimiwa Spika, pili, hoja ya kwamba kampuni hiyo ilikuwa na ubia na kampuni kubwa ya *Pratt & Whitney*, haikuwa ya kweli. Katika mchakato wote wa zabuni ndani ya *TANESCO*, moja ya masuala kadhaa yaliyoifanya *Richmond Development Company LLC* isitiwe maanani, ni ukosefu wa ushahidi wa kisheria wa ubia, *Consortium Agreement*, kati yake na *Pratt & Whitney*. Baada ya kubanwa na Kamati Teule kuhusu ushahidi wa mahusiano wa kampuni hizo mbili, Wajumbe wa Kamati ya Wataalamu waliwasilisha mbele ya Kamati Teule ushahidi wa aina mbili. Kwanza, *business card* ya Mzungu mmoja aliyejulikana kwa jina la John Perun aliyejiita mwakilishi wa *Pratt & Whitney* na pili, kivuli cha mkataba wa kurasa nne kati ya *Richmond Development Company LLC* na *Pratt & Whitney* wa kubadilishana taarifa na siyo kuzalisha umeme. Aidha mkataba huo ulikuwa haujathibitishwa na Wakili au shahidi yeyote wa kuaminika kuwa mkataba halali. Kamati Teule imesikitishwa na kushangazwa kwa kiwango cha chini cha umakini kilichoonyeshwa na wataalam wetu hususan kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, viongozi wote wa Serikali waliohojiwa na Kamati Teule walisisitiza kuwa uamuzi wa kuipa *Richmond Development Company, LLC* kazi hiyo ya

kuzalisha umeme wa dharura, ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na madai ya kampuni hiyo kuwa na ubia na kampuni maarufu ya *Pratt & Whitney*. Hivyo basi, ushahidi wa uhusiano wa kisheria wa Kampuni hizo mbili, ulikuwa suala la msingi ambalo wataalamu wetu waliwajibika kulipa uzito ili kulinda maslahi ya nchi.

Katika tovuti yake, [www.rdevco.com](http://www.rdevco.com), *Richmond Development Company LLC* ilikuwa inajitangaza kimataifa kuwa kampuni yenye miradi mikubwa Tanzania ya ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha michezo, ujenzi wa bomba la mafuta la kilometa 1,150 na ukarabati wa viwanja kadhaa vya ndege nchini. Kamati Teule ilishindwa kuelewa kwa nini Kamati ya Wataalam haikuihoji *Richmond Development Company, LLC* kuhusu uongo huo bayana ambao ulikuwa ushahidi wa kutosha kuipotezea sifa za kuwa mzabuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, ya kwamba *Richmond Development Company, LLC* ni mwendelezaji miradi, ilitakiwa vile vile ifanyiwe kazi badala ya kuiamini tu. Wizara ya Nishati na Madini haiwezi kukwepa lawama kwa kufumbia macho ukweli kuwa *Richmond Development Company, LLC* ilishakuwa na mkataba na Wizara hiyo uliosainiwa tarehe 30 Juni 2004, mkataba uliovonjika mwezi Januari 2006 kwa kampuni hiyo ya Kimarekani iliyojitambulisha kama mwendelezaji miradi kushindwa kutekeleza sehemu yake ya mkataba. Wizara inaelewa fika kuwa kampuni hiyo ilishindwa utekelezaji kutokana na kuyumba kifedha. Mwendelezaji miradi gani ambaye anashindwa kumudu hata fedha ya kununulia maafisa wake tiketi ya ndege kutoka Dar es Salaam hadi Afrika Kusini na kurejea, kama ilivyoelezwa na Mkurugenzi wa *Tanzania Green Company Ltd* katika mahojiano na Kamati Teule?

Mheshimiwa Spika kama tulivyodokeza hapo awali, baada ya Kamati ya Wataalam kumaliza kazi yake na kuwasilisha taarifa Serikalini, Kamati ya Serikali ya Majadiliano, *Government Negotiation Team*, ikiwa na wajumbe kutoka *TANESCO*, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Benki Kuu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikaanza mchakato wa majadiliano ya mkataba na *Richmond Development Company LLC*.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyotokea kwa Kamati ya Wataalam, *Government Negotiation Team* vile vile haikufanya kazi ya kuridhisha japokuwa ilikuwa na uwakilishi mpana. Kwa mfano, suala la kukosekana kwa *Consortium Agreement* kati ya *Richmond Development Company LLC* na *Pratt & Whitney* halikuwasumbua kabisa wajumbe wa Kamati ya Serikali ya Majadiliano. Wajumbe hao, akiwemo mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waliichukulia *business card* ya Bwana John Perun na mkataba wa kubadilishana taarifa kati ya kampuni hizo mbili kuwa ushahidi wa kutosha wa ubia au ushirikiano. *GNT* ilishindwa hata kusisitiza kuwa ubia wa kampuni hizo uwekwe wazi katika mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Cpompant LLC*.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuelewa kuwa *Richmond Development Company LLC* haikufanyiwa uchunguzi wa awali, *due diligence*, *GNT* ilishindwa kupendekeza kwa Serikali umuhimu wa kuifanyia Kampuni hiyo uchunguzi baada ya kuiteua, *post-qualification*, kujua uwezo wake kifedha, kiutendaji, kiutalaam na kiuzoefu. Katika

mahojiano na Wajumbe wa *GNT*, Kamati Teule iligundua kuwa masuala mengi waliyapitisha kwa mazoea tu, baadhi ya wajumbe wake wakiamini kuwa mikataba ya aina hiyo inatoka Benki ya Dunia na vipengele vyake havibadiliki. *GNT* ilifika mahali ikakubali bila vigezo vya kueleweka kwamba *Richmond Development Company LLC* ikichelewesha utekelezaji wa mradi itailipa *TANESCO* faini ya Dola za Kimarekani 10,000 au sh. milioni 12.5 tu kwa siku, lakini *Richmond* itaidai *TANESCO* ilipe Dola za Kimarekani 121,811 au sh. milioni 152 kila siku hadi mwisho wa mkataba kama gharama za kudumu za uwezo wa mitambo yao, *capacity charges*, wazalishe umeme, wasizalishe! Mheshimiwa Spika, Haiingii akilini! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Juni, 2006, Bodi ya Zabuni ya *TANESCO* ilikutana na kupitisha uamuzi rasmi wa kufuta zabuni waliyokuwa wanashughulikia awali na kutangaza kuwa “*TANESCO isihusishwe na mkataba wowote utakaotokana na nyaraka za zabuni waliyoifuta*”.

Mheshimiwa Spika, lakini siku hiyo hiyo ya tarehe 19 Juni 2006, Waziri wa Nishati na Madini alimwandikia Waziri Mkuu dokezo kuwa majadiliano ya awali na *Richmond Development Company LLC* yamekamilika hivyo Serikali iiteue kampuni hiyo kwa lengo la kuingia mkataba na *TANESCO* wa kuzalisha umeme wa dharura kwa miaka miwili. Sehemu ya barua hiyo inasomeka, nanukuu:-

“*Kamati ya Serikali ya Majadiliano (GNT) inayojumuisha wataalam kutoka Wizara Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Benki Kuu na TANESCO ilifanya majadiliano na Richmond Development Company, LLC ya Houston, Marekani kutoka tarehe 8 hadi 16 Juni 2006, kwa kuzingatia maelekezo yako.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Juni 2006, Katibu wa Waziri Mkuu Ndugu B. Olekuyan aliiandikia Wizara ya Nishati na Madini kuitaarifu kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amekubali mapendekezo na ushauri wa Waziri wa Nishati na Madini kama ulivyokuwa umeletwa.

Mheshimiwa Spika, siku hiyo hiyo tarehe 21 Juni, 2006, Waziri wa Nishati na Madini, akamwandikia dokezo Katibu Mkuu wake, aiagize *TANESCO* iingie mkataba mara moja na *Richmond Development Company LLC*, baada ya Waziri Mkuu kuidhinisha mapendekezo ya Wizara. Muda mfupi baadaye, kwa kutekeleza agizo la Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, akamwandikia barua Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO*, Balizi Fulgence Kazaura, kumwagiza ahakikishe kuwa, *TANESCO* inasaini mkataba na *Richmond Development Company LLC*.

Mheshimiwa Spika, Ijumaa ya tarehe 23 Juni, 2006, Kaimu Mkurugenzi Mwendeshaji wa *TANESCO*, Bwana Johannes G. Lottering, alitwa Wizara ya Nishati na Madini na kuagizwa kusaini Mkataba huo kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*. Pamoja na kusita kwake kwingi, hatimaye alisaini mkataba huo.



Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, inaelewa hisia walizokuwa nazo viongozi wa ngazi mbalimbali wa *TANESCO*, kutokana na uongozi wa kiimla wa Wizara, ukipata nguvu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Tulichokiona awali kwa maana ya mchakato wa Zabuni kuchukuliwa na Wizara, ulikuwa ukiukwaji wa sheria na utaratibu mzima wa uwajibikaji. Pamoja na dharura iliyokuwa inaikabili Taifa, Serikali haiwezi kuwa kinara wa kuvunja sheria za nchi. Maoni ya Kamati Teule mi kuwa, Wizara ilikiuka siyo tu masharti ya sheria na kanuni za ununuzi wa umma, bali vilevile maagizo mbalimbali ya Baraza la Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule isingelikerwa sana na matukio haya, kama Wizara ambayo ni taasisi ya ununuzi (*Procurement Entity*), kama ilivyo *TANESCO*, ingemalizia mchakato wake kwa kusaini mkataba huo yenyewe. Kuishinikiza *TANESCO* kusaini mkataba ambao vyombo vyake halali vilikuwa havijaupitia ni udanganyifu na upotoshaji wa hali ya juu wa taratibu za kazi na sheria. Vilevile udhalilishaji wa vyombo vya maamuzi ndani ya *TANESCO*. Inashangaza kuwa, baada ya kudhalilishwa na Wizara kwa kiwango hicho, chombo kikuu cha maamuzi cha *TANESCO*, yaani Bodi ya Wakurugenzi, hakikuchukua hatua ya heshima ya kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyodokeza awali, Kamati Teule ilishindwa kubaini moja kwa moja, chanzo cha ujasiri wa kiburi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini, kiasi cha kupindisha maamuzi ya Baraza la Mawaziri bila wasiwasi wowote; kukaidi ushauri wa kitaalamu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma, mara tatu mfululizo na kinyume na maagizo ya Baraza la Mawaziri yaliyotaka Sheria ya Ununuzi wa Umma izingatiwe; kukiuka sheria kwa makusudi kwa kuingilia mchakato wa zabuni wa taasisi nyingine ya ununuzi; kuvipuza vyombo vya ndani vya maamuzi vya *TANESCO*, yaani Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Zabuni na kadhalika; kuilazimisha Bodi ya Menejimenti ya *TANESCO* kuridhia maamuzi yaliyofanywa na Wizara ya kuibeba *Richmond Development Company LLC* kinyume cha sheria na taratibu na kadhalik. Aidha, Kamati Teule ilishangazwa kama nilivyosema na Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyokuwa ikifuatilia kwa karibu mchakato huo na kushindwa kukemea ukaidi huo wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mashahidi, wakiwemo waandishi wa habari mashuhuri nchini, waliinyooshea kidole Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa, msingi wa ubabe uliokithiri wa Wizara ya Nishati na Madini katika kuibeba *Richmond*. Aidha, baadhi ya nyaraka ambazo Kamati Teule ilizipata katika uchunguzi wake, zilionyesha kuwa, maelekezo na maamuzi mengi ya msingi yalikuwa yanafanywa na Waziri Mkuu, badala ya Wizara. Mfano ni barua kutoka Wizara ya Nishati na Madini kwenda kwa Waziri Mkuu, niliyokwishainukuu ukurasa wa 31 wa taarifa hii, ikitamka wazi kuwa, *GNT* ilifanya majadiliano na *Richmond Development Company LLC* tarehe 8 hadi 16 Juni, 2006, kwa kuzingatia maelekezo ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tarehe 13 Julai, 2006, Waziri wa Nishati na Madini, akamwandikia Katibu Mkuu wake kuwa, ninanukuu: “Nimezungumza tena na Mheshimiwa Waziri Mkuu leo, juu ya bei ya mitambo ya Aggreko. Msimamo ni ule ule niliokueleza awali na ameagiza tuulizie *Richmond* kama anaweza kutoa 40 MW kwa bei

isiyozidi ile ile ya 4.99 cents per kWh na kama tunaweza kuipata basi achukuliwe *Richmond*.”

Mheshimiwa Spika, ushiriki huu wa karibu wa Waziri Mkuu, katika kila hatua ya zabuni ya umeme wa dharura si lazima uwe ushahidi wa kwamba, kiongozi huyo wa kitaifa alihusika katika kuibeba *Richmond*. Unaweza pia ukawa ushahidi wa staili yake ya kawaida kabisa ya uongozi katika kufuatilia masuala yote ya kitaifa kwa karibu sana, tukizingatia kwamba, nchi wakati huo ilikuwa katika kipindi kigumu sana cha ukosefu wa umeme. Watu pekee waliokuwa wanaujua ukweli ambao ungeipa Kamati Teule msingi wa kumhoji Waziri Mkuu kwa kiapo, walikuwa watatu; Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Katibu Mkuu, Ndugu Mwakapugi na Mwenyekiti wa Bodi, Balozi Kazaura.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ikawaita kwa mara ya pili; Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Ndugu Mwakapugi, kwa mahojiano zaidi. Wote wawili, wakiwa ndani ya kiapo, walikataa katakata kupokea maagizo kutoka kwa Waziri Mkuu ya kuipa *Richmond* upendeleo. Mheshimiwa Dr. Ibrahim S Msabaha, baada ya mahojiano chini ya kiapo, akaiuma sikio Kamati Teule kuwa, katika suala hilo, yeye atakuwa kondoo wa kafara tu au kwa maneno yake mwenyewe “*Bangusilo*” kwa Lugha ya Kizaramo.

Maelezo hayo ya ziada nje ya kiapo ya Mheshimiwa Waziri, yaliyotoa ujumbe kuwa si yeye ila mkuu wake wa kazi, yalioana na maelezo aliyoyatoa Balozi Kazaura nje ya kiapo, tarehe 30 Novemba, 2007. Mara baada ya kumaliza mahojiano kwa kiapo na Kamati Teule, Balozi akatoa maelezo ya ziada kuwa, *Richmond* ilikuwa mradi wa Bwana Mkubwa na mshiriki wake mkubwa kibiashara, akimaanisha Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rostam Aziz. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumelazimika kueleza hata mambo tuliyoielezwa kwa siri kiungwana (*in confidence*), kutokana na uzito wa suala lenyewe na dhamana kubwa tuliyopewa na Bunge hili Tukufu ya kuelezea kilichotokea kwa uwazi na ukweli. Ushahidi huu wa ziada na nje ya kiapo wa viongozi hawa wawili, haukutoa msaada stahili kwa Kamati Teule, kwa kuwa msingi wa maamuzi yote ya Bunge si minong’ono au tetesi, bali taarifa zenye uthibitisho halisi. Hivyo, ni dhahiri kuwa, kwa watumishi hao waaminifu wa Serikali, isingelikuwa rahisi kumtaja Waziri Mkuu chini ya kiapo. Hatua hiyo, inahitaji ujasiri mkubwa na uzalendo wa hali ya juu. Pamoja na woga uliokuwa dhahiri wa watumishi hao, ushahidi wa maandishi, wa mdomo na kimazingira, ambao Kamati Teule iliupata kutoka kwa mashahidi mbalimbali, unamhusisha Waziri Mkuu na mchakato wa maamuzi katika suala hili la *Richmond*.

Mheshimiwa Spika, uvumi wa kuhusika kwa Waziri Mkuu na baadhi ya washiriki wake wa karibu katika suala hili la *Richmond*, umeenea sehemu nyingi nchini kwa kiwango cha kushangaza. Kamati Teule inaelewa kuwa, uvumi huo unaweza kuwa umechangiwa na mahasimu wake kisiasa, lakini uharaka, urahisi na wepesi wa wananchi kuziamini tetesi hizo, unazua maswali mengi kuhusu imani, taswira na heshima aliyojijengea yeye mwenyewe katika jamii.

Mheshimiwa Spika, maudhui na utekelezaji wa Mkataba kati ya *Richmond* na *TANESCO*; kama tulivyoona awali, Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*, hatimaye ulisainiwa na pande zinazohusika Jijini Dar es Salaam tarehe 23 Juni, 2006. Madhumuni ya Mkataba, yameainishwa wazi katika utangulizi wa Mkataba kuwa, ni kusambaza umeme wa dharura kwa kutumia mitambo ya kukodi ya kuzalisha umeme wa *MW 105.6* kutokana na gesi.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya msingi ya Mkataba huu, yalikuwa kuzalisha na kusambaza umeme wa dharura (*Emergency Power Supply*), katika kipindi cha ukame kilicholikumba Taifa. Ndiyo maana tangazo la awali la zabuni la *TANESCO*, liliweka kipindi kifupi cha miezi 12 tu cha kutumia umeme huo wa dharura na muda huo ungeweza kuongezwa kutegemea hali ya uzalishaji umeme nchini. Mkataba huo umeongeza muda kutoka miezi 12 hadi 24 na kuifanya dhana ya umeme wa dharura, ipotee kabisa katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, haikuona mantiki ya kuongeza muda mapema hadi miaka miwili, wakati fursa ya kuongeza muda baada ya mwaka mmoja ilikuwepo, kutegemeana na hali ya mvua nchini. Uamuzi wa kuongeza muda kabla ya kutathmini hali ya mvua na upatikanaji maji kwenye mabwawa yetu ya kuzalishia umeme, ulikosa uzalendo na hauwezi kukwepa tuhuma ya ufidiaji. Uamuzi huo umeibebesha nchi gharama kubwa zisizo za lazima, kwani miezi sita tu baada ya kusaini Mkataba huo, mabwawa ya kuzalishia umeme nchini yalikuwa yameshajaa.

Hivyo, tunalazimika chini ya Mkataba huo, kulipia mbali na gharama ya umeme wenyewe, uwepo wa mitambo hiyo nchini, yaani *capacity charges*, kwa gharama ya shilingi milioni 152 kila siku, kwa miaka miwili mfululizo badala ya mwaka mmoja. Aidha, kutokana na mabwawa yetu kuzalisha umeme usio na gharama kubwa, mitambo hiyo ya kukodisha, ambayo umeme wake ni ghali, hutumika chini kabisa ya kiwango kilichokusudiwa (*under utilisation*).

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inasisitiza kuwa, udharura wa mradi huu, ulimalizika pale mabwawa yetu yalipoanza kujaa maji polepole, kutokana na mvua kubwa zilizokuwa zinanyesha nchini mwishoni mwa Desemba, 2006 na kufikia kilele stahili mapema mwezi Februari, 2007. Hivyo, kitendo cha Wizara kuikubalia kampuni iliyoshindwa kutekeleza sehemu yake ya Mkataba kwa wakati muafaka, *Richmond Development Company LLC*, kuyahamishia majukumu yake kwa kampuni nyingine ya *Dowans Holdings S.A*, bila kuufanyia Mkataba huo marekebisho stahili ya kuipunguzia nchi mzigo wa malipo, hakikuwa cha kizalendo bali cha kukidhi maslahi binafsi ya kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbali na hoja hiyo, tulikuwa na fursa ya wazi ya kuuvunja Mkataba huo bila madhara yoyote ya kisheria, chini ya kifungu cha 12.3 cha Mkataba. Tarehe 27 Oktoba, 2006, *TANESCO* ilichukua hatua ya kwanza kuelekea huko kwa kuitumia *Richmond Development Company LLC* taarifa ya tahadhari (*Default Notice*), iliyoelezea mapungufu ya *Richmond* yalitohitaji majibu ya uhakika: kushindwa kwa kampuni hiyo kusafirisha angalau mtambo wa kwanza wa wastani wa *unit 22 kW* kuja Tanzania; kushindwa kwa kampuni hiyo kutoa taarifa za mara kwa mara za maendeleo ya

utekelezaji wa mradi; uwepo wa kampuni hiyo Marekani kihalali; na uwezo wa kampuni hiyo kitaalam na kifedha, kuweza kutekeleza Mkataba huo wa umeme wa dharura katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, kimya cha *Richmond*, kikailazimu *TANESCO* kuiandikia tena kampuni hiyo tarehe 17 na 23 Novemba, 2006 kuikumbusha kuhusu hoja zake za awali ambazo hazikujibiwa na kudai maelezo kuhusu taarifa za kwamba, kampuni hiyo haikuwa na mahusiano na *Pratt & Whitney*, iliyotegemewa sana kubeba sehemu kubwa ya majukumu ya mradi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini, haikufurahishwa na mwelekeo huo wa *TANESCO* wa kuvunja Mkataba huo, licha ya kwamba, hali ya maji nchini ilizidi kuwa nzuri na kampuni hiyo ya Marekani ilikuwa haionyeshi dalili ya kuweza kutekeleza mradi huo kinyume na makubaliano.

Aidha, *TANESCO* ilikuwa imepata uthibitisho usio na shaka kutoka kampuni mashuhuri ya mawakili ya Virginia, Marekani iitwayo *Hunton & Williams LLP* kwamba, *Richmond Development Company LLC* ilikuwa kampuni ya mkobani (*Brief-case Company*).

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazir Karamagi, kupitia kwa Kamishna wa Nishati, Ndugu Bashir Mrindoko, akamtaka Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO*, ajieleze kulikoni anaitumia *Richmond* taarifa za tahadhari, zenye mwelekeo wa kuvunja Mkataba. Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* akajieleza kwa barua, aliyomwandikia Waziri moja kwa moja, yenye Kumb. Na. MD/003 ya tarehe 23 Novemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, siku tano tu baada ya Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* kujieleza, yaani tarehe 28 Novemba, 2006.

Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*, Balozi Kazaura, alimtaarifu Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* kwa barua kwamba, asubuhi ya siku hiyo alikuwa kapigiwa simu na Waziri, Mheshimiwa Nazir Karamagi, akiwa Jijini Calgary, Canada, akimwarifu kwamba, *Richmond Development Company LLC* walikuwa wanataka kuhamisha majukumu yao yaliyobaki katika Mkataba wa uletaji mitambo na uzalishaji umeme wa dharura kwa kampuni nyingine.

Kufuatana na barua ya Balozi Kazaura, yenye Kumb. Na. SEC.216/C/RDC ya tarehe 28 Novemba, 2006, Mheshimiwa Waziri aliagiza, pamoja na mambo mengine kuwa, *TANESCO* iangalie kama Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*, unaruhusu kukabidhi majukumu kwa kampuni nyingine.

Mheshimiwa Spika, siku hiyo hiyo ya tarehe 28 Novemba, 2006, Uongozi wa *TANESCO* ulimshauri Mwenyekiti wa Bodi, amtaarifu Mheshimiwa Waziri kwamba, kifungu cha 15.12 cha Mkataba huo, hakiruhusu kukabidhi majukumu ya Mkataba kwa Kampuni nyingine, isipokuwa kwa maafikiano ya pande mbili za Mkataba.

Hatimaye, siku sita baadaye, yaani tarehe 4 Desemba, 2006, *TANESCO* ikapokea barua kutoka kwa *Richmond Development Company LLC*, ikielezea makusudio ya *Richmond* kuhamisha majukumu yake yote ndani ya Mkataba huo kwenda kwa *Dowans Holdings, S.A.*

Mheshimiwa Spika, siku hiyo hiyo, *TANESCO* ikaijibu *Richmond* kwamba, haikuwa tayari kuridhia pendekezo hilo kwa sababu kuu tatu:-

(i) Kifungu 15.12 cha Mkataba, kinataka kuwepo kwa makubaliano ya pamoja ya kimaandishi (*Written Mutual Agreement*), kutoka kwa wahusika wote wa Mkataba (*Parties*), kabla ya kufikiwa uamuzi wa kuhamisha Mkataba.

(ii) *Richmond Development Company LLC*, haijatoa sababu zozote za msingi kwa pendekezo hilo la kuhamisha Mkataba.

(iii) *TANESCO* haifahamu historia, uzoefu wala uwezo wa kifedha wa hao wanaopendekezwa kuhamishiwa Mkataba. Mheshimiwa Spika, aidha, *TANESCO* ilikumbushia barua zake za awali, ilizoiandikia *Richmond Development Company LLC*, kuhusu ukiukwaji wa masharti ya Mkataba, lakini *Richmond* haikuzijibu. Hivyo, *TANESCO* ikataka ipate kwanza majibu ya masuala yote iliyoyainisha kabla ya kufikiria kuridhia pendekezo la kuhamisha Mkataba huo. Mheshimiwa Spika, kama kawaida ya Wizara ya Nishati na Madini, *TANESCO* ikashinikizwa kukubaliana na ombi la *Richmond*, hata kabla kampuni hiyo ya Kimarekani, haijajibu hoja za msingi za *TANESCO*.

Tarehe 21 Desemba, 2006 *TANESCO* ikaiandikia barua *Richmond Development Company LLC* kukubali pendekezo la kuhamisha majukumu yake kwa *Dowans Holdings, S.A.* Mheshimiwa Spika, uamuzi huo wa kuruhusu uhaulishwaji wa Mkataba kipindi ambacho nchi ilikuwa imeondokana na hali ya dharura, tena kwa masharti yaleyale ya kulaliwa, yanayoweza kukubalika pale tu ambapo nchi imebanwa kweli kweli na tatizo, ulimfedhehesha hata Mkurugenzi Mwendeshaji wa *Dowans Holdings S.A.*, Bwana Guy Piccard, raia wa Kanada. Alipohojiwa na Kamati Teule tarehe 27 Desemba, 2007, Bwana Piccard, alisema haoni kwa nini Mkataba huo usiangaliwe upya kutokana na mazingira ya udharura kutokuwepo. Mheshimiwa Spika, nimeeleza awali kuwa, mbali na kulipia gharama ya umeme wenyewe, *TANESCO* inawajibika chini ya Mkataba huo, kulipa gharama za uwezo wa mitambo (*Capacity Charges*), ambazo ni shilingi milioni 152 kila siku hadi mwisho wa Mkataba.

Aidha, chini ya Mkataba huo, *TANESCO* inabebeshwa mzingo wote wa kodi, malipo na gharama mbalimbali, zinazoweza kumkabili mwekezaji. Kifungu cha 3.4 cha Mkataba wa *TANESCO* na *Richmond* kinasema: “*All taxes and charges arising in relation to the importation and exportation of the plant, equipment, tools, spare parts, consumables, testing and monitoring equipment or in connection with the supplier’s performance of its obligations under this Agreement generally that become due in accordance with the laws of Tanzania shall be paid for by TANESCO at its sole cost and expense.*” Mheshimiwa Spika, tafsiri ya jumla ya kifungu hiki cha Mkataba ni kwamba, kodi na ada zote zinazohusiana na uingizaji ndani ya nchi na usafirishaji nje ya nchi wa

mitambo yote, vifaa, vipuli na kadhalika na gharama zote zinazohusiana na utekelezaji wa wajibu wa *Richmond*, yaani sasa *Dowans*, chini ya Mkataba, yaani gharama za uendeshaji, matengenezo ya mitambo na gharama ya gesi inayotumika kuzalishia umeme, ni wajibu wa *TANESCO* kuzibeba.

Mheshimiwa Spika, mzigo mkubwa ambao *TANESCO* inabeba chini ya mkataba na *Richmond*, sasa *Dowans*, unajirudia katika mikataba yote mingine kati ya *TANESCO* na makampuni mengine ya umeme kama vile *IPTL*, *AGGREKO*, *ALSTOM* na *SONGAS*, ambayo kwa ujumla yanachukua sehemu kubwa ya mapato ya shirika hilo hivyo, kuvuruga kabisa mizania yake. Kwa wigo wa tafsiri wa mikataba hii inayotuumiza kwa kujitakia, *TANESCO* inawajibika kuwalipia hawa wanaojiita wawekezaji hata gharama za bima na ada za mawakili wao.

Mheshimiwa Spika, tumefikishwa hapa tulipofika na mikataba mibovu, maamuzi ya kiimla na papara ya baadhi ya Watendaji Waandamizi wa Serikali, wasiozingatia maslahi ya muda mrefu ya Taifa letu. *Net Group Solution, PTY*, ambayo kwa kiwango kikubwa imechangia sana katika kuidumaza *TANESCO* kiutaalam na kifedha, iliingizwa *TANESCO* kwa ubabe bila kujali hoja za msingi za wataalam na wafanyakazi wa *TANESCO*. Matokeo yake, sote tunayaelewa.

Vivyo hivyo, *Richmond Development Company LLC*, kampuni isiyo na rekodi yoyote ya kiufundi hata ya kuchomeka *bulb* kwenye kishikio chake, ikapewa mradi mkubwa na Serikali wa kuzalisha umeme wa dharura bila kujali kuhusu ufanisi wake, tena katika kipindi ambacho nchi ilikuwa gizani! Huu ni ujasiri wa kifisadi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa haraka wa Mradi wa Umeme wa Dharura, Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*, ulitoa fursa ya kufunguliwa kwa Barua ya Dhamana ya Benki (*Letter of Credit*), kwa kifupi nitaiita *LC*, kwa madhumuni ya kulipia gharama za maandalizi na za usafirishaji wa mitambo ya uzalishaji wa umeme huo wa dharura. Mkataba ulitaka *TANESCO*, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Fedha na *Richmond Development Company LLC*, waketi pamoja kukubaliana masharti ya *LC* hiyo.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivyo vya Serikali, vilikaa tarehe 7 Julai, 2006, baada ya kupokea mapendekezo kutoka *Richmond Development Company LLC* ya namna ambavyo ingetaka ilipwe. Vyombo hivyo vya Serikali, vikarekebisha kidogo madai ya *Richmond* na kuamua kuwa, kampuni hiyo ilipwe Dola za Kimarekani milioni thelathini, sawa na asilimia 30 ya thamani ya malipo ya Mkataba kwa kipindi cha miaka miwili, kwa masharti kwamba, asilimia 12 ya fedha hizo, ilipwe kama malipo ya awali (*Advance Payment*), baada ya kuwasilishwa hati ya madai (*Invoice*) na hati ya uthibitisho wa udhamini wa Benki (*Bank Guarantee*), kwa *TANESCO* na uthibitisho wa kusafirisha mitambo kuleta Tanzania; asilimia kumi ilipwe baada ya kuwasilishwa hati za kusafirishia mitambo kwa mpangilio wa awamu; na asilimia nane ilipwe mara baada ya uzinduzi wa mitambo.

Mheshimiwa Spika, siku tatu baadaye, *Richmond Development Company LLC*, ikataka masharti hayo yarekebishwe ili kuipa kampuni hiyo unafuu zaidi, wazo ambalo

TANESCO ililikataa kwa kuhofia kuwa, kampuni hiyo ingeweza kupotea baada ya kupata malipo ya awali yasiyo na masharti magumu. Tarehe 27 Julai, 2007, Wizara ya Nishati na Madini, ikaingilia kati mmutano huo na kuitisha kikao kilichosimamiwa na Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, kama Mwenyekiti. Kikao hiki kilihusisha Wajumbe kutoka Wizara ya Fedha, TANESCO, Benki Kuu ya Tanzania, Mwakilishi kutoka CTI na Richmond Development Company LLC. Kama ilivyokuwa kwa kikao cha tarehe 7 Julai, 2006, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wala mwakilishi wake, hawakuhudhuria.

Mheshimiwa Spika, ninashindwa hata kufanya *summary* kwa sababu muda ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nisome mapendekezo ya Kamati tu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwa Kanuni, kama mnataka asome taarifa yote, itabidi tuitengue Kanuni inayotoa saa moja. Safari iliyopita kuhusu lile suala la nusu saa au saa moja, nimepata lawama, lakini lazima nishikilie Kanuni. Sasa lazima itolewe hoja kwa mujibu wa Kanuni, kwa sababu mtoa hoja yeyote amepewa dakika zisizozidi 60, labda muamue vinginevyo. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu; mtoa hoja anatakiwa atumie dakika zisizozidi 60. Kwa kuwa, suala lililoko mbele yetu ni suala linalogusa taifa letu; ni suala zito ambalo Bunge lako limekubali kuunda Kamati Teule; ni suala ambalo Taifa limekubali Kamati hiyo itumie fedha za walipa kodi; ninaomba kutoa hoja kwamba, Kanuni hiyo itenguliwe na hotuba hiyo isomwe mpaka itakapomalizika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hoja iliyo mbele yetu sasa ni ya kutengua Kanuni husika, ili kumwezesha mtoa hoja aendelee. Ninadhani hata Kanuni pia bado inasema, kwa muda usiozidi nusu saa. Kwa hiyo, kwa tahadhari hiyo, sasa nitawahoji muamue hoja hiyo.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya kutengua Kanuni kuruhusu mtoa hoja kuongezewa muda ilikubaliwa na Bunge*)

**SPIKA:** Ndugu Wabunge, walioafiki wameshinda. Kwa maana hiyo, ninakuruhusu mtoa hoja, uendelee kwa dakika zisizozidi thelathini. (*Makofi*)

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE (MWENYEKITI WA KAMATI TEULE YA BUNGE):** Ahsante Mheshimiwa Spika. Ninaendelea kusema tu kwamba, kikao hiki kikaamua kurekebishwa kwa masharti ya LC, kama ilivyopendekezwa na Richmond Development Company LLC.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya marekebisho yalikuwa:-

(i) Kampuni hiyo ilipwe asilimia 17.5 ya jumla ya thamani ya Mkataba, baada ya Benki ya kampuni hiyo kupokea hati za usafirishaji wa mitambo (*Shipping Documents*), hati ya bima, orodha ya vifungashio (*Packing List*), hati za uasili wa bidhaa (*Certificate of Origin*), hati za upangaji wa mizigo (*Packing Lists*), pamoja na hati ya madai (*Invoice*), kwa mtambo wa MW 22.

(ii) Kampuni hiyo ilipwe vilevile asilimia 17.5 ya jumla ya thamani ya Mkataba baada ya TANESCO kutoa hati ya uthibitisho ya mitambo kuwasili eneo la kazi (Ubungo, Dar es Salaam).

Mheshimiwa Spika, baada ya makubaliano hayo, tarehe 23 Agosti, 2006, TANESCO iliomba Citibank Tanzania, kufungua LC kwa ajili ya *Richmond Development Company LLC*, yenye thamani ya Dola za Kimarekani 30,696,598.00. Siku hiyo hiyo ya tarehe 23 Agosti, 2006, Citibank Tanzania, iliwajulisha TANESCO kwamba, isingeweza kufungua LC kwa ajili ya *Richmond Development Company LLC*, kutokana na kile walichoeleza kuwa ni kutopata muda wa kutosha, kuchunguza kwa kina uwezo wa mteja anayehusishwa na dhamana ya malipo hayo (*Due Diligence*), kabla ya kuingia Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukataliwa na Citibank, TANESCO waliomba Benki ya CRDB kufungua ULC na tarehe 25 Agosti, 2006, CRDB ikafanya mawasiliano Citibank New York. Tarehe 2 Septemba, 2006, Citibank New York ikaifahamisha CRDB kuwa wao pia wasingeweza kushiriki katika kufungua LC kwa *Richmond Development Company LLC*, kutokana na mahitaji ya lazima ya kuzingatiwa chini ya kifungu namba saba cha Kanuni za UCP 500. Kifungu hicho ndicho kilichowafanya Citibank Tanzania, kukataa kufungua barua kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha benki hizo mbili za Kimarekani kukataa kufungua LC kwa jili ya Kampuni ya Kimarekani, kilitosha kuzua wasiwasi wa msingi kuhusu kampuni hiyo. Kwa kuwa Watanzania tuliishaamua kufa na *Richmond*, tukasonga mbele! Hivyo, tarehe 2 Septemba, 2006, CRDB ikafungua upya LC kwa ajili ya *Richmond Development Company LLC*, kupitia Benki nyingine ya nje iitwayo HSBC, kwa masharti yale yale ambayo CRDB ilipokea kutoka TANESCO. Hatimaye HSBC ikafungua LC kwa ajili ya kampuni hiyo, lakini kwa kutumia jina lingine la RDEVCO na siyo *Richmond Development Company LLC*!

Baada ya LC kufunguliwa na kuthibitishwa, uwajibikaji kwa utekelezaji wa masharti ya Mkataba ulianza rasmi. Hata hivyo, tarehe 4 Oktoba, 2006, *Richmond Development Company LLC*, kwa mara nyingine tena, iliipelekea TANESCO maombi ya kutaka kuifanyia marekebisho LC kwamba:-

(i) LC iruhusu malipo ya awali (*Upfront Payment*), ya Dola za Kimarekani milioni kumi.

(ii) *Richmond Development Company LLC*, iruhusiwe kusafirisha mtambo wa kwanza kwa njia ya ndege kwa gharama ya Dola za Kimarekani 5,696,568.00.



(iii) Asilimia 50 ya Barua ya Dhamana ya Benki, ilipwe baada ya uthibitisho kutoka *TANESCO*, juu ya kupokelewa kwa mitambo nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe hiyo hiyo 4 Oktoba, 2006, Wizara ya Nishati na Madini ikaitisha kikao kujadili maombi hayo. Kikao hiki kilichohudhuriwa na wawakilishi kutoka Wizara ya Nishati na Madini, *TANESCO*, Benki ya *CRDB* na *Richmond Development Company LLC*, kikakubali maombi yote ya *Richmond Development Company LLC* na kuagiza kuwa hatua za utekelezaji zifuatake mara moja. pamoja na ukweli kwamba mchakato mzima ulitawaliwa na udharura, Kamati Teule haielewi ni vipi Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa ikitekeleza kila pendekezo jipya lililotolewa na *Richmond Development Company LLC* bila kujali madhara ambayo yanguwea kutokea pindi kampuni hiyo ingelipwa na kuingia mitini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini kwamba, mapendekezo hayo mapya ya kuibeba *Richmond* yalikuwa nje ya masharti ya *LC*, yaliyoainishwa katika Mkataba wa malipo kati ya *TANESCO*, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Fedha na *CRDB Bank*; Wizara ya Nishati na Madini ikaijulisha Wizara ya Fedha kuhusu maamuzi mapya ya *LC* kutokana na maombi ya *Richmond Development Company LLC*. Wizara ya Fedha haikuridhishwa na mapendekezo yaliyotolewa, kwani malipo yoyote ya awali kutoka fungu maalum la *Multilateral Debt Relief Initiative* ni lazima yafanyike kwa uthibitisho wa kuridhisha.

Sehemu ya barua hiyo iliyoandikwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Ndugu Gray Mgonja, inasema: “Tunaona kuwa tofauti na taarifa zilizotolewa wakati wa majadiliano ya Mkataba kuwa, mkandarasi aliyechaguliwa alikuwa na vifaa tayari kuvileta nchini, sasa ni wazi kuwa si hivyo. Kama unavyojua, msingi wa malipo kuhusu mitambo ya kununua au kukodisha chini ya Mradi wa Nishati ya Dharura, unaofadhiliwa kupitia *IMF* na *MDRI* ni mkataba unaotokana na majadiliano. Ninapenda kupendekeza kuwa, malipo yoyote ya awali kutoka akaunti ya *MDRI*, lazima yaandamane na dhamana ya kuridhisha kutoka kwa mkandarasi. Sharti hili linaonyesha kutokuzingatiwa chini ya mapendekezo yenu.”

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza ni kuwa, pamoja na maelekezo na ushauri huu wa Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, siku hiyo hiyo ikaiandikia barua *TANESCO*, kuitaka itekeleze maombi ya *Richmond Development Company LLC* mara moja na kubadilisha masharti ya malipo; ninanukuu: “*I wish to inform you that the proposed amendments to the existing Letter of Credit are acceptable and you are advised to liaise with CRDB Bank to effect the changes as soon as is practical.*” Barua ya Katibu Mkuu wa Nishati na Madini yenye Kumb. Na. CBD.214/324/01 ya tarehe 6 Oktoba, 2006, inasomeka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, ninaomba unipe muda tu nisogee mbele kuelezea mapendekezo ya Kamati Teule, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, watapata nafasi ya kusoma wenyewe. Kamati Teule, imejiuliza bila kupata majibu; ni nini kilifanyika hadi Wizara ya Nishati na Madini, ikatoa kauli hii ambayo ni tofauti kabisa na ushauri ilioupata kutoka Wizara ya Fedha? Nini msingi wa ukereketwa au ufurukutwa bayana wa Wizara ya Nishati na Madini kuhusu *Richmond*?

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maagizo ya Wizara, *TANESCO* iliandikia barua Benki ya *CRDB*, tarehe 6 Oktoba, 2006, kuitaka ifanye mabadiliko hayo mapya kwenye *LC* ya *Richmond*. Tarehe 9 Oktoba, 2006, Benki ya *CRDB* ilijibu *TANESCO* na kuikumbusha kwamba, *LC* inasimamiwa na makubaliano ya pamoja, chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania. Kwa msingi huo, *TANESCO* ikatakiwa kufuata taratibu kwa kuiomba Benki Kuu ya Tanzania, kibali cha kufanya marekebisho katika kifungu 1(a) cha Mkataba wa makubaliano ya taratibu za malipo ili kuwezesha maombi yaliyopendekezwa, kufanyiwa kazi. Jibu hilo, likailazimu *TANESCO* kufuta maombi hayo.

Hadi *LC* hiyo ya *Richmond* inaisha muda wake (tarehe 30 Novemba, 2006), kampuni hiyo ya Kimarekani, haikuweza kutekeleza sharti hata moja na hivyo, kushindwa kuchukua fedha kama ilivyokuwa imepangwa. Swali linalojitokeza ni je, iwapo *CRDB* ingekubali kubadilisha masharti ya *LC* na kuipa *Richmond Development Company LLC*, fedha ilizoomba bila kibali cha Benki Kuu ya Tanzania; *Richmond* ingeleta nchini mitambo kama ilivyokusudiwa au ingekuwa ni hasara kwa Taifa?

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, mchakato mzima wa *Richmond Development Company LLC* wa kutaka kufanya mabadiliko katika Barua ya Dhamana ya Benki mara kwa mara, unadhihirisha nia yao ya kutaka kupata mtaji. Pia inadhihirisha kwamba, *Richmond Development Company LLC*, haikuwa na uwezo wa kifedha wa kutekeleza Mkataba huu kinyume na tamko kwenye Mkataba kuwa: “*The Supplier (Richmond), has the equipment and the financial and technical capability to construct, install, commission, operate and maintain such a plant as required by TANESCO.*”

Msambazaji, yaani *Richmond*, ana vifaa na uwezo wa kifedha na wa kitaalam; kujenga, kusimika, kuiwasha, kuendesha na kuendeleza mtambo huo kama *TANESCO* inavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati Teule ilijiuliza maswali yafuatayo: Je, utafiti ulifanywa kufahamu gharama halisi za mitambo mipya kutoka kwa watengenezaji wenyewe, bila ya kupitia kwa mawakala?

Kamati Teule ilibaini kuwa, zoezi hilo liliwahi kufanyika mwaka 1998 tu ambapo Wizara ya Nishati na Madini, ilitoa kazi hiyo kwa wataalam wa sekta (*Consultants*) na kufanikisha kugundua kuwa, bei ya mitambo ya umeme ya *IPTL (400 MW)*, ambayo ilitakiwa kuuzwa kwa Dola za Kimarekani milioni 150 (Tsh. 187.5 bilioni); bei yake halisi ilikuwa ni Dola za Kimarekani milioni 85 (Tsh.106.2 bilioni) tu na hivyo kupata kigezo cha kukataa bei yao. Hivyo basi, kutokana uzoefu huo, Wizara ya Nishati na Madini, kwa kushirikiana na *TANESCO*, walitakiwa kufuatilia bei hizo za mitambo na pia makadirio ya kazi za ujenzi ili kupata picha ya gharama halisi ya mradi, jambo ambalo halikufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa Viongozi wa Wizara na *TANESCO* kushindwa kujua bei halisi ya mitambo kutoka kwa watengenezaji wenyewe kwa takribani miaka kumi huku wakisafiri kwenda nje ya nchi kila kukicha kwa mikutano, warsha, makongamano na kadhalika na kwa Wizara kung’ang’ania kutumia mawakala badala ya watengenezaji wa

mitambo, nchi yetu imegeuzwa gulio la wajanja kuikamua na kuwabebesha wananchi mzigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilipotembelea Marekani, iliamua kuwatembelea baadhi ya watengenezaji wa mitambo ya uzalishaji wa umeme huko huko Huston, Marekani, kujua bei za mitambo yao. Mmoja wa watengenezaji wenye jina kubwa duniani, *Kawasaki Gas Turbines - Americas*, anatengeneza na kuuza Mtambo mpya aina ya *GPB180*, wenye uwezo wa kuzalisha *MW 17.5* kwa Dola za Kimarekani 7.5 milioni (Tsh. 9.4 bilioni). Mawakala huwa wanatuletea mitambo ya aina hiyo hiyo, kwa bei mara mbili ya bei halisi.

Iwapo *TANESCO* au Serikali iliweza kufungua *LC* ya Dola za Kimarekani 30,696,598; je, fedha hizo zisingeweza kutosheleza kununua mitambo mipya ya uzalishaji umeme na mitambo hiyo kubakia mali ya *TANESCO*, badala ya kuingia katika Mikataba ya ghali ya kukodisha mitambo? Aidha, taarifa za Watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwamba, wakati wa kipindi cha mchakato wa zabuni ya umeme wa dharura, kulikuwa na ugumu wa kupatikana mitambo ya umeme wa dharura, zimethibitishwa na Kamati Teule kuwa sio za kweli.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba, kulikuwa na ukame, lakini ukame huo haukuwa wa mitambo ya kuzalisha umeme, kwani mitambo hiyo hutengenezwa muda wote na sio kwa kutegemea mvua. Aidha, utafiti wetu umebaini kuwa, katika kipindi hicho cha matatizo ya umeme nchini, makampuni yote ya kutengeneza mitambo hiyo ya umeme, yalikuwa yana mitambo kadhaa ikisubiri wateja. *Kawasaki* ilikuwa na mitambo minane ya kisasa, tena yenye kutumia gesi na dizeli (*Dual Fuel Plant*). Serikali nyingi, ikiwemo ya Nigeria ni wateja wazuri wa kampuni hiyo, ambao huteremshiwa bei kwa mtambo moja hadi Dola za Kimarekani milioni 6.7, badala ya Dola za Kimarekani milioni 7.5 bei ya kawaida.

Kwa thamani ya *LC* iliyofunguliwa kwa *Richmond Development Company LLC* ya Dola za Kimarekani milioni 30.7 au Tsh 38.4 bilioni, *TANESCO* ingeweza kununua mitambo mipya yote minne, pamoja na kumudu kulipia gharama za kusafirisha kwa meli hadi Dar es Salaam. Hivyo, ili zipatikane *MW 105.6* zilizohitajiwa na *TANESCO*, ingehitajika mitambo sita ambayo ni sawa sawa Dola za Kimarekani milioni 45 au Tsh. 56.25 bilioni, badala ya Dola za Kimarekani milioni 87 au Tsh. 108.7 bilioni, tulizobebeshwa na *Richmond Development Company LLC*. Je, si dhahiri kuwa, hii ndiyo ilikuwa nia ya *Richmond Development Company LLC*, yaani kupata fedha za malipo ya awali (*Advance Payment*), ili ikatununulie mtambo mmoja na kuja kutukodisha sisi wenyewe hivyo, kufaidika na *capacity charge* ya kila mwezi kwa Mkataba wa miaka miwili? Kwa mtambo mmoja wa *MW 22*, *capacity charge* ni Dola za Kimarekani takriban 730,871 au Tsh. Milioni 913.6 kwa mwezi hivyo, kwa miezi 24 ni wastani wa Dola za Kimarekani 17,540,912 au Tsh. Bilioni 21.9.

Kwa kuwa thamani ya *LC* inalipwa kama malipo ya awali (*Advance Payment*); je, hii si sawa na kutoa mkopo kwa *Richmond Development Company LLC*? Kamati Teule inaona kwamba, hiyo ni sawa na kutoa mkopo usio na riba kwa mfanyabiashara wa nje ili awe mwekezaji.

Kwa nini katika Mkataba wa *Richmond Development Company LLC*, kifungu cha kufidia malipo ya awali (*Advance Payment*) ya *LC*, hakikuwekwa bayana ndani ya Mkataba, tofauti na Mikataba mingine, badala yake ikawekwa fursa ya kujadiliana na mkandarasi? Kamati Teule, haioni sababu yoyote ya msingi, mbali na wahusika kujiwekea fursa ya kukidhi maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tu ni kwamba, uamuzi wa Serikali wa kuipa *Richmond Development Company LLC*, zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura wa *MW 105.6* na baadaye kuingia mkataba na *TANESCO*, ulizua mjadala wa manung'uniko ya wananchi wa kada mbalimbali, walioshuhudia kushindwa kwa kampuni hiyo kutekeleza mradi huo katika muda muafaka. Umma wa Watanzania wa kawaida, wanasiasa, wasomi, wanataaluma, wanahabari na wadau mbalimbali, hawakusita kuilalamikia Serikali kwa uteuzi huo wa *Richmond*, ambao walihisi kuwa uligubikwa na maslahi binafsi ya baadhi ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*) na Taasisi ya Kuzuia Rushwa (*TAKURU*), ambayo sasa ni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*TAKUKURU*), kwa mamlaka ya kisheria ambayo taasisi hizi inayo, zikaamua kulichunguza suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, *PPRA* ilifanya uchunguzi makini na wa kina, kujua kama Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma zilifuatwa. Taarifa hiyo imebainisha wazi kuwa, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutaka kuiokoa nchi kutokana na hali mbaya ya umeme, mchakato mzima wa zabuni, ulikiuka Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2005, kama tulivyoelezea kwa kina sehemu ya pili ya taarifa hii fupi. Kwa ujumla, Kamati Teule imeridhishwa na taarifa ya *PPRA*, ambayo imeandikwa kitaalamu, ikiwa na vielelezo vya wazi ambavyo Mamlaka imevitumia.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, uchunguzi uliofanywa na *TAKURU*, ambao taarifa yake unadai kuwa ulikuwa wa kina na wenye umakini wa hali ya juu, ulibaini pamoja na mambo mengine kwamba: Mchakato wa kumpata mzabuni ulikuwa wa wazi na shindanishi; Hakuna ushahidi uliopatikana kuthibitisha vitendo vya rushwa, uzembe na hata kupokea kamisheni. Pia hakuna ushahidi uliopatikana wa Afisa yeyote Serikalini, kumiliki hisa au kuwa na madaraka katika *Richmond Development Company LLC*; Kamati Maalum iliyoundwa haikupata muda wa kutosha kuifanyia uchambuzi wa kina, *Richmond Development Company LLC* ili kufahamu uwezo wake kiufundi na kifedha na badala yake, ilitegemea uwezo wa Kampuni ya *Pratt & Whitney* kama kigezo cha kuipatia *Richmond* zabuni; Utafiti wa kina haukufanywa, kutambua uwezo wa Kampuni ambayo ingepaswa kusimamia shughuli za *Richmond Development Company LLC*, yaani *Richmond Development Company (T) Ltd*; na Mapungufu machache yalikuwepo, lakini ya kawaida kiutendaji na hayakuhusisha rushwa au manufaa ya aina yoyote ile kwa Watendaji wa Serikali na wala hakuna hasara iliyosababishwa na upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, ilishindwa kuona mantiki ya matokeo ya uchunguzi wa *TAKURU* kama ifuatavyo:- Mchakato ambao *TAKURU* imedai kuwa ulikuwa wa wazi na shindanishi, uliendeshwa na Wizara ya Nishati na Madini, bila

kuzingatia taratibu za sheria na kanuni za ununuzi wa umma. Kamati Teule imeshindwa kuelewa ni mbinu zipi taasisi hii ilitumia katika kueleza kuwa mchakato wa zabuni ulifanywa kwa uwazi na kuwa shindanishi. Je, uwazi gani na ushindanishi gani ulikuwepo kwa Wizara ya Nishati na Madini, ikishirikiana kwa karibu na Ofisi ya Waziri Mkuu, kusitisha mchakato wa zabuni ndani ya *TANESCO* na kuunda chombo kipya nje ya taratibu ili kumteua mzabuni kwa niaba ya *TANESCO*? Hoja ya TAKURU kuwa kulikuwa na mapungufu, lakini mapungufu hayo yalikuwa ya kawaida, ambayo hayajengi makosa ya jinai, haina msingi. Kwa Wizara kuilazimisha taasisi nyingine ya ununuzi, yaani *TANESCO*, kusaini Mkataba ambao haukupitishwa na vyombo vyake halali vya maamuzi; kwa kampuni hiyo ya Kimarekani kujitambulisha kwa majina mengi katika barua tofauti tofauti mara *Richmond Development Company LLC*, mara *RDC*, *RDVECO* na mara nyingine *RDEVCO*; yote haya kwa TAKURU ni makosa ya kawaida ya kiutendaji! (*Makofi*)

Taarifa ya TAKURU imeeleza kwamba, *Richmond Development Company LLC*, ilikuwa ifunguliwe *Letter of Credit* yenye thamani ya Dola za Kimarekani 30,696,598.00, lakini haikuona jitihada za kampuni hiyo, kujaribu kubadilisha masharti ya *LC* hiyo mara tatu. TAKURU haikushangazwa na Mabenki ya Kimarekani kukataa kuihudumia kampuni ya Kimarekani!

TAKURU haikushangazwa na kiherehere cha Wizara ya Nishati na Madini, kutekeleza matakwa ya kampuni hiyo hata pale ambapo yalikuwenda kinyume na makubaliano ya msingi? TAKURU haikuona hasara ambayo nchi ilipata kutokana na zabuni hiyo wakati kila mwananchi aliona hasara bayana, kwa nchi kukosa umeme kwa kipindi kirefu na kuathiri uzalishaji mali na huduma za lazima nchini?

TAKURU iliamini kuwa, hakukuwa na uzembe. Je, kwa Wizara na Watendaji mbalimbali wa Serikali kuamini kuwa *Richmond Development Company LLC* na *Pratt & Whitney*, zilikuwa na ubia bila kudai nyaraka za ubia; kwa Viongozi wa Serikali kumwona tu Mzungu na *business card* yake na kuamini moja kwa moja kuwa ni mwakilishi wa *Pratt & Whitney* wakati siyo; kwa Serikali kuamua kusaini Mkataba na kampuni ambayo haijafanyiwa uchunguzi wa kina, kujiridhisha kuwa si kampuni hewa au ya mkobani; hivyo vyote kweli si uzembe?

Pamoja na kuwajibika kisheria kujisajili kwenye Bodi ya Usajili ya Makandarasi na wahandisi wake kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*ERB*), *Richmond Development Company LLC* haikufanya hivyo na ililindwa na Wizara ya Nishati na Madini kubaki kama ilivyokuwa; hilo nalo TAKURU haikuliona?

*Richmond Development Company LLC*; haikuwa na nyaraka zozote za kikampuni kuonyesha kuwa imesajiliwa Marekani; haikuwa na uthibitisho wa kibenki kuwa ina fedha za kuendesha mradi wa umeme ili kupata sifa ya uwekezaji nchini; haikuwa na *Business Plan* iliyoandaliwa vizuri na kwa uangalifu, lakini ikapata huduma ya haraka Kituo chetu cha Uwekezaji na kupewa *Certificate of Incentives*?

Mheshimiwa Spika, ikizingatiwa kuwa TAKURU ni taasisi nyeti Kitaifa, ambayo ina uwezo wa kutosha kitaaluma, kifedha na kirasilimali, katika kufuatilia masuala

mbalimbali ya uchunguzi, haikuwatendea haki Watanzania kwa kazi ya ubabaishaji iliyofanya.

Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai wa TAKURU, Ndugu Alex Mfungo, alitetea Taasisi yake mbele ya Kamati Teule kuwa, ilifanya uchunguzi kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1971, iliyokuwa na mapungufu mengi na kwamba, ilikuwa vigumu sana kuthibitisha madai ya rushwa yaliyokuwa yanalalamikiwa na wananchi

Mheshimiwa Spika, pamoja na utetezi huo, bado TAKURU haikufanya kazi iliyotegemewa na wananchi ya kufichua uovu. Ilichofanya ni kuuficha ukweli kwa hoja za ubabaishaji. Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya habari hususan magazeti; vilifanya kazi kubwa mno na ya ziada katika kutafuta ukweli kuhusu suala hili; ni vyombo hivi vya habari kupitia makala mbalimbali, tahariri na taarifa maalum, vilivyoamsha shauku ya wananchi kuhusu suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua fursa hii, kuvipongeza vyombo vyote vya habari, wamiliki wake, wahariri, waandishi wa habari, watangazaji na wapiga picha, kwa ujasiri na moyo wa kizalendo katika kupambana na kila aina ya ufiadini kwa kutumia kalamu. (*Makofi*) Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa karibu wa vyombo vya habari kuhusu suala hili, ulikuwa moja ya sababu kubwa kwa *Richmond Development Company LLC*, kujitoa mapema kwenye Mkataba huo. Mmiliki wa Kampuni hiyo, Bwana Mohamed A. Gire, alikiri mbele ya Ujumbe wa Kamati Teule uliotembelea Huston, Texas, Marekani kuwa, moja ya sababu zilizoifanya kampuni yake kusitisha shughuli zake ni kutokana na kuandamwa kwa kuandikwa kila siku na vyombo vya habari vya Tanzania. Ikamlazimu kuajiri kampuni ya *G & S Media Consultancy* ili kupunguza makali ya maumivu aliyokuwa anayapata, haikusaidia.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, inakumbushia ahadi ya Serikali ya kuanzisha mafunzo maalum, ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya kuwawezesha wanahabari kuongeza ujuzi na kujenga uzoefu wa kuhoji na kuandika habari za uchunguzi, wenye kina stahili, shughuli ambayo ni sehemu muhimu ya kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora nchini. Kuhusu *Richmond Development Company LLC* ni akina nani? Utambulisho wake Kisheria, Mkataba wa Uzalishaji Umeme wa Dharura unaiieleza kwenye utangulizi, *Richmond Development Company LLC* kuwa ni kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria za Jimbo la Texas, Marekani na yenye anuani ifuatayo: 5825 Schumacher, Huston Texas 77057, Marekani. Aidha, kifungu cha 5.1(a) cha Mkataba huo, kinatoa maelezo ya ziada kuhusu *Richmond Development Company LLC* kuwa ni kampuni yenye ukomo wa hisa (*Limited by Shares*), ambayo uwepo wake Tanzania, haukinzani na sheria za nchi. Kifungu hicho kidogo kinamalizia kwa kutamka bayana kuwa, kampuni hiyo ina nguvu na mamlaka yote stahili ya kikampuni (*all requisite corporate power and authority*) ya kumiliki au kukodisha na kutumia mali zake na kuendesha biashara zake kama ilivyokusudiwa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo sura ya *Richmond Development Company LLC*, kama ilivyoainishwa katika Mkataba huo wa kisheria, uliotiwa saina kwa upande wa *TANESCO* na aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi Mwendeshaji wa *TANESCO*, Ndugu Johannes G. Lottering na kushuhudiwa na aliyekuwa Kaimu Katibu (*Ag. Company*

*Secretary*) wa TANESCO, Ndugu Godson Makia na kwa upande wa *Richmond* na Meneja wake, Ndugu Mohamed Gire na kushuhudiwa na wakili maarufu nchini, Dr. Ringo Tenga, ambaye alijitambulisha katika mkataba huo kama Katibu wa *Richmond Development Company LLC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hadhi ya *Richmond* Kisheria au Kikampuni Marekani, uchunguzi wa kina uliofanywa na Kamati Teule, ndani na nje ya nchi na kwa msaada mkubwa wa Ubalozi wa Tanzania, Washington D.C. na Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, umetoa picha tofauti kabisa na ile iliyomo kwenye Mkataba huo. Kamati Teule imejiridhisha kuwa, hakuna kampuni yenye jina la *Richmond Development Company LLC*, iliyokuwa imesajiliwa Jimbo la Texas wakati wa kusaini Mkataba huo au iliyosajiliwa baada ya Mkataba huo, hadi tunapowasilisha ripoti hii kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 31 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Spika, hitimisho tulilofikia, linashabihiana kwa vigezo vyote na ushauri wa kitaalamu, uliotolewa na kampuni mashuhuri ya Mawakili ya Virginia, Marekani, inayoitwa *Hunton & Williams LLP*, kwa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO mwezi Oktoba, 2006. Katika ripoti yake yenye jumla ya kurasa 19, kampuni hiyo ya Mawakili imetamka bayana kuwa, hakuna kampuni yenye jina la *Richmond Development Company LLC* kwenye masjala ya Katibu wa Jimbo la Texas, ambaye moja ya majukumu yake ni sawa na ya Msajili wa Makampuni wa Tanzania.

*Hunton & Williams LLP*, wameituhumu *Richmond Development Company LLC*, kwa upotoshaji wa hadhi yake kikampuni (*misrepresentation of its corporate status*) na kutoa tamko lisilo sahihi (*incorrect statement*), kuhusu hadhi yake chini ya sheria za Texas. Ukaguzi wa kumbukumbu za Katibu wa Jimbo la Texas, uliofanywa na kampuni hiyo ya Mawakili Oktoba, 2006, ulionyesha kuwa, hakuna kampuni yenye jina la *Richmond Development Company LLC*, iliyokuwa imeanzishwa na kuendesha shughuli zake Jimboni Texas wakati huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, tarehe 10 Oktoba, 2006, gazeti la kila siku la Kiingereza linalochapishwa hapa nchini, *The Citizen*, lilimkariri afisa mmoja katika Jimbo la Texas, Bwana William Pate, akisema makampuni yote yanayofanya biashara halali Jimboni humo, yana kumbukumbu zake katika Ofisi ya Katibu wa Jimbo la Texas. Alisema ofisi hiyo haina taarifa au kumbukumbu zozote kuhusu kampuni hiyo inayojiita *Richmond Development Company LLC*.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati Teule, waliotembelea Marekani kati ya tarehe 10 na 16 Desemba, 2007, waliambiwa na Bwana Mohamed Gire kuwa, *Richmond Development Company LLC* ni jina mbadala la biashara la kampuni yake iitwayo *RDEVCO LLC*. Bwana Gire ambaye aliamua mkutano wake na Wajumbe wa Kamati Teule, ufanyike ofisini kwa wanasheria wake; *Duane Morris LLP*, waliopo 3200 Southwest Freeway, suite 3150, Jijini Huston, alisisitiza kuwa, Sheria za Texas zinawaruhusu wafanyabiashara na makampuni, kutumia majina mbadala au tofauti na yale yaliyopo kisheria, kwa sababu za kibiashara. Kamati Teule, iliyazingatia maelezo ya Bwana Gire, kwa lengo la kuyafanyia kazi.

Majimbo mengi Marekani, likiwemo la Texas, ni kweli kabisa kuwa yanaruhusu matumizi ya majina mbadala katika biashara au huduma. Kwa Kiingereza majina hayo yanaitwa “*assumed names*” au “*dba*”, kwa kirefu “*doing business as*”. Katika nchi nyingine nyingi kama vile Tanzania, Uingereza, Ireland, Australia na baadhi ya majimbo ya Marekani na sehemu za Kanada, neno linalotumika zaidi ni “*t/a*”, yaani “*trading as*”.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zote hizo, sheria zinaweka taratibu za kuzingatia ili kuepusha vitendo vya kitapeli katika matumizi ya majina mbadala ya kibiashara. Nchini Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Madola, zipo sheria maalum za usajili wa majina ya biashara tu ambapo kampuni au mfanyabiashara au mtu yeyote yule, ambaye kwa sababu za kibiashara au vinginevyo, asingependa kutumia jina lake halali katika biashara fulani, anaweza kusajili jina mbadala kwa biashara hiyo, bila kulazimika kuunda kampuni tofauti. Majina mbadala ya kibiashara hapa kwetu Tanzania, yanasajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara (*Business Names Registration Ordinance*) Sura ya 213.

Nchini Marekani vilevile, huwezi ukakurupuka tu na kuanza kutumia jina mbadala la biashara bila kupitia usajili maalum, ambao unawawezesha watu wengine kukagua jalada la majina hayo mbadala, kwa lengo la kupata utambulisho kamili wa wanayoyatumia. Vilevile, sheria zinalazimu majina hayo kuchapishwa magazetini kwa lengo la kuutaarifu umma. Lengo, kama tulivyodokeza awali ni kulinda raia wema dhidi ya vitendo vya udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Texas, ambako Bwana Gire anaishi ni kosa la jinai, kutumia jina mbadala bila kulisajili. Usajili wa jina mbadala, unadumu kwa miaka mitano, ambapo mtumiaji lazima asajili jina hilo upya kati ya tarehe 1 Januari na 31 Desemba ya mwaka wa tano.

Sasa je, ni kweli kwamba, jina la *Richmond Development Company LLC* ni jina mbadala la kampuni ya Bwana Gire, iitwayo *RDEVCO LLC*? Je, jina hilo lilisajiliwa ipasavyo? Katika kujibu maswali hayo mbele ya Mwakili wake wawili, Bwana Gire aliwakabidhi Wajumbe wa Kamati Teule, hati ya uthibitisho ya Harris County, Texas ambayo kwa maoni yake, ilikuwa inathibitisha kuwa, *Richmond Development Company LLC* ni jina mbadala la biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imeikagua hati hiyo kwa kina na kuona kuwa, badala ya kumsaidia Bwana Gire, inazidi kuthibitisha kuwa si mfanyabiashara mwadilifu, ila tapeli kwa sababu kuu mbili:-

Kwanza, mbali na kwamba hati hiyo ya Bwana Gire ni kivuli tu au nakala ya hati halisi (kama ipo), nakala ambayo haina uthibitisho wowote wa uhalali na uhalisia wake, ilikuwa ina saina ya afisa mmoja tu badala ya wawili walioainishwa katika hati hiyo. Pili, badala ya hati hiyo kutamka kuwa, *RDEVCO LLC* imesajili jina la *Richmond Development Company LLC*, kama Bwana Gire alivyotaka Kamati Teule ielewe, hadithi mpya kabisa inaanizishwa kuwa *Richmond Development Company* ni jina mbadala, lililosajiliwa na *Richmond Development Company LLC*. La kushangaza ni kuwa, katika baadhi ya barua zake alizoiandikia *TANESCO* na Wizara ya Nishati na Madini, Bwana



Gire anatamka kuwa, *Richmond Development Company* ni jina mbadala la biashara la *RDEVCO LLC*.

Mheshimiwa Spika, mtu anaweza akadanganyika akafikiri kuwa kiwango hiki cha ubabaishaji hakithibitishi utapeli pekee, bali vilevile elimu duni ya mmiliki wa kampuni hizo, Bwana Gire, inayomfanya asione hatari kubwa anayojitwalia ya hata kumfikisha jela kwa udanganyifu. Lakini kwa mfanyabiashara mzoefu aliyejizungushia mawakili wa kumtetea mambo yakimwendea mrama, anajua analolifanya. Hivyo basi, *Richmond Development Company LLC* ni kampuni ya kimakusudi, ya kimkakati ambayo haikamatiki, haishtakiki, haipigiki faini na haiadhibiki kwa lolote lile itakalolifanya, kwani haina uhai wa kikampuni (*Corporate Personality*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na Bwana Gire kuamua kufanyia mkutano wake na Wajumbe wa Kamati Teule ofisini kwa wanasheria wake na si kazini kwake mwenyewe, Wajumbe walihakikisha kuwa, wanatembelea mtaa unaotajwa kwenye Mkataba kuwa Ofisi za *Richmond Development Company LLC*, yaani 5825 Schumacher, Huston Texas, 77057, USA.

Anuani hiyo, ikawafikisha kwenye jengo lenye jina la *Richmond Printing LLC*, jina walilothibitisha kuwa la kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni yenye Ukomo wa Hisa ya Texas (*Texas Limited Liability Company Act*), tarehe 1 Agosti, 1994, kwa madhumuni ya kuendesha biashara ya uchapishaji na biashara nyingine zinazoruhusiwa na sheria kwa kampuni ya aina hiyo. Kampuni hiyo, ilianzishwa ikiwa na mwanahisa na meneja mmoja tu kwa jina Mohamed Gire.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wajumbe wa Kamati Teule, wakatambua kuwa jengo hilo la *Richmond Printing LLC*, linatumiwa vilevile kama Ofisi za *RDEVCO LLC*, kampuni ambayo ilisajiliwa chini ya sheria hiyo hiyo ya Texas tarehe 11 Septemba, 2003, ikiwa na madhumuni mapana ya kujishughulisha na biashara yoyote halali. Kampuni hiyo, vilevile ilianzishwa ikiwa na mwanahisa na meneja mmoja tu kwa jina Mohamed Gire. Tunalazimika kusema kuwa, jengo hilo vilevile ni Makao Makuu ya Kampuni hewa ya *Richmond Development Company LLC*.

Licha ya kutumia jengo moja, makampuni yote hayo yanamhusu mtu mmoja; Mohamed Gire na zinatumiwa anuani moja. Kutokana na uchambuzi huu ni wazi kuwa, maelezo yaliyomo kwenye utangulizi wa Mkataba kati ya *Richmond Development Company LLC* na *TANESCO* kuwa, chombo hicho cha biashara cha Bwana Gire ni kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria za Jimbo la Texas si sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hadhi ya *Richmond* kisheria/kikampuni Tanzania, *Richmond Development Company LLC* si jina geni Tanzania. Jina hilo lilianza kusikika nchini kwa mara ya kwanza, mwaka 2003 na kwa kishindo likihusishwa na mradi mkubwa wa takriban shilingi bilioni 400 wa ujenzi wa bomba la mafuta la urefu wa kilometa 1,150 kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika barua yake ya kujitambulisha iliyotumwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya

Petroli Tanzania (TPDC), tarehe 28 Mei, 2003, *Richmond Development Company* wakati huo ikijiita kwa kifupi RDC, ikajitambulisha kuwa kampuni yenye uzoefu wa zaidi ya miaka 25 katika miradi ya nishati na kwamba, imekamilisha miradi mbalimbali ya aina hiyo kwa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 500 katika nchi zinazoendelea.

Kutokana na wasifu huo, TPDC ikawapa RDC nakala ya ripoti ya upembuzi yakinifu iliyofanywa na kampuni ya *Consulting Engineers and Planners Ltd* mwaka 1997 ili kupata taarifa za awali kuhusu mradi huo. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini, ikairuhusu RDC kuleta mapendekezo ya awali kuhusu mradi huo.

Mapema mwezi Oktoba, 2003, Wizara ikapokea mapendekezo ya awali ya mradi kutoka RDC, ambayo yalipitiwa na wataalam wa Wizara na TPDC na kukutwa na upungufu mwingi, yakiwemo kukosekana kwa tathmini za kifedha na za kiuchumi za mradi; kukosekana kwa tathmini za mazingira; na kukosekana kwa mpango wa kuwapa makazi waathirika katika njia ya bomba. Kutokana na upungufu huo, Wizara ikasita kuipa RDC mradi huo muhimu na kuitaka kampuni hiyo kwanza irekebishe upungufu wote uliojitokeza. RDC nayo ikaweka sharti la kupewa upendeleo wa kutoruhusu kampuni nyingine kwenye mradi huo kwa kipindi maalum (*Exclusivity Period*), ili kukamilisha kazi hiyo bila wasiwasi wa kunyang'anywa mradi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Juni, 2004, Mheshimiwa Daniel Yona, wakati huo Waziri wa Nishati na Madini na Bwana Mohamed Gire, wakati huo akijiita Mwenyekiti wa RDC, wakasaini mkataba wa awali (*Memorandum of Understanding*), ulioipa RDC *exclusivity period* ya miezi 18, kufanya upembuzi yakinifu wa kina. Mkataba huo, pamoja na mambo mengine, uliitaka RDC kuipa Wizara, ripoti za maendeleo ya utekelezaji wa mradi kila baada ya miezi sita na jukumu la kuhakikisha kuwa, mradi huo unatekelezwa na RDC mara baada ya zoezi la upembuzi yakinifu wa kina kufanikishwa.

Mheshimiwa Spika, tangu mkataba huo usainiwe, RDC haikuonekana tena ikijishughulisha na utekelezaji wa sehemu yake ya mkataba. Kumbukumbu za mawasiliano kati ya Wizara na kampuni hiyo, zimetawaliwa na malalamiko ya watendaji wa Wizara kuhusu ubabaishaji wa RDC. Hatimaye tarehe 9 Januari, 2006, Ndugu Bashir J. Mrindoko, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, akaiandikia barua RDC, kuitaarifu kuwa, mkataba kati yake na Wizara kuhusu bomba la mafuta, ulikoma tarehe 30 Desemba, 2005 na wawekezaji wengine sasa wanapewa fursa kuendelea na mradi huo.

Sehemu ya barua ya Katibu Mkuu inasomeka hivi: “*The Ministry of Energy and Minerals, notice with regret that throughout the 18 month exclusivity period, in spite of several reminders, the Richmond Development Company, failed to honor its obligations as provided for in Articles 2.1 and 2.2 of the Memorandum.*” Wizara inasikitika kuwa, kwa kipindi chote cha miezi 18 ya upendeleo, *Richmond Development Company*, pamoja na kukumbushwa mara kwa mara, ilishindwa kuheshimu wajibu wake kama ulivyoainishwa katika Ibara ya 2.1 na 2.2 ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, ninaomba turejee kwenye hoja ya awali ya kupima ukweli uliomo kwenye kifungu cha 5.1(a) cha Mkataba kati ya TANESCO na kampuni hiyo ya

*Richmond*, tulichokinukuu awali kinachosema, *Richmond Development Company LLC* ni kampuni yenye ukomo wa hisa ambayo uwepo wake Tanzania, haukinzani na sheria za nchi na kwamba, kampuni hiyo ina nguvu na mamlaka yote stahili ya kikampuni ya kumiliki au kukodisha na kutumia mali zake na kuendesha biashara zake nchini. Katika kupima ukweli wa kauli hizo ndani ya Mkataba, kikwazo kikubwa cha mwanzo ambacho Kamati Teule ilikipata, kilikuwa ni msingi wa kuichunguza *Richmond Development Company LLC* kama kampuni, wakati uhalali wake kama kampuni huko ilikotoka, unabishaniwa au kwa lugha iliyonyooka, haupo. *Richmond Development Company LLC*, kwa maneno mengine si kampuni ya mchana bali ya usiku, kampuni ya mfukoni au ya sanduku la barua (*mail box company*)! Hiyo ndiyo kampuni ambayo Shirika la Umma (*TANESCO*), iliingia nayo mkataba wa mabilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Wanasheria ya Kimarekani ya *Hunton & Williams LLP*, iliyopewa kazi na Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO* kuichunguza *Richmond Development Company LLC*, kama tulivyoeleza hapo awali, inathibitisha kuwa, tarehe 23 Juni, 2006, siku ambayo Mkataba huo ulisainiwa, *Richmond Development Company LLC* haikuwa na nguvu za kisheria, wala mamlaka yoyote ya kikampuni, kuiwezesha kuendesha shughuli zake Tanzania. Kamati inaamini kuwa, wamiliki au waendeshaji wa kampuni hiyo, wanaotambulishwa kwenye tovuti ya kampuni hiyo (*www.rdevco.com*), Bwana Mohamed A. Gire na Dk. Mohamed S. Huque, waliliona tatizo hilo na kuamua siku 19 tu baada ya kusainiwa kwa Mkataba huo, kusajili kampuni mpya kwa jina la *Richmond Development Company (T) Limited*, yenye Makao yake Makuu Jijini Dar es Salaam.

Kampuni hiyo mpya, ilisajiliwa tarehe 12 Julai, 2006 na kupewa Hati ya Usajili nambari 57014, ikiwa na wanahisa wawili, kwa majina: *Richmond Development Company LLC* yenye anuani ya 5825 Schumacher (tunadhani ni *Schumacher*), Huston – Texas 778057, USA (hisa 750,000); na Naeem Gire wa S.L.P. 1998, Dar es Salaam (hisa 250,000).

Mheshimiwa Spika, kwa kusajili kampuni hiyo mpya, ni dhahiri kuwa, wamiliki wa kampuni hiyo, walitaka wasibanwe na Kifungu cha 434 cha Sheria ya Makampuni ya Tanzania Na. 12 ya 2002, kinachotamka wazi kuwa, makampuni yote ya nje, ambayo yanaanzisha ndani ya nchi mahali pa biashara (*a place of business*), yanawajibika kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni, taarifa mbalimbali za kampuni ndani ya siku 30 toka zianzishe mahali pa biashara, kama vile sheria au mkataba unaoelezea muundo wa kampuni (*Charter, Statutes or Memorandum and Articles of Association*); orodha ya Wakurugenzi na Katibu wa kampuni; anuani kamili ya ofisi kuu ya kampuni; na nakala ya taarifa ya mahesabu ya kampuni na shughuli za kampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza masharti yote chini ya kifungu cha 434 cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kampuni ya nje itathibitishwa na Msajili wa Makampuni kuwa imetimiza masharti. Uthibitisho huo, utakuwa ushahidi kamili wa usajili wa kampuni hiyo ya kigeni nchini, ambao utaipa kampuni hiyo haki sawa na kampuni iliyosajiliwa Tanzania katika kumiliki ardhi. Hii ni dhahiri kuwa, taarifa zinazodaiwa chini ya kifungu hicho cha sheria, zisingeweza kutolewa na *Richmond Development Company LLC*, kwa sababu kampuni hiyo isiyo na usajili stahili Marekani, haiwezi kuwa

nazo. Pamoja na juhudi hizo za wamiliki wa Kampuni ya *Richmond*, Kamati Teule ilibaini kutokana na ushauri mbalimbali iliopata wa kisheria kuwa, tatizo la uhalali wa *Richmond* ya Tanzania lilikuwa palepale, kwani kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Makampuni, kinataka watu wawili au zaidi kuwa na uwezo wa kufungua kampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mmoja wa wanahisa waliofungua kampuni hiyo ya *Richmond* ya Tanzania ni *Richmond Development Company LLC* ya Marekani (yenye asilimia 75 ya hisa zote za kampuni hiyo iliyosajiliwa Tanzania); na kwa kuwa, kampuni hiyo ya Kimarekani haijasajiliwa Marekani wala hapa Tanzania, kwa mujibu wa kifungu cha 434 cha Sheria ya Makampuni; na kwa kuwa, kutokana na hiyo sababu, kampuni hiyo ya Kimarekani haina nguvu wala mamlaka stahili ya kikampuni; *Richmond Development Company (T) Limited* ina mwanahisa mmoja tu kwa jina Naeem Gire, hali ambayo haikubaliki kisheria. Hii ni wazi kuwa, picha iliyojengwa kwenye Mkataba tunaouongelea hapa, kuhusu hadhi na uhalali wa *Richmond Development Company LLC* nchini Tanzania, ilikuwa ya kisanii, ya uongo na isiyo na msingi wowote kisheria. Kinachosikitisha hapa ni kuwa, mwezi Februari, 2006, yaani mwezi moja tu baada ya Wizara ya Nishati na Madini, kuiandikia barua *Richmond Development Company LLC* kuwa haina imani na kampuni hiyo ya Bwana Gire, ikajitosa kwenye zabuni nyingine ya Wizara hiyo hiyo ya Nishati na Madini, zabuni ya kuingiza nchini jenereta za kuzalishia umeme wa dharura wa Megawati 100.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezo wa *Richmond* kifedha, kitaaluma na kiutendaji, tumeeleza kuwa, *Richmond Development Company LLC* iliweza kuaminiwa na Serikali kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa mradi wa bomba la mafuta la Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kujitambulisha kuwa: -

- (a) Kampuni hiyo ina uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 25 katika kuendeleza miradi ya nishati.
- (b) Kampuni hiyo, inaaminiwa na taasisi mbalimbali za biashara na fedha za Marekani na ina mahusiano ya karibu na Serikali ya Marekani.
- (c) Kampuni hiyo imekamilisha miradi mikubwa ifuatayo duniani; kituo cha umeme cha MW 130 cha Gaziantep, Uturuki (gharama za mradi \$117 milioni) na utafutaji wa mafuta na gesi Kusini Mashariki mwa Ulaya (\$150 milioni).

Mheshimiwa Spika, Serikali ingejaribu kuzichunguza sifa hizo za rejareja za *Richmond Development Company LLC*, hata kwa kuuandikia Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam au kukagua tovuti yake ([www.rdevco.com](http://www.rdevco.com)), ukweli ungelidhihirika kuwa, kampuni hiyo si chochote wala lolote. Tovuti yake yenyewe, imesheheni makosa madogo madogo ya Kiingereza na kupambwa na taarifa za juu juu za miradi ambayo kampuni hiyo inadai kuitekeleza hivyo, kuzua maswali mengi na hali inayoashiria upeo mdogo kielimu wa wamiliki wa kampuni hiyo.

Kwa mfano, ukurasa wa kwanza wa tovuti hiyo iliyoandaliwa mwaka 2004, unabeba dhamira mbili za kampuni, lakini dhamira ya kwanza haieleweki, inahitaji mpangilio

mpya wa sentensi kwa Kiingereza sanifu. Mbali na makosa madogo madogo ya kisarufi na mpangilio, ambayo yamepamba kurasa zote 11 za tovuti hiyo, ukurasa wa saba, unaorodhesha miradi mbalimbali ambayo kampuni hiyo ilikuwa inatekeleza; ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo, unaoweza kuchukua watazamani 65,000; ujenzi wa bomba la mafuta la kilometa 1,150; na ukarabati wa viwanja mbalimbali vya ndege nchini Tanzania. Miradi yote hiyo, ilikuwa porojo tupu ambazo watendaji wetu Serikalini, hawakustahili kuzifumbia macho.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyotarajiwa, kampuni hiyo ikashindwa kutekeleza sehemu yake ya Mkataba. Mashahidi kadhaa, walioongea na Kamati Teule wakati wa uchunguzi, walisema ingelikuwa maajabu kwa kampuni ya aina hiyo, iliyokuwa haina uwezo kifedha hata wa kuwasafirisha wawakilishi wao kwenda Afrika ya Kusini, kwa mazungumzo ya kutafuta fedha za mradi, kampuni iliyokuwa haina uelewa stahili wa masuala ya nishati na iliyokosa rekodi nzuri ya utendaji, kufanikisha mradi huo. Kwa hali ya kawaida, kampuni yoyote inayoshindwa kutekeleza masharti ya mkataba na Serikali, inalazimika kukaa pembeni kwa muda, kusubiri angalau upungufu wake usahaulike kidogo. Aidha, muda ambao kampuni hiyo itakuwa imekaa pembeni, utachukuliwa na waungwana kuwa wa kujisahihisha, wa kurekebisha mapungufu na kuweza kuaminiwa tena. Si kawaida kwa kampuni iliyoshindwa kutekeleza kazi moja ya mteja, kurejea muda mfupi baadaye kutafuta kazi nyingine, tena yenye unyeti mkubwa kwa mteja huyo huyo bila kigugumizi wala soni.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, kwa *Richmond Development Company LLC* kuingia kwenye mchakato wa zabuni nyingine ya Wizara ya Nishati na Madini hata kabla wino kwenye barua iliyoandikiwa na Wizara, ikilalamikia utendaji kazi wake haujakauka sawasawa na kwa Wizara kufumbia macho ubabaishaji bayana wa kampuni hiyo na kuiruhusu kushiriki kwenye zabuni ya umeme wa dharura, inayohitaji uzoefu maalum bila wasiwasi wa madhara ambayo yangeweza kutokea kwa Taifa, hisia za maslahi binafsi ya baadhi ya Viongozi wa Serikali, hazikwepeki.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; Kamati Teule, imeuchambua kwa kina mchakato mzima wa zabuni ya uzalishaji umeme wa dharura, ulioipa ushindi *Richmond Development Company LLC* ya Huston, Texas, Marekani, mapema mwaka 2006, ili kuzitolea majibu yaliyokamilika, hadidu za rejea zote sita, ambazo Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samuel J. Sitta, aliipa Kamati Teule tarehe 15 Novemba, 2007 Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kurasa zote 165 za Taarifa kubwa ya Uchunguzi ya Kamati Teule ambayo inatokana na kazi kubwa ya kuwahoji jumla ya mashahidi 75, kuwauliza maswali 2,717 na kupitia nyaraka 104, zimebeba ushahidi usio na mashaka yoyote kwamba Wizara ya Nishati na Madini, iliibebe *Richmond Development Company LLC* kutoka mwanzo wa mchakato wa zabuni hadi mwisho. Kwa kufanya hivyo Wizara, kwa kutokufuata misingi ya utawala bora, ikachangia kwa kiasi kikubwa urefushaji wa mgao wa umeme ulioathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii nchini. Kamati Teule, imeridhika kuwa, ukiukwaji huo, unaweza kuwa ulichangiwa na hoja ya kukidhi maslahi binafsi. Pengine ndiyo sababu ya Wizara hii, kuonyesha tabia ambayo haikuonyeshwa na

Wizara nyingine ya kukataa katakata, kuiruhusu Kamati Teule kuona majalada ya Wizara hiyo, yenye mawasiliano kuhusu zabuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari tu, tumeonyesha katika sehemu ya pili ya Taarifa hii, jinsi Wizara ya Nishati na Madini, ilivyopindisha maamuzi ya Baraza la Mawaziri, kwa kusitisha mpango uliokuwa umekaribia utekelezaji wa kuzalisha umeme kupitia mitambo ya kukodi ya Kampuni ya *CDC Globeleq*, bila kuufikisha ujumbe wa Serikali kwa kampuni hiyo wa kurekebisha masharti yao ili mradi huo utekelezwe. Hayo yamefanyika siku ileile Baraza la Mawaziri lilipotoa maagizo na siku nne baada ya kuanza mgao wa umeme kwa mikoa yote ya Tanzania Bara, inayounganishwa na Gridi na Taifa.

Tumeonyesha vilevile, maamuzi yenye jeuri na kiburi ya kukiuka kwa makusudi, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, licha ya Baraza la Mawaziri kuisitiza kwamba, Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake, izingatiwe. Kama vile Wizara hiyo haihusiki kabisa na Utawala wa Sheria na Utawala Bora, ikailazimisha *TANESCO* isiheshimu ushauri wa kitaalam wa Mamlaka ya Udhubiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*) na kuingilia mchakato wa zabuni wa *procurement entity* nyingine kwa kuiweka pembeni Bodi ya Zabuni ya *TANESCO*, kuiagiza *TANESCO* ivunje sheria kwa kuwabadilisha Wajumbe wa Bodi yake ya Zabuni na Wizara kufanya maamuzi ya ununuzi kwa niaba ya *TANESCO* na kuulazimisha Uongozi wake kusaini mkataba na kampuni ambayo *TANESCO* waliikataa mara tatu, kwa vigezo vya kitaalam kuwa, haifai kwa kazi hiyo; huo ulikuwa udhalilishaji mkubwa wa Viongozi na Watendaji ndani ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, tumebainisha kuwa, mwezi mmoja tu kabla ya hiyo zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura, Wizara ya Nishati na Madini, ilikuwa imeandikia *Richmond Development Company LLC*, kuitaarifu kuwa, imeshindwa kutekeleza mkataba baina yake na Wizara, kuhusu mradi wa bomba la mafuta. Kimya cha Wizara kuhusu udhaifu wa *Richmond Development Company LLC*, kuliipa Kamati Teule mashaka, kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Wizara hiyo.

Tumeonyesha vilevile kuwa, *Richmond Development Company LLC*, ilikingiwa kifua na kufunguliwa kila mlango na Wizara; majaribio ya *Richmond Development Company LLC*, kubadilisha masharti ya Barua ya Dhamana ya Benki (*LC*), yaliungwa mkono na Wizara ya Nishati na Madini, kwa hamasa kubwa kiasi cha kupuuzwa maelekezo ya Wizara ya Fedha, kwa kulazimisha kufanya mabadiliko katika *LC* hiyo, nje ya mkataba wa makubaliano wa fedha kwenye akaunti ya *Escrow*.

Tumenukuu na kuambatanisha kwenye Taarifa hii, barua mbili zilizoandikwa na Wizara hizi mbili, tarehe 6 Oktoba, 2006, zikionyesha hamasa iliyoigubika Wizara ya Nishati na Madini, kuisadia *Richmond* bila hata kujali maslahi ya Taifa. Tumeonyesha hata jinsi *Richmond Development Company LLC* ilivyoanza kazi, bila kujiandikisha Bodi ya Usajili ya Makandarasi na wahandisi wake, kuacha kujiandikisha Bodi ya Usajili ya Wahandisi na jinsi Wizara ya Nishati na Madini, ilivyokuwa wima kuitetea kampuni hiyo ya Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati Teule imejionea jinsi *Richmond Development Company (T) Ltd*, kampuni tanzu ya *Richmond Development Company LLC*, ilivyopata *Certificate of Incentives* kutoka *Tanzania Investment Centre*, bila kukidhi masharti ya msingi kama vile ushahidi wa mtaji wa kutosha kutekeleza mradi. Hatimaye, TANESCO walipotaka kuuvunja mkataba kati yao na *Richmond Development Company LLC*, kwa kampuni hiyo ya Kimarekani kushindwa kutekeleza sehemu yake ya mkataba na kwa kutoa taarifa za uongo kuhusu hadhi ya kampuni hiyo ni Wizara ya Nishati na Madini iliyoingilia kati na bila aibu, kuwezesha Mkataba huo urithiwe na kampuni nyingine katika kipindi ambacho nchi ilikuwa haihitaji kabisa umeme wa ziada, licha ya kuwepo fursa za wazi kisheria kwa TANESCO kuvunja mkataba huo bila ya athari za hasara zozote.

Mheshimiwa Spika, ubebwaji wa *Richmond Development Company LLC* na Wizara ya Nishati na Madini, ulichangiwa na kurahisishwa zaidi na ukosefu wa umakini wa maafisa ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambao badala ya kuwa Washauri wa Sheria wa Serikali, wanageuka kuwa wasindikizaji!

Taarifa hii imesheheni mifano ya matukio mbalimbali ya majadiliano, ambayo Mwanasheria wa Serikali au Wawakilishi wake hawafiki hivyo, kukosa uelewa mpana wa michakato mbalimbali. Hata wakifika, mchango wao wa kuilinda nchi dhidi ya vifungu vya sheria vya kutumaliza, hauonekani.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la *Richmond Development Company LLC*, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ilichangia sana kulea ubabaishaji kwa kutohudhuria vikao vya majadiliano na kufumbia macho dosari bayana au pengine kutojali. Mahojiano ya Kamati Teule na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwakilishi wake kwenye majadiliano ya mikataba, yanajieleza yenyewe katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) za tarehe 30 Novemba, 2006 na tarehe 5 Desemba, 2007.

Ulikuwa wajibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kugundua kuwa, *Richmond Development Company LLC* si kampuni yenye ukomo wa hisa. Ulikuwa wajibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuieleza Wizara ya Nishati na Madini kuwa, Sheria ya Ununuzi wa Umma, inataka kampuni inayoshinda kwa kigezo cha bei ya chini, kufanyiwa *post qualification*, uchunguzi wa kina baada ya kuteuliwa. Ulikuwa wajibu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuishauri Serikali kuwa, *business card* na karatasi walizoonyesha *Richmond Development Company LLC*, haviwezi kuwa mbadala wa *Consortium Agreement* kati yake na *Pratt & Whitney* ya utekelezaji wa mradi huo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, utetezi mkuu uliotolewa na Viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini ni kwamba, nchi ilikuwa katika dharura hivyo, ilibidi Wizara ichukue hatua ilizochukua na kwamba, Kanuni ya 42 ya *Public Procurement (Goods, Works, Non-consultant Services and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations, 2005*, inairuhusu Wizara kuingilia kati mchakato kwenye taasisi yake. Kamati Teule, iliyakataa maelezo haya kwani yanapotosha maana halisi ya *emergency procurement* chini ya Kanuni ya 42.

Kanuni hiyo ni kweli kuwa inatoa mwanya na uhuru mpana zaidi wa maamuzi, lakini uhuru huo ni kwa taasisi yenyewe ni makosa kwa taasisi moja ya ununuzi (*Procurement Entity*), kuingilia maamuzi ya *procurement entity* nyingine kwa kisingizio cha dharura, kama Wizara ya Nishati na Madini ilivyofanya. Ikiwa Wizara ilitaka ifanye kazi hiyo yenyewe, kwa nini basi isisaini Mkataba na *Richmond Development Company LLC* yenyewe as a *procurement entity*, badala yake kuibambikizia TANESCO mzigo ambao haukuwa wake?

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule sasa inaelewa chimbuko la tabia mbaya iliyoenea nchini ya ajali ikitokea watu kukimbilia kusaidia, lakini si wote wenye dhamira ya kusaidia, kuokoa. Baadhi yao lengo kuu ni kuiba/kupora! Viongozi tunaobuni miradi kutokana na majanga ya kitaifa, hatuna tofauti na watu wanaokimbilia ajali kama waokoaji kumbe wezi. Ukame nchini ulitabirika, lakini hatukuchukua hatua mapema pengine kwa kusubiri janga kubwa litokee ili kupata fursa ya miradi ya akina *Richmond*.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, iliyaona mawasiliano ya karibu kati ya Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini katika hatua mbalimbali za zabuni hiyo. Kwa kuwa Waziri wa Nishati na Madini aliyekuwepo awali, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Arthur Mwakupugi, hawakukiri kutumwa au kuagizwa kuibeba kampuni hiyo ya Kimarekani, kwa mfumo wa uongozi na Utawala Bora, wanawajibika wenyewe kama ambavyo Waziri Mkuu atapima wadau kivyake.

Mheshimiwa Spika, ifikapo mwaka 2025, Tanzania inatakiwa iwe imeondoka kwenye kundi la nchi za kipato cha chini (*low-income countries*) na kuingia katika kundi la nchi za kipato cha kati (*middle-income countries*). Kipato cha Watanzania, kinategemewa kupanda kutoka Dola za Kimarekani 210 kwa mwaka kilichopo sasa hadi Dola za Kimarekani 3,420 kwa mwaka. Kwa fedha ya Tanzania ni kutoka Sh.262,500/= hadi Sh.4,275,000/= kwa mwaka. Kama Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyosema, maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana, kila mtu atimize wajibu wake.

Moja ya sifa kuu za nchi za kipato cha kati ni kilimo cha kisasa na maendeleo ya kati ya viwanda, shughuli ambazo haziendi bila nishati ya kutosha na ya bei nafuu. Msingi wa kujenga uwezo wa kutosha wa nishati ili kuendeshea viwanda, unatakiwa uanze kujengwa sasa na si baadaye.

Kamati Teule, inakubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara katika Taarifa yake kwa Bunge kwa mwaka 2006 kuwa, Serikali sasa iandae mpango madhubuti wa muda wa kati na mrefu (*Power System Master Plan*), ukionyesha ni namna gani nchi itatekeleza na kukabiliana na tatizo la mfumo mzima wa uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, mpango wa aina hii, utaipunguzia Serikali gharama ya kuingia mikataba ya dharura mara kwa mara kila kukitokea ukame. Aidha, mpango huo



ujumuishe pamoja miradi kama ya *Stigglers George* ya kuzalisha umeme wa *MW 2100* na zaidi, makaa ya mawe ya Mchuchuma, umeme wa nishati ya gesi asilia, upepo, jua, taka na kadhalika. Hapo tutakuwa tumejijengea msingi mzuri wa kupokea changamoto za maendeleo ya nchi za kipato cha kati.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie kwa kusoma mapendekezo ya Kamati kabla muda haujaisha na kulazimika kuongeza muda mwingine. Kuhusu Mapendekezo ya Kamati Teule, kutokana na uchunguzi wa kina, tuliainisha katika taarifa hii. Kamati Teule imejiridhisha na hivyo inatamka bayana mbele ya Bunge Tukufu kuwa, mchakato wa zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura wa *MW 100*, uliopelekea *Richmond Development Company LLC* kuteuliwa na hivyo kusaini Mkataba na Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*), tarehe 23 Juni, 2006 na baadaye kurithiwa na *Dowans Holdings S.A* tarehe 23 Desemba 2006, uligubikwa na vitendo vya ukiukwaji taratibu, kanuni na sheria za nchi na hivyo kujenga kwingu cha mashaka ya upendeleo, ubadhirifu na rushwa, ambavyo vimechangia kumwongezea mwananchi mzigo wa gharama za umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati Teule imethibitisha bila ya shaka kuwa, uteuzi wa Kampuni dhaifu kifedha, kiufundi na kiuzoefu na ambayo haina usajili Marekani wala Tanzania, kama kampuni yenye ukomo wa hisa, yaani *Richmond Development Company LLC*, ulitokana na kubebwa bila woga wala aibu na Viongozi Waandamizi wa Serikali. Kutokana na msingi huo, Kamati Teule inapendekeza yafuatayo:-

1. Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 (*Public Procurement Act, 2004*), haina nguvu ya kutosha ya kuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*), kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kwamba, Ununuzi wa Umma unaboreshwa kwa kuongeza ushindani wa ukweli na uwazi na hivyo kuipa Serikali thamani halisi ya pesa zake.

Kamati Teule, inapendekeza kwamba, sheria hii ipitiwe upya ili kuiboresha kwa kuipa Mamlaka, nguvu zaidi za udhibiti na uwezo wa kuchukua hatua pale Sheria na Kanuni zinapokiukwa, badala ya kutoa ushauri tu kama ilivyo sasa. (*Makofi*)

2. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma isiwajibike; Wizara ya Fedha ambayo nayo ni taasisi ya ununuzi (*Procurement Entity*), badala yake iwe chombo huru kinachowajibika Ofisi ya Rais na taarifa zake kuwasilishwa Bungeni. (*Makofi*)

3. Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC* na sasa *Dowans Holdings S.A*, kama ilivyo mikataba kati ya *TANESCO* na *IPTL*, *SONGAS*, *AGGREKO* na *Alstom Power Rentals*, inatoa unafuu usiostahili kwa makampuni hayo ya umeme na kuiumiza *TANESCO* na hatimaye watumiaji na walipa kodi nchini. Kwa mfano, mikataba hiyo kuwa na vipengele vya kuibana *TANESCO*, kuyalipia makampuni hayo kodi zinazohusika na uendeshaji (*operations*), matengenezo/marekebisho ya mara kwa mara ya mitambo (*maintenance*), gharama za bima, ada za mawakili na washauri elekezi (*consultants*), gharama za mafuta na gesi ya kuendeshea mitambo na gharama za ukodishaji mitambo (*capacity charges*), ambazo *TANESCO* hulipa kila mwezi si chini ya wastani wa shilingi bilioni mbili kwa kila kampuni, izalishe au isizalishe umeme.

Kamati Teule, inatoa rai kwa Serikali kuwa mikataba yote hii ipitiwe upya mapema iwezekanavyo, kama ambavyo mikataba ya madini inavyopitiwa upya sasa na Serikali. Bila kufanya hivyo, mzigo mkubwa wa gharama za umeme, utawaelelea wananchi na kushindwa kufikia azma ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania. (Makofi)

4. Mkataba kati ya TANESCO na *Richmond Development Company LLC*, ulikuwa wa uzalishaji umeme wa dharura, kipindi ambacho nchi ilikuwa katika hali ngumu ya ukame uliokausha mabwawa yote ya kuzalishia umeme. Kamati Teule, inaitaka Serikali kutathmini upya uhalali wa kuwepo na kuendelea kuwepo na Mkataba huo kutokana na udanganyifu bayana uliofanywa na *Richmond Development Company LLC*, kuhusu uwezo wake kifedha, kiufundi na uzoefu wake katika masuala ya uzalishaji umeme; usajili na uwepo wake kisheria kama kampuni halali, yenye ukomo wa hisa nchini Marekani na Tanzania; uhusiano wake kisheria na Kampuni kubwa ya Kimataifa ya *Pratt & Whitney* na utambulisho wa Mzungu mmoja kwa jina la John Perun, kama mwakilishi wa *Pratt & Whitney*; mambo ambayo Kampuni hiyo kubwa ya Kimataifa imeyakanusha vikali.

5. Mkataba kati ya TANESCO na *Richmond Development Company LLC* na sasa *Dowans Holdings S.A.*, umesheheni makosa mengi ya kisheria, yanayoashiria udhaifu mkubwa wa kitaalamu katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au ukosefu wa umakini ama ubinafsi katika kuiwakilisha Serikali.

Kwa mfano, kushindwa kutambua ukosefu wa sifa za kikampuni za *Richmond Development Company LLC*; kushindwa kuishauri Serikali kuifanyia kampuni hiyo ukaguzi wa awali (*Due Diligence*) au ukaguzi baada ya uteuzi (*Post Qualification*); kushindwa kutambua tofauti kati ya *consortium agreement* na *proprietary information agreement*; kushindwa kuona dosari kisheria za *proprietary information agreement*; kushindwa kuona tofauti kisheria kati ya *Richmond Development Company LLC*, *RDEVCO*, *RDVECO* na *RDC*; majina ambayo wamiliki wa *Richmond Development Company LLC* walikuwa wanayatumia kwa kubadilisha badilisha (*interchangeably*) kwa makusudi; kushindwa kuwashauri Wajumbe wa *GNT* kwamba, *business card* si mbadala wa hati mahsusi kisheria; kushindwa kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa, muhtasari wa majadiliano kati ya Kamati ya Serikali ya Majadiliano (*GNT*) na *Richmond Development Company LLC*, ambao ulizingatia baadhi ya maslahi ya nchi, uwe sehemu ya Mkataba kati ya TANESCO na *Richmond Development Company LLC*; kushindwa kuishauri Serikali kutumia fursa iliyokuwepo wazi ya kuvunja Mkataba baada ya *Richmond Development Company LLC*, kushindwa kutekeleza sehemu yake ya Mkataba; kushindwa kuhudhuria idadi kubwa ya vikao muhimu vya majadiliano na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumeainisha matatizo mengi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nitayasoma; Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye katika majadiliano yake na Kamati Teule alionyesha kutokuelewa kabisa kilichokuwa kinatendeka na wasaidizi wake kule chini na mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili wa Serikali, Ndugu Donald Chidowu, ambaye ushiriki wake katika *GNT* haukuwa na tija yoyote, tunapendekeza wawajibishwe na Mamlaka ya juu ya nchi, kwa kuchangia kuiingiza nchi katika Mkataba wa aibu. (Makofi)

6. Katika mikataba yote na makampuni ya nje, Serikali ihakikishe kuwa, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*BRELA*), inatumika kikamilifu katika kupata taarifa kamili za makampuni hayo, kama vile wanahisa, mitaji na anwani. Aidha, Ofisi zetu za Ubalazi zilizo sehemu mbalimbali Duniani, zihusishwe katika majadiliano na makampuni yanayotoka nje ya nchi, kwa lengo la kupata taarifa zao za msingi na kuboresha nguvu ya hoja ya Serikali.

7. Madhumuni ya Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*, yalikuwa kuzalisha umeme wa dharura kwa kipindi cha miezi kumi na mbili tu. Uamuzi wa *GNT* kuweka miezi 24 ni uamuzi ambao haujaitetea Taifa tija. Muda huo ungeweza kuongezwa baada ya kutathmini hali ya ongezeko la maji katika mabwawa ya kuzalishia umeme nchini. Kabla ya muda wa tathmini hiyo kufikiwa, wakati majadiliano yakiendelea, *GNT* ikaiongezea *Richmond Development Company LLC* muda wa kukodi mitambo hiyo kuwa miaka miwili. Kamati Teule, haikuona vielelezo vyovyote vilivyojenga uhalali kwa *GNT* kuongeza muda huo. Uamuzi huo umeliongezea Taifa mzigo mkubwa wa gharama zisizokuwa za lazima. Mathalani, kwa upande wa *capacity charges* tu, *TANESCO* itailipa *Dowans Holdings S.A*, jumla ya shilingi bilioni 54.8 kwa kipindi kilichoongezwa cha mwaka mmoja.

Aidha, *GNT* ilishindwa kutambua ulaghai wa *Richmond Development Company LLC*, kuhusu mwakilishi wa *Pratt & Whitney* na hivyo, kuamini karatasi ambayo ilikuwa haijathibitishwa na mawakili na *diskette* zenye picha za mitambo ya *Pratt & Whitney*; vielelezo ambavyo Kamati Teule imegundua na kuthibitisha kuwa, vilikuwa vya kugushi. Vilevile bila kujali kwamba, *TANESCO* ingelezimika kuilipa *Richmond Development Company LLC*, shilingi milioni 152 kwa siku, kama gharama ya kuweka vifaa vyao nchini, *GNT* ikakubali kilegelege kuitoa *Richmond Development Company LLC* shilingi milioni 12 tu kwa siku, kama fidia kwa ucheleweshaji wa kuanza kuzalisha umeme kulingana na tarehe iliyokubalika kwenye Mkataba. Kamati Teule inapendekeza kuwa, Wajumbe wote wa *GNT*, ambao ni Maafisa Waandamizi wa Serikali, wawajibishwe mara moja kwa kushindwa kutumia elimu na ujuzi wao kulinda maslahi ya Taifa.

8. Pamoja na Uongozi wa *TANESCO* kubainisha mapungufu ya *Richmond Development Company LLC* na kutoa *notice* tarehe 27 Octoba, 2006 ya kusitisha Mkataba tena kwa ushauri mahususi kutoka Kampuni ya Kimataifa ya Mawakili, Wizara ya Nishati na Madini, haikuupenda mwelekeo huo hivyo, tarehe 28 Novemba, 2006, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazir Karamagi, akiwa nje ya nchi Calgary, Canada, alimwagiza Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*, Balazi Kazaura, kuangalia uwezekano wa kuhaulisha Mkataba wa *Richmond* kwa kampuni nyingine.

Siku tano baada ya mawasiliano hayo, yaani tarehe 4 Desemba, 2006, *TANESCO* ikapokea barua kutoka *Richmond Development Company LLC*, ikielezea nia ya kampuni hiyo kutumia haki yake chini ya kifungu 15.12 cha Mkataba ili kuhamisha majukumu yake ndani ya Mkataba kwenda kwa kampuni mpya ya *Dowans Holdings S.A*. Kamati Teule, ilipata taarifa za ndani ya Wizara na *TANESCO* kuwa, Viongozi wa Wizara kama kawaida yao, waliishinikiza *TANESCO* kuridhia ombi hilo la *Richmond Development Company LLC*, kuhaulisha Mkataba kwa *Dowans Holdings S.A*.

*TANESCO* ikalazimika kuridhia uhaulishaji wa Mkataba huu, badala ya kutumia fursa iliyokuwepo ya kusitisha Mkataba baada ya kutoa *notice* ya siku thelathini.

Kamati Teule inaamini kwamba, uamuzi wa Wizara ya Nishati na Madini, kuizuia *TANESCO* isitumie fursa ya kusitisha Mkataba huo, unaashiria jinsi viongozi wetu wanavyojali zaidi faida na maslahi ya makampuni ya nje, kuliko maslahi mapana ya Taifa. Tarehe 3 Desemba, *TANESCO* kama ilivyoagizwa, ikaridhia uhaulishwaji wa Mkataba huo kwa *Dowans*, lakini kipindi ambacho hali ya maji katika mabwawa yetu ya kuzalishia umeme, ilishaanza kurejea kuwa ya kawaida. Uamuzi huo, umeingizia Taifa hasara kubwa. Hivyo basi, Kamati Teule inapendekeza kwamba, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazir Karamagi, aliyeshabikia sana uhaulishaji huo naye awajibishwe. (*Makofi*)

9. Matokeo ya uchunguzi ya Kamati Teule, kama yalivyoainishwa hapo juu, yanadhihirisha wazi jinsi Taifa lilivyotumbukizwa kwenye hasara kubwa kutokana na Mkataba huo wa *Richmond Development Company LLC* na *Dowans Holdings S.A*, kinyume na taarifa iliyotolewa na TAKUKURU (wakati huo TAKURU) kwamba, Taifa halikupata hasara yoyote. Taarifa ya TAKUKURU, ililenga kuficha ukweli (*white wash*) hivyo, ikaishia kujikanganya kwa kukiri kuwepo kwa upungufu, lakini usiokuwa na athari. Taarifa hiyo, imemong'onyoa kwa kiasi kikubwa, hadhi na heshima ya chombo hiki muhimu cha Kitaifa, kilichopewa dhamana ya kupambana na rushwa na sio kuipamba. Ili kurejesha heshima ya umma katika taasisi hiyo, Kamati Teule inapendekeza mabadiliko ya haraka ya uongozi wa taasisi hiyo. (*Makofi*)

10. Taratibu za malipo ya madai ya Mkataba wa Umeme wa Dharura, zinafanywa kupitia Barua ya Dhamana ya Benki, iliyofunguliwa kati ya *TANESCO* na Benki ya *CRDB* ya dola za Kimarekani milioni 30,696,598 tarehe 27 Desemba 2006. Kamati Teule imethibitisha kwamba, hadi kufikia tarehe 19 Juni, 2007, malipo yaliyolipwa na Benki Kuu, yamefikia Dola za Kimarekani 35,561,598, kiasi hicho ni zaidi ya Barua ya Dhamana ya Benki, kwa dola za Kimarekani milioni 4,565,000, wastani wa shilingi bilioni 5.7. Kamati Teule, inashangaa ni vipi Benki Kuu, iidhinishe malipo hayo nje ya *LLC*, Barua ya Dhamana ya Benki iliyofunguliwa kati ya *TANESCO*, *CRDB Bank* na *Dowans Holdings S.A!* Kwa kuwa Benki Kuu ndio msimamizi mkuu wa akaunti maalum (*Escrow Account*); Gavana wa Benki Kuu, pamoja na Bodi ya Wakurugenzi, wachunguze kwa makini uhalali wa malipo hayo na kuhakikisha kwamba, udhaifu wa namna hii haujitokezi tena hapo baadaye.

11. Wakati umefika sasa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995 (*Public Leadership Code of Ethics Act*), ifanyiwe marekebisho makubwa ili kudhibiti utaratibu unaoonekana wa kawaida sasa wa Viongozi Waandamizi, wenye dhamana kisiasa, kuendelea na biashara zao wakiwa madarakani hivyo, kuwaweka kwenye mtihani mkubwa wa mgongano wa kimaslahi katika maamuzi yao. Tufike mahali ambapo sheria iwalazimu, kuchagua kati ya Utumishi wa Umma au biashara binafsi. Viongozi Waandamizi wenye dhamana kisiasa (Mawaziri na kuendelea), kuendelea na biashara zao wakiwa madarakani hivyo, kuwaweka kwenye mtihani mgumu wa mgongano wa kimaslahi.

12. Serikali iondokane kabisa na utaratibu wa kutumia mawakala katika ununuzi wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini na kuhakikisha kuwa, Wizara husika ina taarifa za bei halisi ya mitambo kila wakati ili kujiepusha na mchezo wa kawaida wa mawakala kupandisha bei mara mbili au zaidi ya bei halisi. Aidha, Kamati Teule ilishuhudia bei za mitambo hiyo Jijini Huston, Texas Marekani kwa watengenezaji kiwandani, ikiwemo Kampuni ya *Kawasaki Gas Turbines – Americas*, ambayo iko chini ikilinganishwa na bei zinazotolewa na mawakala hao; jambo ambalo lingeiwezesha Serikali kununua na kumiliki badala ya kukodi kwa muda mfupi na kwa gharama kubwa. Matalani, *MW 105* zingepatikana kwa kununua mitambo sita ya *MW 175*, kila mmoja kwa gharama ya shilingi bilioni 56.25 badala ya shilingi bilioni 108.7, tulizotandikwa na *Richmond Development Company LLC*, mitambo hiyo ikibaki mali ya wakodishaji. Kwa kumalizia, Kamati Teule ilithibitisha kwamba, kauli iliyokuwa inatolewa mara kwa mara na baadhi ya viongozi wote tuliowahoji kwamba, kipindi hicho cha ukame haikuwa rahisi kupata mitambo hiyo na ilikuwa ikigombaniwa na nchi nyingi, ilikuwa sio ya ukweli na upotoshaji mkubwa.

13. Utaratibu tuliourithi kutoka kwa wakoloni na kuuzoea wa kuiona mikataba ya kibiashara kuwa ni siri hata kwa walipa kodi wenyewe na kuwa uwanja wa pekee wa watendaji, ambao Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, aliusifia Bungeni tarehe 19 Aprili, 2007 kuwa, *best practice* wakati akijibu swali la Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mbunge wa Bububu, umepitwa na wakati na unakiuka misingi ya demokrasia na uwajibikaji. Matokeo ya utaratibu huu ni kuwepo kwa mikataba mibovu, inayoficha vipengele vinavyoibebesha Taifa mizigo mikubwa ya gharama zisizokuwa za lazima, kama tulivyoainisha katika pendekezo namba tatu hapo juu.

Kamati Teule inatoa wito kwa Serikali kuondokana na utaratibu huu usio na tija kwa kuzihusisha Kamati za Kudumu za Bunge, kwenye hatua za awali za maandalizi ya mikataba hiyo. Aidha, Kamati Teule, inatoa wito kwa Kamati zote za Bunge, zihakikishe kuwa, zinapitia mikataba mikubwa na ya muda mrefu ya kibiashara chini ya sekta zao ili kuliondolea Taifa mizigo isiyo ya lazima. Pale ambapo upatikanaji wa mikataba hiyo unakwamishwa kwa urasimu usio wa lazima, Kamati zitumie utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ya kuunda Kamati Teule, yenye ufunguo wa mikataba yote iliyofichika. (*Makofi*)

14. Pamoja na dharura iliyokuwa inalikabili Taifa, Serikali haiwezi kuwa kinara wa uvunjaji wa taratibu, kanuni na sheria za nchi kwa makusudi. Kamati Teule, imeanisha katika taarifa hii vitendo vya ubabe, ujeuri na kiburi, vilivyofanywa na Viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini, alimradi kampuni waliyoitaka iteuliwe kiasi cha kupindisha hata maamuzi ya Baraza la Mawaziri bila wasiwasi wowote; kukaidi ushauri wa kitaalamu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma mara tatu mfululizo na kinyume na maagizo ya Baraza la Mawaziri, lililotaka Sheria ya Ununuzi wa Umma izingatiwe; kukiuka sheria kwa makusudi, kwa kuingilia mchakato wa zabuni wa taasisi nyingine ya ununuzi; kuvipuuza vyombo vya ndani vya maamuzi vya *TANESCO* (Bodi ya Wakurugenzi, Bodi ya Zabuni na kadhalika); kuilazimisha Bodi na Menejimenti ya *TANESCO* kuridhia maamuzi yaliyofanywa na Wizara ya kuibeba *Richmond Development Company LLC* kinyume cha sheria na taratibu na kadhalika; Wizara hiyo

katika kuibeba *Richmond Development Company LLC*, ilifikia hatua ya kupotosha kwa makusudi, ushauri wa Wizara ya Fedha, uliozuia malipo ya awali ya Dola za Kimarekani Milioni kumi katika Barua ya Dhamana ya Benki ya *Richmond Development Company LLC*.

Siku iliyopotosha ilikuwa tarehe 6 Octoba, 2006. Kamati Teule, inapendekeza kwamba, Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi, wachukuliwe hatua kali za kinidhamu kwa kuliingiza Taifa kwa makusudi, kwenye mkataba na kampuni ya mfukoni, ambao umesababisha hasara kubwa kwa nchi. Aidha, Kamishna wa Nishati, Ndugu Bashir Mrindoko, naye achukuliwe hatua za kinidhamu, kwa kushindwa kumshauri Katibu Mkuu mpya wa Wizara hiyo kuhusu udhaifu wa *Richmond Development Company LLC*, ambao ulijulikana dhahiri na Wizara toka mwaka 2004, kwenye Mkataba wa Bomba la Mafuta.

Ndugu Mrindoko, ndiye aliyeandikia barua kampuni hiyo, kusitisha Mkataba wake na Serikali mwezi mmoja tu kabla ya mchakato wa zabuni ya umeme wa dharura haujaanza. (*Makofi*)

15. Utaratibu wa kuteua Wakurugenzi na Makamishna katika Wizara kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika yaliyo chini ya Wizara, unazua mgongano wa kimaslahi, kudhoofisha usimamizi na uwajibikaji hivyo, Serikali iupige marufuku mara moja. Mfano, Kamishna wa Nishati katika hiyo Wizara ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO*, ambaye alishiriki kwenye kikao kilichowakataa wazabuni wote kuwa hawafai na kuishauri Serikali vilivyo, aliporejea Wizarani alishiriki katika kikao kutengua maamuzi ya Bodi ya *TANESCO*.

16. Uhuru mkubwa ambao Viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini waliutumia bila wasiwasi katika kuhakikisha kwamba, kampuni waliyoitaka (*Richmond Development Company LLC*), inapewa zabuni ya umeme wa dharura; maelekezo ya mara kwa mara ya Waziri Mkuu kwa Wizara katika kila hatua ya mchakato huo; upendeleo wa dhahiri ambao *Richmond Development Company LLC* iliupata kutoka taasisi mbalimbali za Serikali, kwa mfano, Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) ambacho kilifikia hatua ya kufumbia macho baadhi ya taratibu zake za msingi ili kuipa kampuni tanzu ya *Richmond Development Company LLC* cheti cha uwekezaji haraka iwezekanavyo; kutotimiza masharti ya Bodi za Makandarasi na Wahandisi na Wizara ya Nishati na Madini, kuikingia kifua kampuni hiyo isichukuliwe hatua za kisheria; uteuzi wa mwisho wa *Richmond Development Company LLC* kuwa mkandarasi kufanywa na Waziri Mkuu mwenyewe tarehe 21 Juni, 2006; uamuzi wa kuiteua *Richmond Development Company LLC* kuwa mkandarasi kusafishwa na TAKURU (sasa TAKUKURU) kuwa ulikuwa wa wazi na wa haki; uamuzi wa Serikali kuizuia *TANESCO* isivunje mkataba na kampuni hiyo licha ya sababu zote kisheria kuwepo; ni baadhi tu ya viashiria vya nguvu kubwa iliyo juu ya Wizara ya Nishati na Madini, kutumika katika suala hili na Kamati Teule kutokana na ushahidi wa kimaandishi, kimazingira na wa mdomo, inaiona nguvu hiyo kuwa ni Waziri Mkuu.

Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inatamka wazi kuwa, Waziri Mkuu ndiye mwenye madaraka ya juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hadi siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kamati Teule, haikufurahishwa hata kidogo na taarifa hizo zinazomgusa moja kwa moja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kuipendelea *Richmond Development Company LLC*.

Hata hivyo, Kamati Teule imetimiza wajibu wake, kwa uwazi na ukweli kama ilivyoagizwa na Bunge letu Tukufu. Kwa kuzingatia umuhimu wa nafasi aliyonayo Mheshimiwa Waziri Mkuu katika uendeshaji wa Shughuli za Serikali na uongozi wa nchi kwa ujumla ni wajibu wake yeye mwenyewe, kupima uzito wa matokeo ya uchunguzi huu na wajibu wake Kikatiba ndani na nje ya Bunge. Vilevile ni wajibu wa Bunge ambalo linathibitisha uteuzi wake, kwa mujibu wa Ibara ya 51 inayothibitisha uteuzi wake, kuangalia ikiwa matokeo ya uchunguzi huu hayajaathiri hadhi na uzito wake ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, Kamati Teule ya Bunge ilifadhaishwa sana na tabia ya baadhi ya Watendaji wa Serikali ya kukaidi amri ya kuwasilisha nyaraka zinazohitajika na Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, inaliomba Bunge litafakari kitendo cha aina hii na kufikiria hatua za kuchukua dhidi ya watendaji wa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kurudia kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu, kwa kutupa heshima hii kubwa ya kuunda Kamati Teule ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuishukuru Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa ushirikiano wake mzuri ambao uliwezesha Kamati hii kupata taarifa mbalimbali. Vilevile ninaushukuru Ubalozi wa Tanzania wa Washington D.C, Marekani kwa kuwawezesha baadhi ya Wajumbe wa Kamati hii, waliosafiri kwenda Marekani kufanya kazi yao kwa ufanisi. Ninakishukuru Chama cha Uwekezaji cha Watanzania waishio Marekani (*Tanzanian American Investment Forum - TAIF*), chini ya Mwenyekiti wake Dr. Lenard Tenende, kwa mapokezi mazuri ya Wajumbe wa Kamati Teule walipozuru Huston, Texas - Marekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba vilevile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo na Wajumbe wake wote, kwa kusimama kidete, kuhakikisha kuwa, kamati yao inapata majibu kupitia Kamati Teule ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee na pongezi, ziwaendee waandishi wa habari na vyombo vyao, walioweka maslahi binafsi pembeni na kupiga kelele kwa nguvu zao zote, kuhusu mwenendo uliokuwa hauridhishi wa mchakato wa zabuni ya umeme wa dharura.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati Teule, ninaomba nichukue fursa hii, kumpa pole mwandishi mahiri na jasiri, Ndugu Saed Kubenea na mwenzake Ndugu

Ndimara Tegambwage, kwa mkasa wa kushambuliwa na kuumizwa vibaya na watu tunaoamini hawafai kuitwa Watanzania.

Vilevile shukrani zetu ziende kwa Watanzania na watu wote wenye nia njema na nchi hii, waliotuunga mkono kwa kutupa taarifa mbalimbali, maoni kwa njia ya barua pepe, simu na kadhalika. (*Makofi*)

Kwa kumalizia, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L Foka, kwa kuisadia Kamati hii kufanya kazi vizuri. Aidha, shukrani za pekee zinatolewa kwa Katibu wa Kamati hii, Ndugu Anselm Mrema, akishirikiana na Ndugu Emmanuel Mpanda, Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Nenelewa Mwiambi, kwa kuisaidia Kamati kufanikisha na kumaliza kazi hii kwa ufanisi na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge likubali mapendekezo ya Kamati Teule na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati Teule ya *Richmond*. Nilikuwa ninataka niongezee tu kwamba, pia mimi kwa niaba yenu, ninapenda kumshukuru Ndugu Eliakim Mrema wa *Hansard* na timu yake, ambao wameweza kuhangaika siku mbili kukesha ili kuweza kutoa nakala za kutosha ni kazi ngumu kweli kweli. (*Makofi*)

Sasa kwa kawaida, Kamati Teule ikishawakilisha taarifa yake, kwa kuwa hakuna suala la upinzani au nafasi kwa nani ni mjadala unaendelea, labda kama ningepata taarifa ya Serikali kama wangependa baadaye kusema jambo, lakini kwa vyovyote vile, uamuzi wa Kamati ya Uongozi ni kwamba, mambo haya ni mazito na ni vyema basi tupeane nafasi ili kesho asubuhi ndio tuweze kuanza mjadala. (*Makofi*)

Sasa kabla ya hatua ya kuahirisha, nilikuwa ninapenda kusema tu kwamba, tumepokea maombi ya wasemaji 19 hadi sasa, bado nafasi ipo; Kamati ya Uongozi imetoa nafasi kwa Alhamisi nzima; kesho na Ijumaa ikibidi, tukimaliza mapema ni vizuri lakini tumeweka siku mbili ili ule Muswada mwingine wa *Financial Leasing* tuweze kuanza Jumatatu ikiwezekana. (*Makofi*)

Kabla ya kuahirisha Bunge, nina tangazo kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwamba, Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ikutane mara tukiitoka hapa katika Ukumbi wa Spika. Baada ya kusema hayo, sasa ninaliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 6.20 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi  
Tarehe 7 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)